# BUNGE LA TANZANIA

# MAJADILIANO YA BUNGE

## MKUTANO WA NANE

**Kikao cha Saba - Tarehe 21 Juni, 2007**

*(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Spika (Mhe.Samuel J. Sitta) Alisoma Dua*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge kabla ya kuingia katika Orodha ya Shughuli za Leo mtakumbuka kwamba kwa siku mbili sikuwepo hapa mezani na kazi ya kuendesha Bunge ilisimamiwa kwa umahiri mkubwa sana na Naibu Spika pamoja na Mwenyekiti Mheshimiwa Jenista Mhagama. Wote wawili ni wanawake na ni ushahidi tosha kwamba wanawake wa Tanzania wanaweza, kinachohitajika na natoa wito kwa jamii tuwape nafasi katika ngazi zote kwa sababu wanaweza. Nawashukuru sana. (*Makofi*)

## MASWALI NA MAJIBU

Na. 57

**Mfumo wa Kisiasa Nchini**

**MHE. HAJI JUMA SEREWEJI** aliuliza:-

Kwa kuwa wananchi walio wengi walipiga kura ya maoni ya kutaka mfumo wa demokrasia ya chama kimoja cha siasa, lakini Serikali ikawakatalia na kuleta mfumo wa demokrasia ya vyama vingi vya siasa; na kwa kuwa baada ya kuanzishwa kwa mfumo huo wa demokrasia ya vyama vingi, upinzani vimekuwa vikishindwa kwa kishindo sawa na mfumo wa chama kimoja cha siasa:-

(a) Je, Serikali haioni kuwa haikuwatendea haki wananchi walio wengi ambao ni sawa na asilimia 80 (80%) kuwakatalia ushindi wao?

(b) Je, sasa Serikali iko tayari kukubaliana na wananchi walio wengi wa kutaka mfumo wa chama kimoja hasa baada ya vyama vya upinzania kushindwa kwa kishindo kikubwa?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, MAAFA NA KAMPENI DHIDI YA UKIMWI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu naomba kujibu swali la Mheshimiwa Haji Juma Sereweji, Mbunge wa Mwanakwerekwe, Zanzibar, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, wananchi waliopata fursa ya kujadili suala la nchi yetu kuingia katika mfumo wa vyama vingi vya siasa au kuendelea na mfumo wa chama kimoja ulikuwepo wakati huo mwanzoni mwa miaka ya tisini walitoa maoni yao. Utaratibu uliotumika ulikuwa ni wa Serikali kuja na mapendekezo na mipango ambayo kwa lugha nyingine inaitwa *White Paper* na siyo kupiga kura kama alivyoeleza Mheshimiwa Mbunge. Maoni yalikusanywa na Tume ya Marehemu Mheshimiwa Jaji Francis Nyalali na kuwasilishwa Serikalini pamoja na mapendekezo.

Mheshimiwa Spika, ni kweli asilimia 80 ya waliotoa maoni walitaka mfumo wa chama kimoja uendelee wakati asilimia 20 iliyobaki walipendekeza mfumo wa vyama vingi.

Mheshimiwa Spika, mapendekezo ya Tume yaliyotokana na uchambuzi wa maoni ya wadau mbalimbali pamoja na hali halisi ya mazingira ya kisiasa na kiuchumi ndani na nje ya nchi yalikuwa tuingie katika mfumo wa vyama vingi. Aidha ushauri wa hekima na busara uliotolewa na Muasisi wa Taifa letu, Hayati Mwalimu Julius Kambarage Nyerere wa kuafiki mapendekezo ya Tume ulichangia sana kwa Serikali kukubali nchi yetu kuingia kwenye mfumo huo. Hivyo basi, uamuzi huo wa Serikali ulikuwa na malengo mema kwa wananchi wote na kwa msingi huo hakuna aliyeshinda wala kushindwa.

(b) Mheshimiwa Spika, uamuzi wa Serikali wa kuanzisha mfumo wa vyama vingi vya siasa bado ni wa maana katika maendeleo ya nchi yetu kwani ni dhahiri mfumo huo unakifanya chama tawala kuwa macho na kujiweka katika hali ya ushindani wakati wote kwa kuwa na sera nzuri na kuzitekeleza kwa kiwango ambacho wananchi wanaridhika. Napenda kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge na Bunge lako Tukufu kwamba mfumo wa vyama vingi uliopo kwa mujibu wa Sheria unakipa changamoto Serikali na Chama Tawala kutekeleza wajibu wao. Kadhalika Bunge letu Tukufu ni miongoni mwa Taasisi zinazopewa heshima kubwa ndani na nje ya nchi kutokana na kuwa na uwakilishi unaotokana na uchaguzi unaoendeshwa kidemokrasia na kuthibitishwa na waangalizi wengi wa kimataifa na wa ndani ya nchi kuwa ni huru, wa amani na wa haki. Hivyo basi, kwa manufaa ya Taifa na hatua iliyofikiwa haitakuwa vyema kwa wakati huu kurejea kwenye mfumo wa chama kimoja.

**MHE. HAJI JUMA SEREWEJI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kuniruhusu kuuliza swali la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Naibu Waziri nataka kuuliza swali moja la nyongeza. Kwa kuwa mfumo wa vyama vingi uchaguzi wake una gharama kubwa sana na nia ya kuleta upinzani kidogo hapa Bungeni; na hivi sasa wapinzani wana asilimia 14 tu. Je, Serikali itakuwa tayari badala ya kuweka kipindi cha

miaka mitano cha kupiga kura iwe kwa miaka saba ili kuvipa vyama vya upinzani kujipanga alau wafike asilimia 20?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, MAAFA NA KAMPENI DHIDI YA UKIMWI:** Mheshimiwa Spika, kwanza chema chochote lazima kinakuwa na gharama yake; na tuelewe kwamba taratibu hii ni kwa ajili ya kudumisha demokrasia ambayo msingi wake ni kutaka kuweka *checks and balance* ili kusiwe na uburuzwaji kwa upande wote. Suala la kuwa na kipindi cha miaka saba baada ya miaka mitano itategemea ninyi Waheshimiwa Wabunge mtakavyopendekeza lakini kwa hakika kipindi hiki cha miaka mitano kinatosha ili wananchi wasiwachoke watu wengine.

**MHE. MASOUD ABDALLAH SALIM**: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kunipa nafasi ya swali moja la nyongeza. Kwa kuwa Mheshimiwa Mbunge anavunja Katiba aliyoapa kuitetea kama inavyoeleza kwenye Ibara ya 3.1 inasema kwamba Jamhuri ya Muungano ni Nchi ya Kidemokrasia na ya Kijamaa isiyokuwa na dini, yenye kufuata mfumo wa vyama vingi vya siasa. Je, Mheshimiwa Mbunge haoni kama kuna haja ya kuomba radhi ndani ya Bunge hili Tukufu? (*Kicheko*)

**SPIKA:** Alikuwa anatoa pendekezo tu hata kama halipendezi sana lakini ni pendekezo. Swali la mwisho la nyongeza Dr. Slaa.

**MHE. DR. WILBROD P. SLAA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kuniona swali moja la nyongeza. Kwa kuwa wakati maoni ya wananchi yanakusanywa na kupata asilimia 80 ya wananchi waliosema wangependa mfumo wa chama kimoja wananchi wengi walikuwa hawana uzoefu wala elimu ya kutosha kuhusu vyama vingi. Je Serikali sasa inakubali kufanya tathmini ya kina kuona ni wananchi wangapi leo wanakubali mfumo wa vyama vingi?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, MAAFA NA KAMPENI DHIDI YA UKIMWI:** Mheshimiwa Spika, tunaamini kabisa kama wakati ule ambapo wananchi walikuwa hawana mwamko wa kuelewa faida ya kuwa na vyama vingi sasa hivi kwa hakika pamoja na kwamba kilichotumika wakati ule ili ni *white paper* naamini wengi watakubali kwamba vyama vingi ndiyo msingi wa demokrasia katika nchi yetu na hivyo watakubali hilo.

Na. 58.

**Malipo ya Kupimiwa Ardhi**

Swali namba 58 lilifutwa kwa kuwa lilishaulizwa katika Mkutano uliopita wa Saba.

Na. 59

**Madeni ya Serikali**

**MHE. MASOUD ABDALLAH SALIM** aliuliza:-

Kwa kuwa Tanzania bado inaendelea kuwa na Bajeti hivyo inahitaji mikopo na misaada toka nje katika kuimarisha uchumi wake na kupambana na umaskini na kwa kuwa baadhi ya mikopo hiyo inakuwa na riba ambazo huwa ni mzigo kwa Taifa letu:-

(a) Je, Serikali inaweza kueleza Bunge kuwa madeni yetu ni kiasi gani kwa kuweka mchanganuo wa deni la ndani na lile la nje hadi leo?

(b) Pamoja na kuwa na Bajeti tegemezi. Je, Serikali ina mkakati gani wa ziada ili kuhakikisha Taifa letu linapunguza madeni hayo ili kudhibiti ongezeko la deni linatokana na ongezeko la riba?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. ABDISALAAM ISSA KHATIB)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Fedha naomba kujibu swali la Mheshimiwa Massoud Abdallah Salim, Mbunge wa Mtambile, kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, hadi kufikia tarehe 30 Aprili 2007 deni letu lilikuwa jumla ya shilingi 5.738. trilioni kasma ifuatavyo:-

- Deni la ndani ni Shilingi bilioni 1,788.
- Deni la nje ni Sh. trilioni5,736.486 sawa na USD. 4,513. 40.

(b) Mheshimiwa Spika, mikakati ya Serikali yenye lengo la kuhakikisha kuwa deni la Serikali halipandi kwa kiasi kikubwa kutokana na ongezeko la riba ni kama ifuatavyo:-

(i) Kulipa mikopo yote kwa wakati kwa mujibu wa makubaliano na hivyo kuepuka adhabu ya riba (*penalty*).

(ii) Kukopa kutoka vyanzo vyenye masharti nafuu *(concessional sources),* ili kuliepusha Taifa na mzigo mkubwa wa malipo ya riba. Vyanzo hivyo ni kama vile Taasisi ya Benki ya Dunia, (*IDA*) na Taasisi ya Benki ya Afrika (*ADB*).

(iii) Kuendeleza utaratibu wa kufanya majadiliano na baadhi ya wadau waliopo hivi sasa ambao ni nchi rafiki kwa nia ya kupata misamaha. Majadiliano kama hayo yalishafanyika na nchi ya Libya na hatimaye Serikali yetu ikapunguziwa deni. Serikali italazimika kufanya majadiliano kutokana na uzito wa deni. Aidha nchi zilizokusudiwa katika mpango huo ni zile zilizopo katika kundi ambalo sio wananchama wa Kundi la *Paris (Paris Club)*

(iv Kufanya uchambuzi wa madeni *(debt sustainability analysis)* kila baada ya miaka miwili ili kuweza kuona mwenendo wa deni la Taifa kwa kuzingatia vigezo mbalimbali vya Ki-uchumi kama vile mauzo ya nje, mapato ya ndani ya Taifa na kadhalika.

(v) Kuendelea kuongeza nguvu zaidi katika majadiliano ya awali ya mikopo *(loan negotiations)* ili Taifa liweze kupata nafuu zaidi katika vipengele mbalimbali vya Mkataba ihusuyo mikopo hiyo.

**MHE. MASOUD ABDALLAH SALIM:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru, pamoja na majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri nina swali moja la nyongeza. Kwanini Tanzania inajiingiza kwenye mikopo yenye riba kubwa ikijua kwamba uwezo wa kulipa ni mdogo?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. ABDISALAAM ISSA KHATIB):** Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema kwenye jibu langu la msingi; tunachukua mikopo yenye *concessional terms* kwa mujibu wa *IDA* ambayo riba yake hazidi asilimia moja.

Na. 60

**Shirika la Reli ya Kati**

**MHE. SIRAJI J. KABOYONGA** aliuliza:-

Kwa kuwa mchakato wa kubinafsisha baadhi ya huduma za Shirika la Reli ya Kati *(TRC)* Umekamilika au unakaribia kukamilika na kwa kuwa huduma za Shirika hilo ni muhimu sana kwa maendeleo ya Uchumi wa Tanzania na nchi nyingine za jirani kama Uganda, *Democratic Republic of Congo,* Rwanda na Burundi.

(a) Je, ni mali zipi na madeni yapi ya shirika hilo yatakayo husika katika ubinafsishaji huo na ni kampuni gani iliyopewa nafasi ya kuwa mwekezaji binafsi katika shirika hilo la Reli na kwa masharti gani?

(b) Je, ni lini hatima ya ajira na maslahi ya wafanyakazi wa Shirika hilo (*TRC*) na Serikali inaweza kulihakikishia Bunge hilo kwamba, wafanyakazi watakaoachishwa kazi watalipwa maslahi yao yote bila matatizo makubwa kama ilivyokuwa kwa wastaafu wa mashirika ya iliyokuwa Jumuiya ya Afrika Mashariki ilivunjika mwaka 1977.

(c) Je, Chuo cha Reli Tabora kilichopo Mjini Tabora kitaendelea kuwepo au kitafungwa na kitakuwa chini ya mamlaka gani?

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU (MHE. DR. MAUA A. DAFTARI):** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Miundombinu napenda kujibu swali la Mheshimiwa Siraji Juma Kaboyonga Mbunge wa Tabora Mjini lenye sehemu (a) (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mchakato wa kubinafisha au kukodisha Shirika la Reli Tanzania umefikia hatua za mwisho na Mkodishwaji ni Kampuni ya *RITES Ltd.* ya India.

*M/S RITES Ltd.* ya India na Serikali ya Tanzania wataunda Kampuni itakayojulikana kwa jina la *Tanzania Railways Limited (TRL)* ambayo itakabidhiwa jukumu la kuendesha shughuli zilizokuwa zinafanywa na Sherika la Reli Tanzania.

Kampuni ya *RITES* itamiliki asilimia 51 ya hisa katika kampuni hiyo na Serikali ya Tanzania itamiliki asilimia 49 ya hisa. Tanzania *Railways Limited* itafanya biashara ya kusafirisha abiria na mizigo kwa kukarabati na kutumia vichwa vya garimoshi na mabehewa yaliyopo na vilevile kukodisha au kununua mabehewa na vichwa vya garimoshi vingine kufuatana na mwenendo wa biashara itakavyokuwa.

Aidha kimkataba mkodishwaji atafanya matengenezo ya kawaida ya njia ya reli na mtandao wa mawasiliano na kuboresha kilomita 648 za njia za reli kwa kutandika reli nzito zaidi.

(b) Mheshimiwa Spika, Mkodishwaji atachukua wafanyakazi 3,700 kati ya wafanyakazi 6,631 waliopo sasa na wafanyakazi 2,931 ajira zao zitasitishwa na kulipwa mafao yao yote ya kisheria pamoja na mkono wa heri. Kiasi cha shilingi bilioni 59 zilitengwa katika bajeti ya Serikali ya mwaka wa fedha 2006/2007 kwa ajili ya malipo hayo?

(c)Chuo cha Reli Tabora ni mojawapo ya rasilimali ambazo zitakodishwa ili mkodishaji aweze kukitumia kwa kufundishia taaluma mbalimbali zinazohusiana na shughuli za reli.

**MHE. SIRAJI J. KABOYONGA:** Mheshimiwa Spika, namshukuru Naibu Waziri kwa majibu mazuri, naomba niulize maswali yafuatayo ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, la kwanza Serikali imejihakikishiaje kwamba huyu mkodishaji ana uwezo wa kifedha wa kufanya majukumu ambayo Mheshimiwa Naibu Waziri ameyaorodhesha kwenye majibu yake? Kwa sababu kama fedha zitaleta utata itakuwa ni kitendawili.

La pili mkodishwaji inasemekana reli kwa urefu wa kilomita 648 Je, urefu wa reli kutoka Dar es Salaam mpaka Kigoma kwa ujumla ni kilomita ngapi na nani atawajibika kuzikarabati hizo zinazosalia.

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU (MHE. DR. MAUA A. DAFTARI):** Mheshimiwa Spika, napenda nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali imeifanyia uchunguzi kampuni ya *RITES* na kujua inaweza kufanya shughuli hizo. Lakini kwa sababu tunaingia naye ubia tutakuwa naye sambamba katika masuala ya kukopa na kulipa ili reli hii isije ikasimama.

Kilomita zilizobaki za reli napenda nmhakikishie Mbunge ni kazi ya Serikali kuona zinarekebishwa na tayari tumeshapata fedha za awali za kufanya maswala hayo na tutaendelea kuhakikisha kwamba reli hii inaboreshwa na hata kule kwake Tabora kazi inaendelea vizuri kilichobakia ni *fish plates* za zile reli ambazo zimewasili tayari na karibu tutazifunga ili reli ile iwe imara zaidi

**MHE. AZIZA S.ALLY:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Kwa kuwa mwaka jana wakati imesitishwa treni kwenda moja kwa moja Dar es Salaam kutokea Mwanza , Mheshimiwa Waziri alisema kuwa mpaka mwezi huu sita treni hiyo itakuwa tayari kwenda moja kwa moja na huu sasa ni mwezi wa sita umeshafika Waziri anasemaje?

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU (MHE. DR. MAUA A. DAFTARI):** Mheshimiwa Spika, ni kweli tulikubaliana kwamba baada ya majadiliano kuyapima tuliona kwamba mwezi wa sita tungekuwa mwafaka kwamba mwekezaji atakuwa yupo tayari *on site* na kufanya hizo shughuli. Bahati mbaya tumechelewa kidogo lakini shughuli hizo zitafanywa kama tulivyopanga.

Na. 61

**Hitaji la Soko la Kisasa – Tanga**

**MHE. NURU AWADH BAFADHILI** aliuliza:-

Kwa kuwa hivi sasa Tanga ni Jiji licha ya kwamba halina soko la kisasa wakati kuna Halmashauri nyingine za miji zenye masoko ya kisasa:-

Je, ni lini Serikali itajenga soko la kisasa linaloendana na hadhi ya Tanga kuitwa jiji?

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA MASOKO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Viwanda, Biashara na Masoko naomba kujibu swali la Mheshimiwa Nuru Awadh Bafadhili, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ujenzi wa soko la kisasa katika Jiji la Tanga unategemea uamuzi wa Halmashauri ya Jiji la Tanga lenyewe. Lengo la kufanya hivyo ni kuhakikisha kuwa Halmashauri hiyo inaweka utaratibu wa umiliki, uwajibikaji na utunzaji mzuri wa soko hilo. Uamuzi huo ni lazima ukubalike na uongozi husika na kuuweka katika mpango wa maendeleo.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia hayo, naomba kumshauri Mheshimiwa Mbunge ashirikiane na wananchi wakazi wa Halmashauri ya Jiji la Tanga kuibua mpango wa Ujenzi wa soko la kisasa na hivyo kuingizwa katika mpango wa maendeleo wa Halmashauri ya Jiji la Tanga.

**MHE. NURU AWADHI BAFADHILI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza. Kwa kuitumia Halmashauri mpaka ikae na kuibua miradi itachukuwa muda; na kwa kuwa Tanga inapakana na wenzetu wa Pemba ambao wananunua mazao kutoka Tanga na hali kadhalika kutoka nchi ya jirani ya Kenya wanaenda wenyewe shambani. Je, Serikali haitupii jicho la huruma Jiji la Tanga kuweza kusaidia kujenga soko ili tupate mapato kutokana na fedha za kigeni kutoka nchi za jirani?

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA MASOKO:** Mheshimiwa Spika, nimesema hapa kwamba utaratibu wa kujenga masoko katika majiji au Halmashauri za miji upo chini ya mikono ya Halmashauri husika. Kwa hali hiyo mimi nimemshauri Mheshimiwa Mbunge kwamba ashirikiane na uongozi wa Jiji la Tanga ambapo yeye ni sehemu ya uongozi huo ucheleweshwaji anaousema anaweza akauharakisha ili wananchi waendelee kuteseka kwa kukosa soko.

Na. 62

**Mradi wa Kupeleka Maji Kahama**

**MHE. EMMANUEL J. LUHAHULA (K.n.y. MHE EZEKIEL M. MAIGE)** aliuliza:-

Kwa kuwa mradi wa kupeleka maji – Mji wa Kahama na Shinyanga unaendelea vizuri kwa upande wa Mkandarasi:-

(a) Je, ni wananchi wangapi wa Kata za Bulige Ngaya na Kinanga katika Jimbo la Msalala wameathiriwa na mradi huo kwa maeneo yao kuchukuliwa ili kupitisha mradi?

(b) Je, ni kiasi gani cha fedha kimetengwa kwa ajili ya fidia kwa wananchi hao?

(c) Je, ni kiasi gani cha fidia kimelipwa kwa wananchi hao na kama hakijalipwa, ni lini basi kitalipwa?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Ezekiel Maige, Mbunge wa Jimbo la Msalala naomba kutoa maelezo ya ujenzi wa mradi wa maji kutoka Ziwa Victoria hadi miji ya Kahama na Shinyanga kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, mradi wa maji wa Kahama-Shinyanga unachukua maji kutoka Ziwa Victoria na mitambo ya kusafisha na kutibu maji ipo katika kijiji cha Ihelele Wilayani Misungwi. Mitambo hii itatumia umeme wa megawati 10 ambao usanifu umeonyesha utapatikana kutoka kwenye kituo cha Bulyanhulu. Hivyo kituo hicho

kinapanuliwa ili kukidhi mahitaji. Aidha, njia ya umeme itapita katika Wilaya ya Geita kuelekea kwenye mitambo hiyo. Njia ya umeme itaanzia Bulyanhulu kupitia Kata za Bulige Ngaya na Kinanga urefu wa kilometa 52 hadi kijiji cha Nyamtukuza.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, sasa naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge, lenye vipengele (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, wananchi wapatao 341 wanaoishi katika maeneo ambayo njia ya umeme itapita kuanzia Bulyanhulu hadi Kijiji cha Nyamtukuza urefu wa kilometa 52 pamoja na wananchi wale wanaoishi katika Kata za Bulige, Ngaya na Kinanga katika Jimbo la Msalala wameathirika na mradi huo kwa maeneo yao kuchukuliwa ili kupitisha njia ya umeme.

(b) Mheshimiwa Spika, kiasi cha fedha kinachohitajika kuwalipa fidia wananchi hao ni shiilingi 31,518,065.70.

(c) Mheshimiwa Spika, hadi kufikia tarehe 18/6/2007 jumla ya watu 333 wamelipwa shilingi 30,808,22/= na watu 8 bado hawajalipwa kiasi cha shilingi 709,785.70. Aidha, wataalam kutoka jijini Mwanza wanaendelea kufanya tathmini kwenye vijiji vingine katika Wilaya ya Kahama.

**MHE. EMMANUEL J. LUHAHULA:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Maige na wananchi wa Jimbo la Msalala napenda kutoa shukrani kwa Serikali kwa uadirifu uliofanyika hasa katika utekelezaji wa mradi huu. Lakini baada ya kutoa shukrani hizo naomba niulize swali moja la nyongeza. Kwa kuwa mradi wa Ziwa Victoria ni mradi ambao tunategemea unaweza ukasaidia sana katika utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya mwaka 2005; na kwa kuwa tatizo la maji katika Wilaya ya Bukombe linafahamika na katika Bajeti iliyopita nililieleza; na kwa kuwa Waziri wa Maji alipofika kule aliona shida kubwa ya maji iliyopo katika Wilaya ya Bukombe na jitihada ambazo wananchi wanafanya katika kuvuna maji.

Je, Serikali inasema nini kuhusiana na Mradi wa maji wa Ziwa Victoria kwa wananchi wa Wilaya ya Bukombe?

**WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, ni kweli nimetembelea jimbo la Bukombe na pia Wizara imepokea maombi mengi kutoka maeneo ya mbalimbali. Shinyanga Mjini na Vijijini, Wilaya Bukombe kwa kupanua wapate maji kutoka kwenye Mradi huu wa Kahama Shinyanga. Mradi huu sasa hivi unatekelezwa kwa awamu ya kwanza na utahusisha miji miwili ya Kahama na Shinyanga na pia vijiji 54 ambavyo viko katika umbali usiozidi kilomita tano katika njia inayopita bomba kuu linalipeleka maji Kahama na Shinyanga.

Ni kweli Serikali inatambua mahitaji makubwa kwa wanavijiji wengi zaidi ya vijiji 54 ambavyo vimeasisiwa sasa hivi lakini mradi huu ambao umeighairimu Serikali shilingi bilioni 225, una uwezo kiasi hicho. Kwa sasa hauta mudu kuchukua vijiji zaidi au miji zaidi au Wilaya zaidi hizo ambazo zimeasisiwa.

Mheshimiwa Spika, nitamwomba Mheshimiwa Mbunge na Waheshimiwa Wabunge wote waliopo kwenye Bunge lako Tukufu kuvuta subira Serikali mara awamu hii ya kwanza itakapokamilika, ndani ya mwaka huu 2007, uasisi wa awamu hiyo itajaribu kuchukua maeneo mengi zaidi kwa kadri ambavyo Halmashauri husika zitakavyokuwa zimewasilisha mahitaji yao. Kwa sasa tunayapitia na kuyafanyia tathmini maombi yote yale ambayo yamewekwa na ahadi zile ambazo Mheshimiwa Rais alizitoa wakati anatembelea majimbo hayo. Ahsante sana! *(Makofi)*

Na. 63

**Vyama vya Kitaifa vya Watu Wenye Ulemavu**

**MHE. ANIA SAID CHAUREMBO** aliuliza:-

Kwa kuwa, Vyama vya Kitaifa vya Watu wenye Ulemavu vimesajiliwa kisheria na vinafanya kazi za utetezi wa ushauri kwa ajili ya watu wenye ulemavu kwa mujibu wa sheria; na kwa kuwa, sehemu kubwa kama si yote ya Vyama hivyo havijapangiwa Bajeti zao:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuwaondolea watu wenye ulemavu kero hiyo kwa kuwapangia ruzuku yenye kutosheleza Vyama vya Kitaifa vya Watu wenye Ulemavu?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Ania Said Chaurembo, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza, napenda nikubaliane na Mheshimiwa Mbunge kwamba Vyama vya Kitaifa vya Watu wenye Ulemavu vimesajiliwa kisheria na kwamba vinafanya kazi zao kwa mujibu wa sheria. Vyama hivi ni vya hiari na vinafanya kazi ya kuwaunganisha wanachama wao na pia kuwa sauti ya utetezi.

Vyama vya hiari vikiwemo Vyama vya Watu Wenye Ulemavu vinaundwa kwa lengo la kuisaidia Serikali katika uboreshaji huduma kwa wananchi. Hata hivyo, Serikali haina kifungu maalum cha Bajeti kinachotengwa kwa ajili ya shughuli za uendeshaji wa vyama hivi.

Mheshimiwa Spika, ni dhamira ya Serikali kuweka mazingira yanayohakikisha kuwa vyama hivi vya hiari vinajengewa uwezo wa kuendesha shughuli zake ipasavyo. Kwa msingi huo, Serikali kupitia Wizara yangu imekuwa ikitoa ruzuku kwa Vyama vya hiari vikiwemo Vyama vya Watu wenye Ulemavu pamoja na Shirikisho la Watu wenye Ulemavu (SHIVAWATA).

Mwaka wa fedha 2005/2006 Vyama hivyo vilitengewa shilingi milioni saba (7), mwaka 2006/2007 Wizara ilitoa Shilingi 14,000,000/=. Tunafahamu kwamba kiasi tunachotoa hakitoshelezi mahitaji ya vyama vya Watu wenye Ulemavu, lakini ni nia ya Serikali kuongeza ruzuku hiyo kadri uwezo wa bajeti utakavyoruhusu. Katika mwaka ujao wa fedha 2007/2008, kiasi cha shilingi 30,000,000/= kimetengwa kwa madhumuni hayo. *(Makofi)*

**MHE. ANIA SAID CHAUREMBO:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili madogo ya nyongeza. Katika jibu la msingi la Mheshimiwa Naibu Waziri nimefurahi kuona kwamba ruzuku za watu wenye ulemavu zinaongezewa mwaka hadi mwaka. Swali langu linakuja, kwa kuwa Rais wa Awamu ya Nne mara tu baada ya kuchukua madaraka alitembelea taasisi mbali mbali kuangalia mwenendo mzima wa kazi na matatizo ya taasisi hizo; na kwa kuwa katika taasisi hizo alitembela masoko, magereza na hospitali; na kwa kuwa Rais, bado hajatembelea Taasisi ya Watu wenye Ulemavu.

Je, Serikali itakubaliana nami kwamba iweze kumwandalia Rais ziara ya kukutana na Walemavu katika Jumuiya yao ya SHIVAWATA ambalo ndilo Shirikisho lao? Swali la pili; Kwa kuwa Waziri Mkuu alifanya Ziara ya Mwaliko rasmi siku ya Maalbino tarehe 4/5/2007; na kwa kuwa Waziri Mkuu alitoa tamko kwamba Watu wenye Ulemavu wasaidiwe katika miradi yao katika Serikali pale ambapo watahitaji msaada wa Serikali; na kwa kuwa Watu wenye Ulemavu hata pale wanapopeleka miradi yao Serikalini, bado wanakwamishwa kwa kutaka baraka tu ya Serikali. Je, Serikali inatoa tamko gani kuhusu baadhi za Wizara ambazo zinakwamisha miradi ya maendeleo ya Watu wenye Ulemavu?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Spika, ni kweli Mheshimiwa Rais alitembelea Wizara mbali mbali na katika Serikali ameweza kutembelea Vikundi mbali mbali vikiwemo masoko, hospitali, magereza na kadhalika.

Lakini, bado hajatembelea Wenye Ulemavu. Mheshimiwa Spika, ninachofahamu ni kwamba Rais anafahamu umuhimu wa kila kundi na Mheshimiwa Rais anayo ratiba maalum na ana kazi nyingi zikiwemo kutembelea Mikoa, Kutembelea Vikundi na pamoja na Ziara zile za kutoka nje ya nchi. Kwa maana hiyo, ni kwamba, kama Wizara ya Afya, sisi hatuwezi tukasema kwamba Mheshimiwa Rais, leo nenda kaone kikundi cha Watu wenye Ulemavu.

Lakini, ninachoamini ni kwamba kwa vile Mheshimiwa Rais anatambua makundi haya, anajua yeye atakavyopanga ili aweze kuwafikia. Namhakikishia Mheshimiwa Mbunge asiwe na wasi wasi, Rais wetu anajali na kwamba makundi yote atayafikia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu swali lake la pili ambapo amesema kwamba Mheshimiwa Waziri Mkuu alitoa tamko kwamba Watu wenye Ulemavu wapewe ruzuku. Nakubali kabisa kwamba Mheshimiwa Waziri Mkuu alitoa tamko hilo wakati tunaadhimisha siku ya Walemavu Duniani ambapo Serikali iliahidi kutoa pesa mwaka 2007.

Mheshimiwa Spika, kwa taarifa yako Wizara tayari ilikwishatekeleza ahadi hii kwani mnao mwezi Februari mwaka huu, Serikali ilitoa ruzuku kwa Vyama 7 vya Watu wenye Ulemavu vya kitaifa kama ifuatavyo:-

- Chama cha Watu wenye Ulemavu wa Viungo walipata shilingi milioni 2;
- Chama cha Wasioona Tanzania walipata milioni 2;
- Chama cha Viziwi Tanzania walipata shilingi milioni 2;
- Chama cha Maalbino Tanzania walipata milioni 2;
- Cha cha Walemavu wa Akili walipata milioni 2;
- Chama cha Viziwi – Wasioona walipta milioni 2; na
- Shirikisho la Vyama vya watu wenye ulemavu (SHIVAWATA) walipata milioni 2, ndio maana nikasema mwaka jana Wizara ilitenga shilingi milioni 14 kwa sababu ya vyama.

Mheshimiwa Spika, lakini nataka niwafahamishe Waheshimiwa Wabunge kwamba pesa tunazotoa hizi tunapeleka Makao Makuu ya Vyama hivi nilivyovitaja. Kwa maana hiyo, wale ambao Vyama viko mikoani, ni wajibu wao wenyewe waende kule Makao Makuu ili waweze kuona kwamba hii pesa wanagawana namna gani.

Sisi huwa hatuinglii hilo. Lakini, vile vile naomba nitoe wito kwamba siamini kwamba kama kweli kikundi cha Walemavu kimefanya machanganuo na kimeomba msaaada, Serikali kwa makusudi itaacha. Mimi nahakikisha kwamba Serikali ni sikivu. Na kama kweli Vyama vya Watu wenye Ulemavu waliomba msaada mahali, kama pesa ipo Serikali haitakuwa na matatizo yoyote ya kuwasaidia. *(Makofi)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (BUNGE) :** Mheshimiwa Spika, napenda kumpongeza sana Mheshimiwa Naibu Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii kwa majibu mazuri sana aliyoyatoa. Lakini nami naomba niongezee tu kwamba, kuhusu suala lake kwamba Wizara zinakwamisha kuwasaidia Walemavu. Kama alivyosema, siyo kweli na sasa hivi kwa kusisitiza zaidi kuonyesha kwamba kuna utaratibu wa kuwasaidia. Mheshimiwa Waziri Mkuu ameagiza Wizara zote kuwa na Mkakati na mafunzo na ajira kwa Walemavu na kutoa taarifa katika utaratibu wa utekelezaji katika kila awamu ya miezi mitatu. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Job Ndugai, sikujua umerejea! Pole sana na masomo. Natumaini unaendela vizuri. *(Makofi)*

Na. 64

**Mlipuko wa Magonjwa Mapya Nchini.**

**MHE. JOB Y. NDUGAI** aliuliza:-

Kwa kuwa, katika miaka ya karibuni kumejitokeza magonjwa mengi mapya kwa binadamu kama *RVF,* UKIMWI*, EBOLA, AVIAN FLUU* n.k. Je, magonjwa hayo mapya yanatoka wapi hasa? Virusi husika vimetoka wapi kama havikuwepo?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Job Y. Ndugai, Mbunge wa Kongwa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, magonjwa mengi mapya yanayojitokeza kama *SARS, EBOLA, AVIAN FLU, RVF* na kadhalika yapo katika kundi la magonjwa yanayojitokeza upya na magonjwa mapya *(emerging and re-emerging diseases)*. Magonjwa haya yana tabia zinazofanana kwa kuwa yote ni vigumu kutibika yaani hakuna dawa inayoweza kutibu magonjwa hayo.

Mara nyingi yanapotokea huenea kwa haraka na kuathiri watu wengi kwa njia ya mlipuko na huweza kusababisha vifo kwa wingi kama yasipothibitiwa mapema. Mheshimiwa Spika, vile vile, magonjwa haya yana tabia nyingine za ziada kama zifuatazo:-

- § Njia za Maambukizi ni tofauti na zile zilizozoeleka.
- § Huleta madhara mapya *(complications)* ambayo huwa tofauti na yaliyozoeleka.

Mheshimiwa Spika, magonjwa haya husababishwa na virusi vilivyobadilika kijenetiki *(Genetic Recombination)*. Virusi hivi si vipya bali vimekuwepo tangu zamani na inapotokea mabadiliko ya kijenetiki yanayoitwa *mutation*, husababisha kuzaliwa kwa aina ya Virusi vipya ambavyo vina tabia tofauti nna Virusi vya zamani.

Ikiwa Virusi hivi vitamshambulia binadamu, ni rahisi sana kuleta madhara kwa sababu binadamu anakuwa hana kinga *(Immunity)* ya kujilinda na Virusi hivyo vipya.

Mheshimiwa Spika, mabadiliko ya tabia ya Virusi hivi hutokea kutokana na mabadiliko ya tabia za binadamu ambapo kuna muingiliano mkubwa kati ya binadamu na wanyama, hivyo kusababisha magonjwa mengi ambayo hapo awali yalikuwa yakiwashambulia wanyama pekee huanza kushambulia binadamu pia kutokana na sababu zilizoainishwa hapo awali.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha miaka 15 iliyopita magonjwa mapya yaliyojitokeza katika mataifa mbali mbali duniani ni kama ifuatavyo:-

- § *Hantavirus Pulmonary Syndrome (US);*
- § *Bovine Spongiform Encephalopathy (UK);*
- § *Nipah Virus Encephalopathy* (Malaysia – Singapore);
- § *Avian Influenza (Korea)*

- § *Severe Acute Respiratory Syndrome – SARS* (China);
- § *Rift Valley Fever* (Nchi za Ukanda wa Bonde la Ufa – Kenya, Tanzania, Sudan, Somalia, Uganda, Afrika Kusini n.k.).

**MHE. JOB Y. NDUGAI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kunipa nafasi niweze kuuliza swali la nyongeza na namshukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu mazuri kuhusiana na swali langu la magonjwa mapya ambayo yanajitokeza hapa Duniani mara kwa mara kama Mafua ya Ndege, mara utasikia *Ebola,* UKIMWI na hivi majuzi tumepata habari ya Bonde la Ufa. Ni magonjwa ambayo ni magumu kutibika, yanaenea kwa haraka, yanaathiri watu wengi na yanasababisha vifo vingi. *(Makofi)*

Lakini, swali la kwanza dogo ni kuhusiana na ugonjwa hususan wa Bonde la Ufa. Ugonjwa huu umeathiri kwa kiwango kikubwa nchi yetu na kampeni yake ilienda vizuri sana, wananchi wakaogopa kula nyama kabisa. Je, kampeni kama ile ambayo imefanikiwa, watu wakaogopa kula nyama kabisa, haiwezi kutumika mbinu zile zile kwa ugonjwa wa UKIMWI? Maana hata Mikoa ya Shinyanga, Mwanza na Tabora waliogopa kula nyama kabisa! Hilo la kwanza. La pili, kwa ugonjwa huo wa Bonde la Ufa, kwa hali ilivyo sasa, unawaambiaje Watanzania na hasa wananchi wa Mkoa wa Dodoma hususan wa Jimbo la Kongwa. Je, sasa ruksa kula nyama au vipi ?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Spika, swali la kwanza; Mheshimiwa Spika, kampeni kweli ilifanyika kuhusu Homa ya Bonde la Ufa. Kampeni anayotaka tuifanye kitaifa kwa susla la UKIMWI, Mheshimiwa Spika na Waheshimiwa Wabunge wenzangu, mimi nafikiri Serikali tangu tuanze kupata tatizo la UKIMWI miaka ya 1980 imekuwa ikihangaika huku na kule ikiwashirikisha viongozi, wananchi, jamii kuweza kupigana na janga hili la UKIMWI.

Suala la kusema tufanye kampeni kama tuliyofanya wakati wa Bonde la Ufa, mimi nafikiri ni lazima tuelewa kwamba tulipokuwa tunazungumzia Bonde la Ufa, hatukuwa tumeacha kampeni dhidi ya gonjwa hili la UKIMWI. Nataka tu niwakumbushe kwamba Serikali bado inaendelea kupiga vita na kampeni kali inaendelea na sisi Waheshimiwa Wabunge wote ni mashahidi kwamba hata sisi wenyewe tumeambizana kwamba katika mazungumzo yetu, ajenda mojawapo ni lazima iwe suala zima la UKIMWI.

Mheshimiwa Spika, swali la pili kuhusu *Rift Valley* na hali ya kula nyama katika Mkoa wa Dodoma na hususan katika Wilaya ya Kongwa. Napenda kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba hali ya ugonjwa sasa hivi kwa kweli imepungua sana na ng’ombe wengi ni salama kwa sababu kampeni ya chanjo ilifanyika na muda tangu wanyama wote walipopata chanjo, sasa hivi ng’ombe ni salama. Kwa hiyo, tunawashauri kwamba wale nyama kwa bidii kabisa ili waweze kuboresha afya zao. Nshukuru. *(Makofi)*

**MHE. ELIETTA N. SWITI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi. Kwa kuwa Serikali inaelewa fika kwamba magonjwa haya mapya yataendelea kutokea. Je, imejiandaa vipi kupambana na magonjwa haya mara yafikapo nchini ili yasiweze kuenea kwa kasi? Ahsante!

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Spika, ni kweli magonjwa haya kwa mfano kama *Rift Valley Fever* na magonjwa mengine ni magonjwa ambayo huwa yanalipuka. Nataka nitoe mfano tu, Serikali imekuwa ikiendelea kueleza kwa mfano nikichukulia mfano wa Ugonjwa wa Homa ya Bonde la Ufa, tumekuwa tukipewa maelezo kwamba ugonjwa huu huwa mara nyingi unatokea katika historia na jinsi walivyofuatilia, kila baada ya miaka 10 ugonjwa huu huwa unajitokeza hususan ikifuatiwa na hali ya ukame mkubwa na baadaye ikija hali ya mvua nyingi.

Kwa maana hiyo tunaendelea kutoa elimu kwa wananchi ili kuendelea kufuatilia mwenendo wa ugonjwa huu ikiwemo na magonjwa mengine yote. Hivyo, napenda kuchukua nafasi hii kuwashauri Waheshimiwa Wabunge tutakapokuwa tunaenda kuona wananchi wetu, tuendelee kuwakumbusha kwamba magonjwa ya milipuko huwa yanakuja kwa msimu, lakini kuna ishara zinazojionyesha na kuna kipindi.

Kwa hiyo, wawe waangalifu na waendelee kujiweka katika hali ya tahadhari na sisi Serikali tutaendelea kujidhatiti ili hali hii tuweze kuidhibiti.

Na. 65

**Utekelezaji wa Mradi wa Umeme Busega**

**MHE. DR. RAPHAEL M. CHEGENI** aliuliza:-

Kwa kuwa Serikali katika Mkutano wa Bunge wa Novemba 2006 iliahidi kutekeleza katika Bajeti ya mwaka 2006/2007 mradi wa umeme vijiji vya Lamadi, Kalemera, Nyamikoma hadi Nyashimo na ule wa Lamadi, Mkula, Nyangili, Malili hadi Ngasamo katika Jimbo la Busega, na kwa kuwa mradi huo hadi sasa haujatekelezwa licha ahadi iliyotolewa Bungeni tangu mwaka 2003:-

(a) Je, ni kiasi gani cha fedha kimetengwa kwa ajili ya mradi huo na utaanza kutekelezwa lini?

(b) Je, Serikali haioni kuwa ni vyema miradi kama inayochangia kukuza pato la taifa kupitia kuongeza uzalishaji na kutoa ajira kwa wananchi hasa vijana na akina mama ikapewa kipaumbele cha utekelezaji kuliko ilivyo sasa?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Dr. Raphael M. Chegeni, Mbunge wa Busega, lenye sehemu (a) na (b) naomba kutoa maelezo ya utangulizi yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika,Vijiji vya Kalemela, Nyamikoma, Nyashimo vipo kando kando mwa barabara kuu ya Mwanza hadi Musoma. Vijiji vya Mkula, Nyangili, Malili vipo kati ya barabara itokayo Lamadi kuwelekea Bariadi. Kijiji cha Lamadi kimeishapatiwa umeme kutoka kwenye kituo cha umeme Bunda.

Mheshimiwa Spika, ili kufikisha umeme kwenye vijiji vya Mkula ikiwa ni pamoja na hospitali ya Mkula, Malili hadi Ngasamo ambapo kuna jineri, inategemewa kujenga njia ya umeme wa msongo wa kilovoti 33 kutokea Lamadi. Serikali imekuwa ikitafuta fedha za utekelezaji wa miradi mbali mbali ikiwemo ya kupeleka umeme kwenye maeneo aliyoyataja Mheshimiwa Mbunge. Serikali ya Ufalme wa Hispania imeonyesha nia ya kufadhili upelekaji umeme katika maeneo hayo ikiwa ni pamoja na Vijiji vya Kalemera, Nyamikoma na Nyangili chini ya mradi ujulikanao kama *Spanish Phase IIIC for Rural Electrification*.

Mheshimiwa Spika, kampuni ya ujenzi ya *ABB Distribution & INABENSA* imeishaingia mkataba na *TANESCO* unaohusu utekelezaji wa mradi huo unaojumuisha pia ujenzi wa kituo cha kupoza umeme katika eneo la Mabuki Wilayani Misungwi. Kinachosubiriwa ili utekelezaji uanze ni ukamilishaji wa upatikanaji wa fedha hizo kutoka Serikali ya Ufalme wa Hispania. Hata hivyo Shirika letu la *TANESCO* Mkoani Mwanza wameomba kwenye Bajeti ya Mkoa shilingi milioni 93 ili kuanza ujenzi wa njia ya umeme ya msongo wa kilovoti 33 na yenye urefu wa kilomita 10 kwa ajili ya kijiji cha Nyamikoma. Ujenzi wake unategemea kuanza kama *TANESCO* itakuwa na uwezo wa kifedha na hivyo kuridhia na kuidhinisha bajeti hiyo.

Baada ya maelezo hayo ya utangulizi, naomba sasa kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, kiasi cha fedha kilichoombwa chini ya ufadhili wa Serikali ya Hispania kwa ajili ya upelekaji umeme kwenye Vijiji vya Mkula, ikiwa ni pamoja na Hospitali, Malili, Nyangili na Kalemela ni shilingi bilioni 3.0.

(b) Serikali hutoa kipaumbele kwenye miradi inayochangia kukuza pato la taifa kupitia kuongeza uzalishaji na kutoa ajira kwa wananchi hasa vijana na akina mama. Hata hivyo, ufinyu wa Bajeti ndio unaosababisha miradi mingi ya aina hii isitekelezwe kwa muda uliopangwa.

**MHE. DR. RAPHAEL M. CHEGENI:** Mheshimiwa Spika, napenda nimpongeze sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu mazuri. Kwa kweli kwa mara ya kwanza nasema kwamba nimepata mwanga juu ya suala hili ambalo toka mwaka 2003

nimekuwa nikiuliza hapa Bungeni na Serikali imekuwa ikiahidi. Sasa kwa ahadi ya Serikali imenipa mwanga.

Mheshimiwa Spika, swali langu ni kwamba; la kwanza, ni lini sasa nia na hasa ya wafadhili kupitia Serikali ya Mfalme wa Hispania itatekelezwa? Kwa sababu nilikuwa nikiahidiwa kila mwaka kwamba wafadhili watatoa pesa, watatoa pesa. Sasa Mheshimiwa Naibu Waziri ajaribu kunihakikishia hapa kwamba ni lini hiyo nia itathibitishwa au itatekelezwa ili tuweze kujianda kwa ajili ya kupokea umeme huo.?

La pili, kwa kuwa matatizo yaliyoko Jimbo la Buswega yako sambamba sawa na matatizo katika maeneo kama ya Nyalugusu, Katolo, Kome, Nzela katika Wilaya ya Geita. Na vile vile katika Wilaya ya Sengerema katika maeneo ya Kamanga, Busisi, Buyagu na Nakatungulu; Je, ni lini sasa Serikali itaweka mpango mkakati walau hatua kwa hatua ili miradi hii iweze kutekelezwa?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, nianze kwa kuipongeza Serikali kwa jitihada ambazo imekuwa ikifanya na hususan katika utekelezaji wa mradi ambao Mheshimiwa Mbunge amekuwa akifuatilia hasa kwenye Jimbo la Busega. Lakini, sehemu ya kwanza ya swali lake la nyongeza kwamba ni lini ahadi ya Wafadhili wetu itatekelezwa, naomba nimshawishi Mheshimiwa Mbunge kwamba kama tulivyokwisha kusema kwenye jibu la msingi, hatua inaendelea vizuri sana ya ufuatiliaji na utekelezaji kwa sababu haya ni makubaliano ya nchi na tunaamini kwamba wananchi wanalitambua hili. Tunaomba kupitia Bunge hili tukufu ahadi ambazo zimekuwa zikitolewa na wafadhili na Serikali kwa ujumla, wananchi wazidi kuvuta subira akiwemo Mheshimiwa Dr. Raphael Chegeni kwa niaba ya wananchi wake wa Jimbo la Busega. Tunafuatilia na tuna imani kwamba mradi huu utatekelezwa kama yeye mwenyewe alivyokiri katika utangulizi wa maelezo ya kuishukuru Serikali.

Mheshimiwa Spika, sehemu ya pili, tunafahamu matatizo haya ambayo yanajitokeza katika Jimbo la Busega yanafanana na matatizo yanayojitokeza katika sehemu nyingi sana kwa nchi yetu. Lakini mipango mikakati ipo mingi na mara kadhaa

Serikali ilishaahidi katika Bunge hili Tukufu kwamba ipo mipango ambayo inaendelea kiutekelezaji. Niseme tu kwamba tuna mipango ambayo inapitia Serikali Kuu, tuna mipango ambayo inapitia kwenye Shirika letu la *TANESCO*.

Lakini pia kuna mipango ambayo utekelezaji wake unategemea wafadhili wa kutoka nje. Mheshimiwa Spika, naomba wananchi kupitia Bunge hili Tukufu wazidi kuvuta subira, tunafahamu utekelezaji upo na tutakuwa tunawataarifu kwa kadri siku zinavyoendelea. *(Makofi)*

**MHE. DR. FESTUS B. LIMBU:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi niulize swali la nyongeza. Kwa kuwa kuna wawekezaji wazalendo wamejitokeza katika mji wa Magu kuwekeza katika viwanda vya kukoboa Mpunga, lakini tatizo ni kwamba sasa pamoja na kwamba umeme upo, unakuwa wa mgao kwenye eneo lile kwa sababu mashine zimekuwa nyingi.

Mheshimiwa Spika, Je, Naibu Waziri atakubaliana na mimi kwamba kuna haja sasa ya kuongeza umeme katika maeneo hayo ili hawa wawekezaji waweze kurudisha mikopo ambayo wamechukua kwa ajili ya mashine walizoweka?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, ninakubaliana naye na kwamba si sehemu ya eneo la Magu tu, ni nia ya Serikali na ni vyema tukaendelea kuongeza nguvu kuboresha huduma ya umeme mahali popote pale ambapo mahitaji yake yanahitajika na viwango vinakidhi.

Lakini, nataka kumwondolea hofu Mheshimiwa Dr. Limbu, sisi kama Serikali Kuu, pia tuna Taasisi zetu, tuna Ofisi zetu Mikoani, naomba nimkaribishe Ofisini, jambo hili tulishughulikie kwa kina zaidi kwa ajili ya utekelezaji. *(Makofi)*

Na. 66

**Wachimbaji Wadogo wadogo – Kilwa, Ruangwa na Nachingwea**

**MHE. RIZIKI SAID LULIDA** aliuliza:-

Kwa kuwa, katika Wilaya ya Kilwa, Ruangwa na Nachingwea kumejitokeza wachimbaji wadogo wadogo wa madini kama dhahabu, *gemstone* na *gypsum*. Je, Serikali imefanya utafiti gani kujua kuwa maeneo hayo yana madini na kuna mpango gani wa kuwasadia wachimbaji wa maeneo hayo?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Riziki S. Lulida, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Kazi ambazo Serikali imezifanya katika maeneo ya Wilaya za Kilwa, Ruangwa na Nachingwea ni uchoraji wa ramani za kijiolojia na utafiti wa kijiofizikia kwa kutumia ndege katika zoezi lililofanyika nchi nzima. Aidha, utafiti wa kina ulifanyika kwenye maeneo ya Wilaya hizo yaliyobainika kuwa na madini wakati wa tafiti za awali.

Mheshimiwa Spika, matokeo ya tafiti hizo yameonyesha kuwa katika Wilaya za Kilwa, Ruangwa na Nchingwea kuna madini ya chumvi, jasi, dhahabu, shaba, *uranium*, *graphite* na madini ya ujenzi.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu ina mikakati ya kuwasaidia wachimbaji wadogo nchini. Mojawapo ya Mikakati hiyo ni kufungua Ofisi za Madini kwenye Wilaya na Mikoa yenye shughuli nyingi za uchimbaji madini. Lengo la mkakati huu ni kusogeza huduma za ugani na ushauri karibu zaidi na wachimbaji. Kwa maeneo yaliyotajwa, Ofisi

ya Madini ya Kanda iliyoko Mtwara inatoa huduma za ugani na ushauri kwa wachimbaji madini katika maeneo yote niliyoyataja.

Mheshimiwa Spika, mkakati mwingine ni kuhamasisha watu na kampuni mbali mbali kufungua maduka ya kuuza vifaa na nyenzo kwa ajili ya uchimbaji. Aidha, taratibu za kuwapatia leseni za biashara ya madini wafanyabiashara wa madini zimerahisishwa ili waweze kuwaendea wachimbaji katika maeneo yao kwa lengo la kuwasaidia wachimbaji kuwa na huduma za masoko karibu yao.

Mheshimiwa Spika, mikakati mingine ni kuimarisha usalama migodini na kuwahamasisha wachimbaji wadogo kuanzisha na ama kujiunga katika vikundi vya *SACCOS* ili wajijengee mazingira mazuri ya kupata mikopo kutoka kwenye taasisi za fedha.

**MHE. RIZIKI SAID. LULIDA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana! Napenda kumshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu mazuri na matokeo mazuri ya tafiti ambayo yanaonyesha Ruangwa, Kilwa na Nachingwea kwamba ipo dhahabu, shaba, *gypsum*, *graphite* na kadhalika. Nina maswali mawili ya nyongeza, Swali la kwanza.

Kutokana na uzoefu uliojitokeza sasa hivi kwa migogoro ya wachimbaji wadogo wadogo na wakubwa. Je, Wizara inafanya mikakati gani ya kuhakikisha na kuepusha migogoro ambayo inaweza kujitokeza katika sehemu hizo ambazo tayari madini yameanza kupatikana?

Swali langu la pili: Je, Serikali ina mkakati gani wa kuihakikishia kampuni ya *Twiga Cement* ambayo kwa sasa hivi inaagiza *gypsum* kutoka nje wakati jirani zetu wa Msumbiji wanachukua *gypsum* kutoka Kilwa; Haioni inatunyima haki na kuwakwaza wachimbaji wadogo wadogo katika kujinufaisha na kuondokana na umaskini? Ahsante! *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Naibu Waziri, Wizara ya Nishati na Madini tunatambua kwamba pamekuwepo na migogoro mingi katika maeneo mbalimbali ikiwemo wachimbaji wadogo wadogo ama kuingilia sehemu ambazo ni hifadhi ya Taifa ama kuingilia maeneo ambayo tayari yana leseni kubwa. Lakini kwa kutambua hilo tumechukua hatua zifuatazo:-

Tumeanza na Kanda ya Ziwa ya Magharibi kuwasiliana na wale ambao wana leseni kubwa kutenga maeneo maalum ili kuweza kuyabainisha kama maeneo ya wachimbaji wadogo wadogo. Wenye leseni kubwa kama *Barik* wamekubali katika maeneo fulani *Ayemu Gold* imekubali kwenye maeneo fulani na wengine sehemu mbalimbali, kitu kikubwa ambacho tunafanya sasa hivi ni kuhakikisha yale maeneo tunapoyachukua tuyapangilia vizuri ili wale wachimbaji wadogo wadogo wasiingie kwa kuyavamia, waingilie kwa mpangilio ambao itabidi wafuate sheria ya kuwa na leseni.

Swali la pili juu ya Kampuni ya *Twiga Cement* kuagiza *gypsum* nje tunajua kwamba kuna *gypsum* Kilwa ambayo ina ubora nzuri sana kuliko sehemu nyingine hapa

Tanzania. *Gypsum* ya Kilwa wanaitumia walikuwa na tatizo moja kwamba kuna kipande cha barabara, ambayo ni barabara kubwa ya *TANROAD* ambayo kufika kwenye njia inayopandisha kuelekea *gypsum* inakopatikana kinakuwa kibovu sana wakati wa masika, waliomba Serikali za Mitaa inayohusika sehemu hiyo watengeneze hicho kipande halafu na wenyewe kipande kinachochipuka kutoka kwenye hiyo barabara kuu kwenda kwenye machimbo ya *gypsum* ambacho ni kama kilomita 20 wakitengeneze wao kusudi pawepo na uhakika wa kupata *gypsum* nyakati zote.

Wakati wa masika inashindikana, na ikishindikana inabidi watoe *gypsum* kwingine kama Makanya, Itigi au kutoka nje. Tunaomba Waheshimiwa Madiwani wa sehemu hizo wahakikishe kwamba maeneo hayo yanatengenezwa vizuri kusudi na wenyewe pawepo na uhakika wa kuwa wanatoa *gypsum* nyakati zote za masika ama za jua. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, maswali yamekwisha na muda wa maswali umepita. Matangazo, kwanza nimeandikiwa barua mbili hapa zinasema kwamba Mheshimiwa Halima Kimbau, kavaa sare ya Chama cha Mapinduzi. Na kuuliza kama hii ni sahihi. Kanuni hazikatazi na pia hapa nilipo sioni sketi yake. Kwa hiyo, sijui amevaa sketi ya rangi gani. Kwa hiyo, nadhani amevaa nadhifu la kijani na linampendeza. Ahsante sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, ninayo furaha kubwa ya kutangaza mgeni mashuhuri kutoka Marekani, huyo si mwingine ni Pastor Herbert Lusk, Mjumbe wa Bodi ya Ushauri ya Rais Bush kuhusu UKIMWI. *(Makofi)*

*Pastor Lusk, could you please stand up so that the Members of Parliament can acknowledge you.* Alaa hayupo? Basi sikuwa najua, naona labda ametoka. Huyu licha ya kuwa ni Mshauri katika Bodi ya Ushauri ya Rais George Bush kuhusu UKIMWI pia ni mchezaji mashuhuri wa zamani wa ile *American Football* alikuwa nyota. Ahsante na tunamkaribisha. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa Mwenyekiti wa Umoja Wabunge wa Mkoa wa Iringa, Mheshimiwa Galinoma, anaomba leo saa 7 mchana Wabunge wote wa Mkoa wa Iringa mkutane kwa mkutano mfupi chumba namba 221, Wabunge wa Mkoa wa Iringa chumba namba 221 saa 7 mchana leo.

Mheshimiwa Zitto Kabwe kwa niaba ya Kiongozi wa Upinzani Bungeni, ameniomba nitangaze kwamba Wabunge wote wa Kambi ya Upinzani watakuwa na kikao chao saa 7 mchana mara baada ya Bunge kuahirishwa katika ukumbi namba 219 ghorofa ya *pili wing (b),* Wabunge wote wa Kambi ya Upinzani saa 7 mchana ukumbi namba 219 hii leo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Ali Ameir, Katibu wa Kamati ya Wabunge wa Chama cha Mapinduzi, ameniomba nitangaza kwamba Wabunge wote wa Chama cha Mapinduzi, leo kuna mambo gani sijui. Wapinzani wanakutana, CCM wanakutana basi kutakuwa na

mkutano wa Kamati ya Wabunge wa Chama cha Mapinduzi mara baada ya kuahirisha Bunge jioni. Kwa hiyo, Wabunge wa CCM katika ukumbi wa Pius Msekwa mara baada ya kuahirisha Bunge basi inaweza kuwa ni jioni au usiku kutegemea na wachangiaji. Kwa hiyo inaweza ikawa saa mbili kasoro robo. Hayo ndiyo matangazo, namwomba sasa Katibu kwa orodha ya shughuli zilizobaki.

## HOJA ZA SERIKALI

### Hali ya Uchumi kwa Mwaka 2006, Mpango wa Maendeleo kwa Mwaka 2007/2008 na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa Mwaka 2007/2008

*(Majadiliano yanaendelea)*

**SPIKA:** Kabla sijamwita msemaji ambaye nitawatangaza majina ni kwamba kuna simu ambayo Mheshimiwa Mbunge amebadilishana na simu ya mwenzie. Kwa hiyo, Mheshimiwa Balozi Seif Iddi, Naibu Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa, anayo simu ambayo si yake na anahisi kwamba pale nje wakati wa kuingia amebadilishana, mwingine akachukua simu ambayo si yake naye sasa ana simu si yake. Naomba mhusika basi waonane ili waweze kubadilishana.

Waheshimiwa Wabunge leo tuna wazungumza 22 bado, nadhani tutamaliza jioni. Orodha yangu naanza na Mheshimiwa Chacha Wangwe, anafuata Mheshimiwa Adam Malima, halafu Mheshimiwa Hafidh Ali Tahir na Dr. Harrison Mwakyembe kwa mpangilio huo. Sasa Katibu kwa shughuli zinazofuata? Tunaendelea.

**MHE. ADAM K.A. MALIMA:** Mheshimiwa Spika, naomba nianze kwa kukushukuru kwa kunipa nafasi hii. Na kama walivyofanya wenzangu walionitangulia naomba niwapongeze sana Mheshimiwa Zakia Meghji, Waziri wa Fedha na Mheshimiwa Alhaj Juma Ngasongwa, Waziri wa Mipango, Uchumi na Uwezeshaji.

Ama Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Wanamkuranga wote niungane na Watanzania wenzangu niwape pole ndugu zetu waliofiwa na wapendwa wao kwenye ajali mbalimbali ikiwemo hii ya hivi majuzi ya *Mohamed Trans* huko Singida.

Mheshimiwa Spika, naomba pia niitumie nafasi hii kuwapongeza sana sana *Taifa Stars* kwa ushindi katika mazingira magumu sana. *Taifa Stars* wametupa somo ambalo sisi sote humu ndani tunaweza tukalitumia. Naomba pia nitambue hotuba zote za Wabunge wenzangu walionitangulia kwa pande zote na ama niseme pia kwamba naunga mkono hoja hii asilimia 100 na pamoja na kwamba Waheshimiwa Wabunge wenzangu wa Kambi ya Upinzani wengine wamekataa kuinga mkono hoja japo wamekiri kuna mambo mengine mazuri mazuri, basi mimi nafikiri katika *mathematical propoRtions* wangesema wanaunga mkono japo asilimia 50. Lakini ukisema huungi mkono kabisa maana ni kwamba yote hukubaliani nayo, wakati wao wenyewe wanakiri kuna mambo mazuri mazuri.

Naomba nitambue katika hilo na niwa-*recommEnd* kusema kweli, naomba unipe nafasi hii ya kuwapongeza, Mheshimiwa Mnyaa na Mheshimiwa Ibrahim Sanya, hasa pale waliposema jana kwamba kazi yao kama Wabunge wa Upinzani, si kupinga tu. Bali kukosoa ili kuboresha. Mimi nafurahi kwamba wao wanalifahamu hilo. *(Makofi)*

Kazi yetu hapa sisi wote ni uboreshaji wa Bajeti na mpango huu ili tupate utekelezaji unaoelekea kwenye kufikia malengo ya Ilani ya Uchaguzi ya CCM, MKUKUTA na maisha bora kwa kila Mtanzania. Katika mandhari haya, Bajeti ya Serikali, naomba niungane na Mzee wangu, Baba yangu, Mzee Mzindakaya, kwamba wakati tunajadili hapa tujue kwamba kuna Bajeti moja tu. Na hakuna Bajeti mbadala. Hii *concept* ya *alternative Budget* ni *missleading.* Wanayoleta ndugu zetu ni maoni ya maeneo yao ili kuboresha kwa maoni yao kwa mtazamo wao. Na sisi pia tunaleta, lakini Bajeti ni moja tu, na ili ulete Bajeti humu ndani lazima uwe na Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa mwenye kutaka kuleta Bajeti, siyo leo sasa labda 2010 na kwa hali hii labda 2011 na kwa hali hii kwa Rais huyu na chama hiki na Serikali hii, sijui tena labda 2020. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ukweli ni kwamba sisi kwenye Kamati ya Fedha na Uchumi tulipata bahati ya kukaa na Wizara hizi mbili kabla haujaja hapa. Kwa hiyo, tunajua *constraints* walizokuja nazo kwenye Kamati, walikuja na maombi ya trilioni 12, wakati mapato kwa vyanzo vya ndani ni trilioni 3.5. Hiyo ndiyo *reality* yenyewe. Kwa hiyo, kwa mahitaji yao wenyewe walikuwa wanahitaji trilioni 12, *they had a short fall of 8.5 trillion.*

Mheshimiwa Spika, kwa hali hiyo, tunasema Bajeti ya leo ina trilioni 6, hilo ni ongezeko la 22% ya asilimia 23 kwa Bajeti ya mwaka jana. Sasa kwa namna yoyote ile hata tungechukua Bajeti ya mwaka jana tukaiongezea asilimia 10 basi vyanzo vya leo vingetukidhi kwa asilimia 65. Lakini *what is happening? The country is growing, we are moving forward. We are expanding.* Kwa hiyo, *in economic theory* kwa sababu tuna-*expand* mahitaji yetu ni makubwa zaidi. Kwa hiyo, 4.85 ya mwaka jana kwa leo haitutoshelezi *now we need six trillion, just to make it.* Ili turuke tu pale tunahitaji 6 trilioni. Na *what are the contraints? What is the difference* baina ya mwaka jana na mwaka huu?

Mheshimiwa Spika, kama alivyosema Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi, Mama Sitta, ametuambia hapa, kwamba *we have a thousand eight hundred new schools.* Sasa *unless* tukiwa tayari ku-*invest seriously* katika shule hizi, tutakachokuwa nacho ni magofu na tutakuwa na watoto ambao wanakwenda asubuhi wanacheza wanarudi jioni. *What is the reality of these schools?* Tunahitaji shule mpya, madarasa mapya 3,000, walimu si chini ya 18,000, mabweni ili waharibifu wasiwakatishe shule mabinti zetu. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tusipojenga maabara tutakuwa na *artists* tu hatutakuwa na *engineers* wala *doctors, that is the reality. So, we have to spend and all these things* zinahitaji pesa. Na kwa sababu hatukushinikizwa na mhisani kujenga mashule, hii ni

*choice* yetu sisi, *it means* kwamba lazima tufanye *descision* humu ndani ya ku-*finance choice* zetu *by our own money. (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, *we have another reality* tuna *reality* ya barabara ya miundombinu. Huwezi kuleta bidhaa kutoka Singida, Lindi, Sumbawanga, Kigoma na kadhalika kama huna barabara. Tutawahimiza walime mazao mbadala na kadhalika na kadhalika, wanaletaje mazao haya sokoni, *their export products* wanaletaje bandarini Dar es Salaam, *it is impossible.*

Mheshimiwa Spika, *this is the economic reality* lazima humu ndani tufanye maamuzi leo katika Bajeti hii ili tusiyafanye baadaye wakati ambapo ni gharama zaidi kuyafanya. Kilimo cha bidhaa asilia kimeshuka. Jana ndugu yangu Mheshimiwa Vita Kawawa alisema. Sasa naomba nitambue pia kwamba kama ilivyokuwa, ni kazi yetu kuboresha, naomba niseme kwamba mpango wa mwaka huu umelalia mno kwenye kisingizio cha ukame. Bidhaa za asilia zimeshuka kwa mambo mengi. Kuna matatizo ya pembejeo, kuna ruzuku za maendeleo ya mazao. Kuna uwekezaji duni katika *agriculture.* Tuna ukosefu wa mikopo katika kilimo. Kila unapokwenda benki katika mabenki haya wanasema *there is a high risk factor* katika kilimo, sasa *what is the solution, how do we move forward?* Hili ndiyo tatizo la ukweli.

Mheshimiwa Spika, mwaka 1973 Tanzania ilikuwa inazalisha tani 140,000 za korosho, leo tukizalisha tani 70,000 *we barely make it,* ni bahati. Sasa Wana mipango watuambie, ili washirikiane na Kilimo na Fedha watoe fedha. *How are going to move from the current* 75,000 *tons* za korosho twende kwenye 140,000 ambazo tulifanya miaka 30 iliyopita halafu tuende kwenye 200,000. *This is how we are going to move forward.*

Vietnam wamekuja kuchukua mbegu za korosho kwetu, sasa wanazalisha *400,000 tons* za korosho, *it is not right.* Lazima mipango yetu ielekee katika ku-*expand.* Leo hii Mkuranga, zao letu kuu ni korosho. Nikipata milioni 750 kwa ajili ya kuendeleza zao tu, ndani ya miaka minne nitazalisha tani za ziada 10,000 zitakazokuwa na thamani ya 5.2 bilioni, *just from 750 million in four years.* Sasa *spill over effects* zake ni kubwa mno, na hii inaweza ikafanyika kwa tumbaku, kwa pamba, Mheshimiwa Shah ananikumbusha samaki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lazima tuangalie *planning* katika mfumo huu. Pana suala la mfumo wa kodi. Ni kweli kwamba lazima tuangalie mfumo wa kodi kama kitu chenye uhai. *The tax system is a live*, ina-*move through time. Tax meassures* tunazochukua leo hapa, tungeziweka mwaka 96 wakati *TRA* ina mwaka mmoja nchi ingesimama, *the country was not ready. The tax administrative framework was not ready. The tax paying public was not ready.* Sasa leo tunakusanya 250 milioni kwa mwezi na tunampongeza *Commissioner General,* siyo bahati*, it is not by chance. This is because of ten years* ya *building up capacity* ya kiuchumi lakini *building up capacity* ya walipa kodi.

Sasa, *some where, some how,* lazima tufike kwenye ulipaji kodi wa milioni 500 kwa mwezi. Sasa *because the tax system is growing*, inakua, tunaamini kabisa mimi naamini na nawaomba ndugu zangu Waheshimiwa Wabunge msihofu suala la *fast trucking* na *traders compliance.* Hii inafanywa pia kwa ajili ya kuwarahisishia kazi na kuongeza uzalishaji hao wazalishaji. Sasa hapa tumezungumzia tukasema kuna wengine watatumia kuingizia unga. Huyo ambaye alikuwa anasubiri hili jambo ili aongIze unga alikuwa na mipango yake tangu zamani, siyo mfanya biashara.

Mheshimiwa Spika, lazima Serikali ituambie hapa kwamba kama tunawaridhia hii f*ast trucking* na *traders compliance* pia watuambie kwamba mtu yoyote atakaye-*abuse system* hii, ukarimu huu, ambao sisi tunafanya ili wao waongeze uzalishaji, mtu aki-*abuse* basi *penalty* zake wenzake waone na asipatikane mwingine yoyote wa kufanya tena hivi.

Mheshimiwa Spika, kuna suala la mafuta na kodi za leseni. Lazima tukubaliane kwamba kuongeza kodi ya mafuta kunaweza kuongeza bei ya bidhaa hiyo, na *most likely* itafanya hivyo. Mfumko wa bei na kadhalika. Lakini jamani tuangalie ukweli wa mafuta, leo bei za mafuta leo hii bei ya mafuta ni *69 dollars per barrel* sababu, siyo kwa sababu Mheshimiwa Mama Zakia Meghji ameongeza kodi, ni *69 dollars per barrel* kwa sababu ya nini, ni kwa sababu kuna matatizo ya Iraq na Iran, US na Iran, kuna matatizo Nigeria kwenye *oil fields.* Sasa hii ndiyo ukweli, kwa hiyo, leo hii basi bei za mafuta zikishuka kwenda *USD* kwa mfano 40 kwenye *world system* hata kama tukiwa na kodi ya shilingi 200 kwa kila lita bado tutaweza kununua mafuta humu ndani kwa 900/=. Kwa hiyo, kuna *factors* nyingi na tatizo lingine ni *syndication ya* wauzaji wa mafuta humu ndani, lazima tuangalie vyombo kama *EWURA* vinafanya kazi yao ili kuwadhibiti.

Mheshimiwa Spika, kuna suala la kodi la leseni, naomba nikubaliane na Mheshimiwa Masolwa kwamba shilingi elfu 80 kwa pikipiki ni kubwa sana namwomba Mheshimiwa Waziri wa Fedha aliangalie. Laki mbili na elfu 30 kwa mtu mwenye Benzi halafu ukamtoza tena mwenye *Corolla* bei hiyo hiyo halafu pengine kuna *pick up* ya Mheshimiwa Fuya kule kwake Milimani zinapanda na kushuka na mizigo na abiria vitu hivi naomba kwamba *classification* iliyofanywa isizingatie uzito wa injini tu, kuwe na viashiria vingi zaidi ili tupate mapato haya haya ya milioni 192 lakini kwa mfumo ambao unakuwa karimu zaidi kwa walipa kodi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuna suala la sekta ya Fedha. Mazingira ya Biashara ya Fedha humu ndani ni mazuri mno Tanzania. Hakuna hata Taasisi moja ya fedha inayopata hasara. Sasa Serikali inasema haitakopa tena. *Fine* Bajeti lazima ielekeze wazi kwamba Benki zitaingia katika sekta ambazo zina mashaka nazo. Awamu ya pili ya maboresho ya sekta ya fedha kama ilivyotajwa na Mheshimiwa Waziri ni sehemu kamili ya utekelezaji wa MKUKUTA lakini hauendani sambamba na *speed* tunayoitaka. Tunataka mikopo na riba *interest rate* yake zipungue.

Mheshimiwa Spika, ni muhimu sana kwamba sekta ya kilimo ipatiwe *collateral* iwe inapatiwe *guarantee from somewhere* ili hawa watu wa *financial sector* waache kusema kwamba kilimo *is too expensive to finance.* Lazima tuwe na mfumo wa

*development finance. Financing developing is specific* haifanyiwi tu na *Commercial Bank.* Kwa hiyo kwa maana hiyo lazima *TIB* wawezeshwe. Kama sekta ya fedha haikwenda sambamba na sisi tutapata taabu. Utekezaji wa MKURABITA utakuwa hauna maana, na uwezeshaji wa kiuchumi utakuwa utaangalia upande mmoja tu kwa wale ambao wana uwezo wa kwenda benki na kukopa.

Mheshimiwa Spika, mwisho adui mkuu wa Bajeti na mpango *as it is* leo ni udhaifu wa usimamizi. Tunagombana kugawa rasilimali humu viduchu. Tukishagawa nani anayetuthibitishia kwamba maamuzi haya tuliyofanya ni sahihi. Utaalamu wa kubuni vyanzo ni mdogo. Lakini utaalamu wa kusimamia *capicity building* kwenye Kamati tumemwomba Waziri wa Mipango na tumemwomba Waziri wa Fedha kwamba wafanye kila linalowezekana kufanya *reallocation* ndani ya Wizara zao ili waongeze taaluma ya usimamizi wa pesa tunazopeleka chini. Kuna Kitengo pale kwenye Wizara ya Fedha kinaitwa *Expenditure Trucking Unit* ambacho kinafanya kazi ya kufuatilia fuatilia hizi pesa ambazo zimekwenda huko kwenye Halmashauri na Mawizara na kadhalika. Namwomba sana Mheshimiwa Waziri wa Fedha ajaze watu kwenye kitengo hiki na ajaze fedha, *we are spending in order to save. (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kama tunatumia milioni 200 kwa ajili ya kuokoa bilioni 2 mimi nadhani *that is the right way forward.* Katika kumaliza hilo naomba niseme kwamba wakati ambapo Rais na Waziri Mkuu wanaamrisha mdundo, watu wachangamkie, naiomba Serikali iboreshe usimamizi wa matumizi ya fedha na rasilimali na ikiwezekana watendaji wake wakuu wapewe *performance related contracts* ili kila Mkurugenzi au kila Katibu Mkuu anapokuwa na lengo anapewa lengo anaambiwa kazi yako wewe ni kusimamia fedha *one, two, three, four.* Ameshindwa kutekeleza lengo lile maana yake anashindwa kazi yake. Tukikaa tunawabana hawa *political responsibles* tujue kwamba na wao hiki wanacholeta hapa wanaletewa na wataalam wao. Kwa hiyo, mimi ninaomba niseme kwamba kwenye kubana na kusimamia matumizi ya fedha na rasilimali ndiyo kwenye funguo ya matumizi mazuri kwa kuzingatia kidogo tulichokuwanacho.

Mheshimiwa Spika, maisha bora kwa kila Mtanzania naomba nipingane na Wapinzani yanawezekana kwa bajeti hii. Nakushukuru sana, ahsante. Naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. HAFIDH ALI TAHIR:** Mheshimiwa Spika, na mimi nikushukuru kama wenzangu walivyofanya katika kunipatia nafasi ya kusema machache katika bajeti hii ya Serikali na kwanza kabisa nisije nikasahau labda kwa jazba au ragba kuunga mkono hoja kwa asilimia moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda sana kuzipongeza sana Wizara zote mbili kwa Bajeti walizozileta katika Bunge letu Tukufu. Lakini vile vile niungane na wenzangu wote waliopongezwa na vile vile waliopata misiba na mambo mengine kama hayo, basi naungana na wenzangu katika kuwapongeza na kuwafariji katika misiba yao.

Mheshimiwa Spika, kwa sababu ya muda kabla sijaingia katika ule Waraka wangu wa michango niliotaka nifanye naomba unipe ruhusa kwanza nitie nyama katika mambo mawili. Napenda nitie nyama katika jambo la kwanza lililozungumzwa na Mkuu wa upande wa Upinzani katika hotuba yake ambayo amewasisha hapa Bungeni, halafu pia naomba nitie nyama pale ambapo tulipoambiwa kwamba Warsha, Sermina na mambo mengine yanapoteza pesa bure za wananchi wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, katika hotuba ya Mkuu wa Upinzani alisema hivi nanukuu kipande kidogo tu. Watanzania walio wengi wanapenda kuwa na imani na kauli ya Rais na sisi katika Kambi ya Upinzani tunaahidi kufuatilia kwa karibu mwenendo mzima wa mazungumzo huku tukielewa kuwa muda wa subira nao unazidi kuyoyoma.

Mheshimiwa Spika, mazungumzo haya ni ya muafaka. Ninachotaka kutia nyama ni kwamba aliyoleta wazo hili ndani ya Bunge hili la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania la kwamba anakereketwa na mpasuko wa kisiasa kule Zanzibar ni Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Jakaya Kikwete. *(Makofi)*

Na hili alilisema wazi, lakini sasa kwa bahati nzuri aliyetoa Waraka huu yeye yumo kwenye Kamati ya Muafaka. Na nina hakika Mheshimiwa Kikwete alipozungumza pale hakuna hata mahali pamoja katika hotuba yake alisema kwamba kutokana na kukasirishwa kwake yeye basi anashirikiana na nchi moja ya nje au anashirikiana na Marekani. Sasa la kushangaza ghafla wenzetu wamekwenda Ubalozi wa Marekani. *(Makofi)*

Mazungumzo Mheshimiwa Spika, yanaendelea. Na Mwenyekiti wa Chama cha Mapinduzi akiwa ni Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwamba yeye atahakikisha haya mabo yanakwenda vizuri. Sasa iweje tena wenzetu hawa wanaacha Chama cha Mapinduzi wanakurupuka na kwenda ubalozi wa Marekani. Walipofika kule wakaulizwa mnasemaje, wakasema tumekuja kumshitaki Makamba. Wakaulizwa kafanya nini Makamba, Makamba Pemba alisema kwamba uchaguzi haurudiwi.

Lingine, wakasema kwamba kama Yanga wameshinda basi si vyema Yanga wakawapa ushindi Simba. Mambo ya kitoto haya. Wanachama wa sehemu hizi wameandamana kwa sababu hizi, sasa Mheshimiwa Makamba ni mmoja katika watu ambao wanashiriki katika mazungumzo. Sasa kama kuna kasoro wenzetu hawa wasingekwenda Marekani. Rais Jakaya Kikwete yupo ndiyo aliyeleta muafaka huu. Lakini alichosema Katibu Mkuu Makamba, uchaguzi haurudiwi. Mheshimiwa si tuna katiba, hii katiba ipo hapa Jamhuri.

**SPIKA:** Mheshimiwa Hafidh, mada iliyopo mbele yetu hapa, inahusu hotuba ya Waziri wa Fedha na hotuba ya Waziri wa Mipango. Ningeomba ujitahidi basi urejee katika hayo.

**MHE. HAFIDH ALI TAHIR:**Ahsante sana. Nilisema mwanzo kwamba naomba nitie nyama, lakini kwa kauli hiyo nataka nirudi kwenye mada baada ya neno langu la

mwisho kusema kwamba bila shaka ujumbe umefika na waliotakiwa kutekeleza waendelee kutekeleza yale ambayo yametakiwa na Rais Jakaya Kikwete. *(Makofi)*

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Kuhusu utaratibu.

**SPIKA:** Utaratibu kwenye Kanuni ipi?

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Kanuni ya 50 kipengele cha saba, kipengele cha 8.

**SPIKA:** Endelea!

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Ni marufuku kwa Mbunge yeyote kutumia lugha ya kuudhi. Wakati Mheshimiwa hapa akitoa mada yake ambayo umeizuia alitumia neno kiherehere. Sasa naomba unipe mwongozo wako kama neno kiherehere ni muhimu kutumika katika Bunge hili.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, neno *kiherehere* katika mazingira ambayo alikuwa akizungumza Mheshimiwa Mbunge lilikuwa ni sahihi kwa sababu ni kwenda kimbelembele au kujiweka kimbelembele katika jambo fulani. Lakini nimekwisha mrudi na Mheshimiwa amekwisha rudi kwenye mada kwa hiyo, tuendelee! (*Makofi*)

**MHE. MASOUD ABDALLAH SALIM:** Kuhusu utaratibu!

**SPIKA:** Huwezi kurudia hilohilo, nimekwishatoa maamuzi. Mheshimiwa Hafidh Ali Tahir tuendelee!

**MHE. HAFIDH ALI TAHIR:** Mheshimiwa Spika, niendelee kukushukuru tena na kwa busara zako unajua kila mtu ana namna yake ya kuelewa jambo linapozungumzwa.

Mheshimiwa Spika, muungano wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania una faida zake na mimi kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Dimani basi sisemi kwamba Muungano huu una hasara zake. Ninachosema ni kwamba Muungano una faida zake na utaendelea kuwa na faida kwa wananchi wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Wakati nilipokuwa naipitia bajeti hii nilikuwa naangalia sana Waziri na Serikali wameiangalia vipi Zanzibar kwa sababu ndani ya Bajeti hii kuna sehemu zinagusa Zanzibar moja kwa moja, na nilichokuwa nakitegemea ni kwamba Waziri ataweza kuweka msukumo katika maendeleo ya Zanzibar ndani ya bajeti hii. Lakini cha kusikitisha ambacho sikukiona ni pale ambapo nilikuwa namtegemea Mheshimiwa Waziri na kwa bahati nzuri sijui kwa nini Serikali inafanya hivyo, maana yake mara zote katika miaka yote Mawaziri wanaoingia katika Wizara ya Fedha basi kama siyo Waziri, Naibu wake atakuwa anatoka Zanzibar. Sasa nilikuwa nategemea sana hapa tuweze kuona msukumo lakini nilipokuwa nakipitia kitabu hiki nimekuta kurasa za 23, 47 na 51 peke yake na kurasa za 23 na 47 hazizungumzi tija itakayopata Zanzibar katika bajeti hii, lakini ukurasa wa 51 peke yake ndiyo unazungumza nini kitapatikana kule Zanzibar. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, sasa Mheshimiwa Waziri Zakia Meghji na Abdisalaam Issa Khatib bahati nzuri kwangu mimi kidogo hawa wote nawaita Wazanzibari. Maana kule Zanzibar kuna mtu mmoja anaitwa Mariam Hamdani ndugu yake Mheshimiwa Waziri. Sasa mimi nilikuwa naona atafanya jambo ambalo litaisaidia Zanzibar katika maendeleo. Kwa nini nikasema hivyo?

Nimesema hivyo kutokana na ujio wa 4.5 ndiyo maana nikaelekea huko na hili limekuwa likizungumzwa sana kuwa ni kiwango cha fedha ambacho kinapewa Zanzibar katika utaratibu ambao umewekwa. Lakini ukurasa 113 wa Katiba, ukurasa wa 113 wa kitabu hiki cha Mheshimiwa na Ibara ya 133 vinazungumzia habari ya makusanyo na mambo mengine. Lakini ninachotaka kusema ni kwamba sasa hivi pesa zinazopatikana kwenda Zanzibar katika 4.5 ni kutokana na fedha za nje na faida ya benki ambazo fedha hizi zilianza kutolewa tangu mwaka 1995. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lakini ukiingalia Katiba hii ya 1977 suala hili limezungumzwa na kinachotakiwa na Zanzibar na ninaiomba sana Serikali ielewe, kwamba nalisema suala hili wala silisemi kwa jazba, hapana! Nalisema katika lugha laini. Kinachotakiwa kwa Zanzibar sasa hivi ni kwamba Zanzibar inasonga mbele, inataka maendeleo, kwa hiyo, kinachotakiwa ni kupewa gawio lake katika fedha zinazopatikana kwenye makusanyo ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kung'ang'ania kuipa asilimia 4.5 ya fedha zinazopatikana kwa fedha za nje na Benki Kuu wakati umekwishapita. (*Makofi*)

Katika Mwaka wa Fedha 2006/07 mimi nashukuru kwamba angalau hiyo 4.5 Zanzibar tumepata bilioni 21, sawa! Lakini bilioni 21 bajeti ya mwaka jana ni bilioni 276! Sasa naiomba sana Serikali, zile Halmashauri ambazo zimewekwa za Waziri Mkuu na Waziri Kiongozi, hii miaka 31 sasa hivi inayokaribia imalize hii kazi ili Zanzibar iweze kupata mgao wake katika kipato kinachopatikana katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, isiwe kila siku tupo tu tunasikiliza kuna watu wanakutana, tunaomba wamalize kukutana ili Zanzibar iweze kusonga mbele ikiwa ndani ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, nimeingiwa na hofu kidogo, na hofu yangu ninaiomba sana Serikali itambue kwamba katika Muungano tulifika pahali tukawa tunasuguana kidogo maana ndiyo kawaida vikombe huwa vinagongana je, binadamu? Sasa katika ile misuguanosuguano ikaonekana labda siku nyingine kuna kiongozi mmoja mkaidi kaidi kule Zanzibar. Sasa kama hiyo iliwahi kutokea huko nyuma na halafu likatolewa agizo labda hawa Zanzibar wanajidai jeuri na kiongozi wao lazima tuwakomoe. Wakati umeshapita, nasema kama lipo basi liondoke na kama halipo Serikali ikae iangalie Zanzibar kwa jicho la huruma, iangalie Zanzibar kama sehemu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwamba ni moja katika sehemu ambayo viongozi wetu wawili walikaa kwa hiari na kwa mapenzi na kwa kuthamini utu wa wananchi wao pande zote mbili, kwa kuona kwamba sehemu moja kubwa na moja ndogo basi hizi zikutane pamoja zisaidiane ili na nyingine iweze kwenda mbele.

Mheshimiwa Spika, kwenye Katiba humu hakuna Rais mkubwa au Rais mdogo, hakuna humu! Humu kuna Marais wawili, mmoja wa Zanzibar na mwingine wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Mna Zanzibar ambayo ina Serikali yake na Baraza lake la Wawakilishi na ina shughuli zake na kuna Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naiomba sana Serikali ifike mahali shughuli hizi zinazozungumzwa sasa hivi ambazo zinakaribia kwenye miaka 25, 26 na 30 zimalizwe kuzungumzwa ili Zanzibar ijenge barabara kama wanavyolilia mikoa mingine kujengewa barabara. Zanzibar ifanye biashara hasa ikiwa kisiwa kama tunavyofanya biashara nyingine.

Mheshimiwa Spika, sasa hivi Zanzibar inakufa kibiashara, kiwango cha fedha ambazo zilikuwa zinakusanywa Zanzibar shilingi milioni 13 kwa mwezi katika bandari sasa Zanzibar inakusanya shilingi milioni 2, haiwezekani! Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ikae kitako ione kwamba tuna upande mwingine wa Jamhuri ambao unataka kusaidiwa na sehemu moja ilikuwa kubwa.

Mheshimiwa Spika, naomba nafasi yangu ya ……!

**SPIKA:** Nakuongeza dakika mbili kwa sababu kuliingia mambo ya utaratibu.

**MHE. HAFIDH ALI TAHIR:** Mheshimiwa Spika, kwa hiyo nafikiri hilo limefahamika na ninaiomba sana Serikali tufike mahali tuweze kuona kwamba Zanzibar inapata 4.5 lakini inapata mgao wake kutoka katika makusanyo ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kama Katiba hii inavyosema.

Mheshimiwa Spika, kuna mambo haya yamezungumzwa mimi nakwenda sana kwenye mafuta sasa kwa sababu nimepewa dakika mbili.

Suala la mafuta na mimi nalizungumza makusudi …….!

**SPIKA:** Imebaki dakika moja sasa!

**MHE. HAFIDH ALI TAHIR:** Mheshimiwa Spika, sawa!

Nalizungumza kwa makusudi kwa sababu nina hofu, kuna wenzetu upande wa pili wamezungumza suala la mafuta isije ikaonekana kama wao ndiyo wametetea sana na sisi huku CCM tumenyamaza kimya, linatukera. Suala la upandisha mafuta linatukera.

Wazo langu na shauri langu kwa Serikali ni kwamba hapa kuna suala la pombe, pombe hapa sisi Watanzania si walevi sana japokuwa Mheshimiwa mmoja juzi alisema vijengwe viwanda vingi vya pombe tupate kulewa, Tanzania haina walevi bwana! Haiwezekani! (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ninachosema mimi ni kwamba tuangalie katika sehemu ya pombe tunaweza kusaidia vipi katika suala la mafuta maana mafuta tunachozungumza sasa hivi mafuta ya taa yamezidi kiasi gani? Ni shilingi nne, dizeli imezidishwa kwa shilingi 20 na petroli imezidishwa kwa shilingi 22, ukizijumlisha hizi ni shilingi 46.

Mheshimiwa Spika, hizi tuzipeleke kwenye pombe, sigara ili tuwapunguzie wananchi wetu mzigo wa mafuta ya taa.

Mheshimiwa Spika, baada ya kunipa nafasi hiyo narudia tena kuunga hoja. Ahsante sana.

**MHE. DR. WILBROD P. SLAA:** Mwongozo wa Spika!

**SPIKA:** Mwongozo wa Spika kwanza.

**MHE. DR. WILBROD P. SLAA:** Mheshimiwa Spika,….!

**SPIKA:** Kifungu!

**MHE. DR. WILLBROD P. SLAA:** Mheshimiwa Spika, Kifungu cha 55(3).

Mheshimiwa Spika, wakati msemaji aliyemaliza sasa hivi alipokuwa akizungumza ametoa maneno ambayo yanaweza kuwa ni tuhuma nzito sana ikizingatiwa kuwa taifa letu sasa hivi linafuatilia mazungumzo yanayoendelea kati ya Chama cha CCM na CUF. Mazungumzo haya yanalenga muafaka, kuleta amani katika taifa letu, utulivu na kuepuka yaliyotokea kule nyuma.

Inapotolewa tuhuma nzito kwamba kuna mtu amekwenda kushtaki kwa ubalozi wa nje nadhani ni vema Bunge hili likaelezwa huyu aliyekwenda kushtaki ni nani? Alikwenda kushtaki tarehe ngapi? Aliyeshtaki ni kati ya wale wanaohusika na mazungumzo au huyu anayeleta hii taarifa Bungeni alikuwepo kwenye mjadala huo na alishiriki au ana ushahidi gani.

Nadhani kwa kifungu cha 50 tunatakiwa Bunge hili tuthibitishiwe tuhuma hiyo nzito iliyotolewa ndani ya Bunge hili.

Mheshimiwa Spika, nashukuru.

**SPIKA:** Tuhuma hii hata mimi niliisoma katika Vyombo vya Habari sasa si lazima awe alikuwepo ili kuitamka.

Kwa hiyo, nadhani anaweza tu akasimama akaelezea chombo alichosoma kuipata hiyo taarifa na inatosha kwa sababu tunaruhusiwa kunukuu yale ambayo tumeyasoma na hatuna wajibu tena wa kuwa lazima tulikuwa pale ama tulishiriki.

Mheshimiwa Hafidh!

**MHE. HAFIDH ALI TAHIR:** Mheshimiwa Spika, kwanza nikushukuru kwa maelezo yako. Lakini mimi ninaomba tu kwa ndugu zangu hawa wa upande wa Upinzani wanapoamka asubuhi wawe na desturi ya kusikiliza redio au kusoma magazeti. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ndani ya Tanzania kuna magazeti yamekubaliwa na kusajiliwa rasmi na Serikali na hivi ni vyombo maalumu ambavyo vimekubaliwa kutoa taarifa, sasa waanze kuwa na desturi hii kama niliyonayo mimi, kama wangefanya hivyo naamini kuwa wasingeleta suala hili leo.

Gazeti la tarehe 19 la Mwananchi hili hapa! na bahati nzuri hata wao hawajapinga yale yaliyoandikwa humu, sasa wapinge kwanza hili gazeti halafu wanitake mimi nizungumze nimeyapata wapi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nakushukuru.

**SPIKA:** Inatosha. Waheshimiwa sasa ni zamu ya Mheshimiwa Dr. Harrison George Mwakyembe atafuatiwa na Mheshimiwa Benson Mwailugula Mpesya.

**MHE. DR. HARRISON GEORGE MWAKYEMBE:** Mheshimiwa Spika, nianze kwa kukushukuru kwa kunipa fursa hii nami kuweza kuchangia kwenye mjadala unaoendelea.

Awali ya yote kwa niaba ya wapiga kura wa Jimbo la Kyela naomba nitumie fursa hii kutoa pole kwa Watanzania wote waliojeruhiwa na waliopoteza maisha yao kwenye ajali ya basi iliyotokewa Singida hivi majuzi.

Mheshimiwa Spika, ajali hii inatukumbusha swali la msingi lililoulizwa juzi hapa na Mbunge mwenzetu Mheshimiwa Brg. Gen. Hassan Athumani Ngwilizi, Mbunge wa Mlalo kuhusu fidia kwa majeruhi na watu wanaofariki dunia kutokana na ajali mbalimbali hapa nchini na ukweli ulijitokeza hapa kwamba kweli asilimia kubwa ya Watanzania wanaoathirika kutokana na ajali mbalimbali hawapati fidia. Yote hii inatokana na udhaifu mkubwa tulionao katika mfumo wetu wa bima nchini ambao unaruhusu ujanja ujanja katika kufanya biashara.

Mheshimiwa Spika, naomba nichukue fursa hii kusema kwamba mimi nadhani ni wajibu wa Polisi wa Usalama wa Barabarani ambao wako pale kupima hiyo ajali kuangalia *cover note* ya hilo basi, kuwakumbusha watu wote walioathirika mle ndani na ndugu zao wakapata hiyo fidia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nawapongeza vilevile Wabunge wenzetu wa kutoka Mkoa wa Singida ambao walihudhuria mazishi ya hao ndugu zetu. Lakini tutawapa pongezi nyingi zaidi ikiwa wao watafuatilia kuhakikisha kwamba kwa mara ya kwanza waathirika wote wa hiyo ajali wanalipwa fidia, hii si hisani ni haki yao. Siyo kwamba tunawapa kazi tu Wabunge wenzetu kutoka Singida bali hata sisi wenyewe Wabunge wengine kwa sababu hii ni haki ambayo wamenyimwa Watanzania kwa muda mrefu.

Ikitokea ajali Mbeya wafuateni Wabunge tuhakikishe kwamba mnalipwa fidia, hatuwezi kuwa tunalipa tu kwenye makampuni haya pesa tu inaishia mifukoni lakini kazi unayotaka kuifanya kisheria na kihalali kufidia watu wanaoathirika haifanyiki.

Baada ya kusema hayo naomba uniruhusu sasa niitumie fursa hii niwapongeze Mawaziri wetu wawili, Mheshimiwa Zakia H. Meghji Waziri wa Fedha na Mheshimiwa Dr. Juma A. Ngasongwa Waziri wa Mipango, Uchumi na Uwezeshaji kwa kazi kubwa waliyokuwa nayo iliyowakabili ya kuandaa bajeti ya mwaka 2007/08.

Mheshimiwa Spika, nasema hivyo kwa kuwa wote tunajua kwamba wenzetu walikabiliwa na mahitaji makubwa sana ya nchi zaidi ya shilingi trillion 12. Suala hili amelielezea vizuri sana Mheshimiwa Adam K. Malima hapa na uwezo wa nchi unajulikana ni shilingi trillion 3.5, hiyo ni kazi kubwa sana. Una mahitaji hayo makubwa na pesa uliyonayo kidogo, haya fanya miujiza! (*Makofi*)

Nafikiri kwa Wakrisho ni Yesu Kristo peke yake ndiye aliyefanikiwa kulisha watu 5000 kwa kipande kimoja cha samaki na kipande cha mkate. (*Makofi*)

Lakini sasa hapa yupo Mheshimiwa Zakia H. Meghji na Mheshimiwa Dr. Juma A. Ngasongwa huo uwezo hawana, kwa hiyo, cha msingi tu ni kupanga na kupanga kwa kuweka vipaumbele.

Mheshimiwa Spika, nashukuru kwamba Wabunge tulihusishwa kwenye zoezi hili, vipaumbele vyote vilivyopo pale tulihusika hata na sisi wenyewe kuvitambua.

Mheshimiwa Spika, nilichofarijika zaidi ni kwamba katika vipaumbele vyote vilivyojitokeza na kuainishwa nimefurahi kwamba elimu imepewa kipaumbele namba moja, huu ni uamuzi wa busara sana kwa sababu wenzetu walioendelea kutupita ambao wapo mbali kisayansi na teknolojia bado wameiweka elimu nambari moja katika mipango yao na yote hii wanatambua kwamba bila elimu hawawezi kwenda mbali zaidi ya pale.

Wengi mnakumbuka Waziri Mkuu wa Uingereza *Tony Blaire* alipokuwa anaingia madarakani miaka 10 iliyopita alisema “Kipaumbele nambari moja cha Serikali ya *Labour* kitakuwa ni elimu, kipaumbele namba mbili kitakuwa ni elimu na kipaumbele namba tatu kitakuwa ni elimu.” Lakini yote alikuwa anasisitiza kwamba bila elimu Uingereza haitakwenda mbele ya hapa ilipofikia. Mimi nashukuru kwamba tumefikia hapo, uelewa huo sisi na vilevile tumechukua hatua mbele kuonyesha uelewa wetu ndani ya bajeti. Elimu itachukua zaidi ya 18% ya bajeti nzima, hiyo nashukuru sana. Nina ombi moja tu kwa Serikali kwamba tumefanikiwa sana katika elimu katika kipindi kifupi sana chini ya Serikali ya Awamu ya Nne. Kufuatana na Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi tumejenga zaidi ya shule za sekondari 1084 katika kipindi kifupi sana cha miaka miwili. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nimefurahi sana kwamba Mheshimiwa Waziri Mkuu ameondoka hapa, angekuwepo ningeshindwa kusema hivyo kwa sababu ningekuwa kama

namwangalia machoni. Lakini tuwe wakweli, tunajivuna Wabunge hapa kwamba tumejenga shule nyingi sana kwenye majimbo yetu lakini kazi aliyoifanya Mheshimiwa Waziri Mkuu kutuhamasisha, kutusukuma ilikuwa kubwa sana na anastahili pongezi. Mimi sijawahi kuona ufuatiliaji wa karibu wa kiongozi wa ngazi ya juu kama alivyofanya Mheshimiwa Waziri Mkuu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lakini pamoja na mafanikio yote haya ya kujenga shule nyingi kuna dosari moja kubwa imejitokeza kwamba shule zetu karibu zote hizo hazina maabara ya Fizikia, Baiolojia na hata Kemia. Sasa hiyo ni hatari! Nchi hii itakuwa ni nchi gani ambayo haina wahitimu wa Sayansi. Kwa hiyo, naomba Serikali itumie sehemu ya bajeti hii ya Elimu kuchochea ujenzi wa maabara hata angalau moja moja katika kila Wilaya kutoa mfano wa ujenzi wa maabara sahihi.

Mheshimiwa Spika, mimi naamini kwamba ujenzi wa maabara ni ghali kuliko darasa la kawaida, ujenzi wa maabara unahitaji utaalamu wa kuzingatia usalama siyo tu wa wanafunzi bali hata wanaowafundisha. Kwa hiyo, ninaomba Serikali pamoja na uzito waliopata kifedha katika sekta hii ichukue mstari wa mbele kusaidia juhudi za Wananchi.

Mheshimiwa Spika, hotuba zote mbili ambazo naziangalia hapa za Waziri wa Mipango na Waziri wa Fedha zote zinaonyesha maeneo mbalimbali yenye udhaifu ambayo inabidi tuyafanyie kazi na mimi nitayataja machache kwa sababu kwa kweli mengi Waheshimiwa Wabunge wameyajadili hapa kwa kirefu sina haja ya kuyaongelea. Niangalie tu harakaharaka ukurasa wa 16 wa hotuba ya Waziri wa Mipango. Ukurasa huu unaelezea udhaifu mkubwa tulionao katika kuuza bidhaa zetu nje ya nchi na Waziri hapa anaeleza kabisa kwamba thamani ya bidhaa tunazoingiza toka nje ya nchi kwa kweli ukipiga hesabu za harakahara ni kama mara 15 ya thamani ya bidhaa zetu tunazouza nje ya nchi na hii ni hatari sana.

Mheshimiwa Waziri anasema: "Bila uzalishaji kwa viwango vinavyokidhi matakwa ya soko la dunia hatutaenda mbali".

Mheshimiwa Spika, nataka kusema tu kwamba nakubaliana na Mheshimiwa Waziri kwenye hili, moja ya vikwazo vikuu vinavyofanya Tanzania bidhaa zetu zisiuzike nje ni ufungashaji mbaya na mbovu wa bidhaa zetu. Kuna Balozi wetu mmoja alikuwa Falme za Kiarabu siwezi kumtaja jina lakini yeye mwenyewe atajua. Alitusimua wakati fulani tulipotembelea Dubai kwamba alihamasisha huku nyumbani upelekaji wa matunda Dubai na wananchi wetu waliitikia hilo na akawepo Airport kupokea mzigo wa kwanza ilibidi ajifiche kwa sababu Mananasi na Maembe yetu yalikuja kwenye mabox ya sabuni, mengine ya Hexa sitaki kutaja Hexa ni nini wote mnajua ni mabox ya nini yale. Kwa hiyo, ilikuwa ni hatari ikabidi ajifiche. Kwa hiyo, packaging ni tatizo kubwa sana tulilonalo.

Mheshimiwa Spika, nataka niipongeze Serikali siyo tu kwa kutambua kwamba hilo ni tatizo kubwa tulilonalo lakini vilevile naipongeza Serikali kwa kuiwezesha TBS, Shirika la Viwango Tanzania katika kujenga kitengo cha kisasa cha ufungashaji yaani *Packaging Technology Centre*. Kitengo hiki tumekitembelea sisi Kamati ya Uwekezaji

na Biashara kimekaribia kukamilika na kitakapokamilika kwanza kitaweka kiwango cha vifungashio na vilevile kitatoa mafunzo kwa wajasiriamali wa Tanzania hata viwanda kuhusu ufungashaji. (*Makofi*)

Ninachoomba kutoka Serikalini ni kwamba hili suala la hicho kituo kituo kuanza lisiwe ni la Wizara ya Viwanda na Biashara tu, Wizara ya Fedha, Mipango pia zote zishiriki kuhakikisha kwamba hiki kitengo kinaanza mara moja kwa sababu ugonjwa huu tumekuwa nao muda mrefu wa Watanzania kushindwa kuweka bidhaa zetu katika vifungashio vinavyotakiwa. Ukurasa wa 23 wa Hotuba ya Waziri wa Fedha unaongelea mpango maalum wa kuwawezesha wananchi kupata mikopo nafuu kupitia Benki ya *CRDB* na *NMB* na Waziri anaamini kuwa baada ya awamu ya kwanza kupita basi wananchi watakuwa wameelewa zaidi utaratibu wenyewe. Nataka tu kuliweka hili kwa usahihi.

Mheshimiwa Spika, wananchi hawana tatizo kabisa katika kuelewa masharti ya mikopo hii, tatizo lililopo ni ukiritimba uliopo kwenye mabenki yetu sisi wenyewe na vilevile kutokuelewa mazingira ya watu wetu wanaohitaji hiyo mikopo. Kwa sababu mimi nadhani mikopo hiyo toka mwanzo imekuwa inamfikiria mjasiriamali wa mjini na siyo wa wilayani. Mimi natoka Kyela, 90% ya wakazi wa Kyela ni wakulima, sasa anahitaji masharti tofauti. Mkulima wa Kyela wa mpunga akikopa fedha ataiwekeza mwezi Novemba, ataanza kuvuna mwezi Juni mwaka unaofuata. Kwa hiyo, anahitaji miezi tisa ndipo aanze kudaiwa ili kuilipa lakini anaambiwa mwezi mmoja. Sasa hii mikopo imemfikiria mjasiliamali wa kukaanga vitumbua na kadhalika yaani wa mijini tu lakini siyo mkulima. Mkulima wa *Cocoa* akikopa Januari anahitaji mwezi Juni aanze kuchuma. Sasa mdai mwezi Julai apewe miezi saba. Tukifikia hatua hiyo nina uhakika Serikali itakuwa imechangia sana katika kuendeleza hii mikopo na kuendeleza wajasiriamali nchini.

Mheshimiwa Spika, nimalizie haraka haraka ukurasa wa 32. Ukurasa wa 32 unaongelea umuhimu wa kuimarisha usimamizi wa Sheria ya Fedha za Kigeni ya Mwaka 1992 (*Foreign Exchange Act, 1992)* ili kusimamia zaidi maduka ya fedha za kigeni na vilevile taasisi au makampuni yanayotoa huduma kwa kudai dola*. (Makofi)*

Kusema kweli nia ya Mheshimiwa Waziri hapa ni nzuri sana lakini namwomba aelewe kwamba hii sheria anayoisema ya 1992 pamoja na *regulations* zilizotengenezwa mwaka 1999 vimepitwa na wakati, hata ukiimarisha usimamizi wake hutafanya chochote kwa sababu tulichokifanya katika kutunga sheria 1992 ni kuiondoa ile *Exchange Control Ordinance* ya nyuma ambayo ilikuwa imefunga milango tukaachia milango wazi chini ya hiyo sheria mpaka tukang'oa na bawaba, sasa utaimarisha kitu gani? Huimarishi chochote! Namwomba Mheshimiwa Waziri awaite wataalamu wake wakae chini na waipitie upya hii Sheria, haitufai kwa mazingira yaliyopo sasa hivi.

Mheshimiwa Spika, nimalizie kwa kitu cha haraka sana. Waheshimiwa Wabunge wenzangu wamesisitiza sana juu ya umuhimu wa viongozi wa Serikali kuwa makini na kuwa wakali katika utekelezaji wa bajeti hii. Mimi kwa kweli siwezi kuongeza zaidi. Juzi Mheshimiwa Aggrey Deaisile Joshua Mwanri alimaliza mjadala mzima kuhusu hili.

Lakini labda nisisitize kidogo tu kwamba hii ni bajeti ya kujifunga mkanda na kila mtu ajifunge mkand. Tumefanya nyongeza ndogo tu kwenye mafuta, hii kelele inayopigwa ya mafuta sijui kama watu wanaelewa, inapigwa kelele kwa sababu pengine tumewaachia mno wafanyabishara kufanya wanalolitaka. Nyongeza ndogo hii wao wataitafsiri kwa nyongeza mara 50 ya hapo, sasa huo ni usimamizi mbovu, tunaomba Serikali ilisimamie hili kwa makini.

Mheshimiwa Spika, hii ni bajeti ya kujifunga mkanda siyo kwa wananchi tu peke yao hata kwa wafanyabiashara wa mafuta nao wajifunge mkanda na sisi wenyewe viongozi humu tujifunge mkanda. Wenzangu wamesisitiza kwamba Wizara zijifunge mkanda, hapana! siyo Wizara tu hata sisi *life style* zetu zionyeshe tumejifunga mikanda tusionekane tumejifunga vibwewe. Kwa sababu tutatoka hapa kama viongozi tunaanza kuwa na tabia ya kuonyesha kwamba tunaelea katika pesa na uadilifu wa Mwalimu umepotea kabisa hapa, kwa sababu kwa kweli viongozi tumekuwa mabingwa kwenye matumizi ya ajabu ajabu *(conspicuous consumption)* na tukifanya hivyo wananchi hawatatuelewa na hawatatuamini tena.

Mheshimiwa Spika, nimalizie kwa kusema kwamba Waziri atueleze mapendekezo yetu ya kuitaka *TPDC* ijihusishe kwenye biashara ya mafuta yamefikia wapi? Kwa sababu *TPDC* kama Shirika la Umma litakatakata hii ngebe na kiburi cha hawa wenzetu wanaodhani kuwa wana nguvu kuliko Serikali katika kupanga bei ya mafuta, tunataka tulielewe hilo. (*Makofi*)

Loh! naogopa hiyo kengele lakini pengine niseme la mwisho sasa mpaka itakapopigia …..!

*(Hapa Kengele Ililia Kuashiria Muda wa Mzungumzaji Umekwisha)*

**MHE. DR. HARRISON GEORGE MWAKYEMBE:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Dr. Mwakyembe anafuatia sasa Mheshimiwa Benson M. Mpesya Mbunge wa Mbeya Mjini, halafu naomba Mheshimiwa Richard Said Nyaulawa na baada ya hapo Mheshimiwa Wilson Mutagaywa Masilingi wajiandae.

Mheshimiwa Benson Mwailugula Mpesya, karibu.

**MHE. BENSON M. MPESYA** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa naomba nikushukuru wewe kwa kunipa nafasi hii ili na mimi niweze kuchangia katika hotuba zote mbili ya Waziri wa Fedha, Mama Zakia Meghji pamoja na Waziri wa Mipango, Uchumi na Uwezeshaji Mheshimiwa Dr. Juma Ngasongwa.

Mheshimiwa Spika, nianze kwanza tu kwa kuwapa shime Mawaziri wetu wawili kwa maneno aliyoyazungumza aliyewahi kuwa Rais wa Marekani Theodory LuseBat.

Alisema hivi katika Kitabu chake, *The Art of Following the Plan Regardless the Critics.* Alisema, "*It is not the critic who counts not the man who points out how the strong man stambled or where the dual of deeds could have done than better. The credit belongs to the man who is actually in the arena"* . Mko kazini chapeni kazi.

Mheshimiwa Spika, nimeyasema maneno haya kuonyesha kwamba Mawaziri wote wawili hawa wamefanya kazi nzito ya kuiandaa bajeti. Kwa watu wanaojua taratibu za bajeti toka mwezi wa Novemba, 2006 *budget circle* ilishaanza. Leo ni takriban miezi sita mpaka wanaileta bajeti hii kama *final document*. Hatuwezi tukapuuza kabisa jitihada za kutoka mwezi Novemba, 2006 mpaka Mei, 2007 ikaonekana kwamba hakuna kazi iliyofanyika. Wamefanya kazi nzito, ninaamini walikuwa hawapati hata kidogo usingizi kwa sababu ya maandalizi hayo ya kuwaandalia Watanzania. Mimi ninaamini wana uchungu sana na Watanzania kwa sababu ni sehemu ya viongozi. Pili, naomba niseme tu kwamba mimi kwa mara ya kwanza katika historia ya utengenezaji wa bajeti wa Tanzania katika ule mchakato, kwa mara ya kwanza Waheshimiwa Wabunge, wamekuwa sehemu ya mchakato ule. Ninakumbuka ilikuwa ni mwezi Aprili, 2007, wakati sisi Waheshimiwa Wabunge wote kwa mara ya kwanza na tulishajaribu sana kusema namna sisi Waheshimiwa Wabunge tuwe sehemu ya mchakato wa bajeti ilishindakana. Lakini katika Serikali hii ya Awamu ya Nne na katika bajeti hii Waheshimiwa Wabunge tulipata fursa ya kuweza kuzungumza vipaumbele. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, na mimi ninaamini ni mwanzo mzuri. Ninaamini kabisa Mheshimiwa Dr. Juma Ngasongwa na Mheshimiwa Zakia Meghji, watazidi kutupa nafasi tena katika bajeti itayofuata ili tuweke nyama ya kutosha katika bajeti ya Serikali. Kwa hiyo, mtu mzima kwa kawaida si vyema ukayakana yale ambayo ulishiriki, haileti heshima hata kidogo.

Mheshimiwa Spika, Kiongozi kama Mbunge ulivyo unatakiwa uishi kwa maneno yako wewe mwenyewe uliyoyasema. Maneno yako na matendo yako viwiane. Tulishiriki, tulifanya kazi na tulielekeza ni kitu gani kifanyike. Naishukuru sana Serikali kwa sababu imekuwa *flexible* yale tuliyoyasema kwamba tunataka miundombinu, tunataka elimu, tunataka kilimo, tunataka afya vipewe vipaumbele imeyazingatia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kama ninakumbuka tulipozungumzia habari za miundombinu tulisema kwamba haya tunayoyasema ya miundombinu si ya kwetu ni ya wananchi. Sasa sijui ni mwananchi gani huyo tena atakayechukia tunaposema tumeamua kuanza na elimu na kutengeneza miundombinu ili tuboreshe hali yao ya maisha, basi atakuwa ni mwananchi wa ajabu sana. Mimi nafikiri tusipoteze rasilimali za nchi hii, kuzunguka bila mpango, tuzunguke tuwaambie wananchi wazalishe sana ili kuongeza pato la Taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nilipokuwa napitia bajeti zote mbili na kufanya uchambuzi niligundua kwamba eneo tunalolizungumzia la mafuta ni asilimia 6.83 ya bajeti nzima na ni eneo hilo tu la kiasi cha shilingi bilioni 239 hivi. Lakini kwa maana nyingine ni

kwamba asilimia 93.17 ya bajeti iko safi. Sasa mimi nilikuwa mwalimu, hapo ningeweza kutoa *A +*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa tunapozungumzia eneo la mafuta, mimi nafikiri hapa tuziachie kanuni za uchumi zifanyie kazi, si suala la kuzungumza tu, ni kanuni za uchumi. Tunachosema, Mwalimu katika kitabu chake cha *Man and Development* ukurasa wa 26 anaeleza kwamba maendeleo ni pamoja na kumjali mtu. Lakini tuangalie uchumi wa Afrika sasa hivi ni asilimia 2 tu ya mchango wake katika dunia nzima. Watu wanasema *the World is best off without Africa*. Wanasema dunia ingekuwa ni salama kama si Afrika, ni asilimia 2 ya mchango wetu.

Mheshimiwa Spika, lakini miongoni mwa nchi hizo katika Afrika ambazo zinafanya vizuri katika uchumi ni pamoja na Tanzania. Kukua kwa uchumi wetu pamoja na matatizo tunayoyapata si ongezeko dogo la kukua kwa pato la Taifa, ni kubwa. Lakini tatizo linakuja kwamba katika kanuni za uchumi, *economic growth* lazima iwe na *effects* kwenye *economic development*. Lakini kwa kiwango gani ni kwamba tunataka yale matunda ya kukua kwa pato la Taifa yashuke mpaka chini ya *trickle down to the mass*es, lakini yanapo-*trickle down to the masses* unaangalia huyo mtu utampa nini, unaimarisha barabara yake ili alipe kidogo.

Mheshimiwa Spika, mimi nataka kuwambieni kwamba tunapozungumza mafuta kwa kweli wakati mwingine hatujawa wakweli sana. Nataka niwambieni kabisa tunachozungumza ni nadharia. Mimi nitawapa mfano wa Mbeya. Mji wa Mbeya uko katikati, Tukuyu ni kilomita 75 kutoka Mbeya, Vawa ni kilomita 75 kutoka Mbeya, Chunya ni kilomita 75 kutoka Mbeya, wakoloni walijenga hizi kama *satellite cities,* lakini utakuta nauli ya kutoka Mbeya kwenda Tukuyu hazidi shilingi 1,500, kwa nini, barabara ni nzuri. Kwenda Mbozi Vawa nauli ni shilingi 1,500, kutoka Mbeya kwa nini, kwa sababu barabara ni nzuri. Lakini kutoka Mbeya kwenda Chunya nauli ni shilingi 4,500 kwa nini, kwa sababu barabara si nzuri. Sasa unaanzia wapi, mimi nafikiri unaanzia kuimarisha kwanza nyenzo za kumletea huyo maendeleo na nyenzo za kuleta maendeleo ni barabara, shule, afya, miundombinu, ukishamaliza hayo moja kwa moja *(automatically)* gharama zitajipunguza zenyewe kwa mujibu wa taratibu za uchumi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa mimi nafikiri ndugu zangu tunachotakiwa hapa tumepewa kama changamoto. Changamoto iliyopo mbele yetu tufanye nini kurekebisha uchumi wetu ili lile ongezeko la pato la Taifa liweze kumfikia mtu wa kawaida. Lakini katika hatua hii ya kukua kwa pato la Taifa tunachoweza kufanya ni kuimarisha nyenzo za maendeleo, halafu baada ya hapo zije zileta athari kwenye uchumi wa mtu mmoja mmoja. Hiyo ndiyo hali halisi ya uchumi. Kwa hiyo, nilikuwa naomba Watanzania wenzangu tuzunguke nchi nzima kuwaelimisha watu, kwanza kuhusu kilimo. Kilimo kina faida mbili. Kwanza, kilimo ni kama zana ya kudhibiti mfumko wa bei, lakini pili, kilimo ndicho kinachotusaidia katika kulikuza pato la Taifa.

Mheshimiwa Spika, nafikiri tuwe na *marshal plan* ya kuhakikisha kwamba tunaanzia kwenye kilimo. Wenzetu Wachina imewachukua miaka 25 mpaka 30 na

tunaposema kujifunga mikanda siyo mikanda kama hii tunayovaa, ni hali halisi. Tunazungumza hapa kifasihi. Wachina waliokuwa wanajenga reli tunawakumbuka walikuwa wanavaa suruali za aina moja na masharti ya aina mmoja na masharti mengine yalikuwa yamewekwa viraka walikuwa wanafunga mikanda kwa ajili ya kuhakikisha kwamba wanakuza uchumi wa Wachina. Leo hii hata nguo tunazovaa zinatoka China.

Mheshimiwa Spika, mimi nafikiri tuwe na *marshal plan* tuanzie na kilimo na tukiimarishe. Mwaka jana Serikali ilifanya mambo mazuri kuhusu pembejeo kwa Mikoa ya Nyanda za Juu Kusini, utaratibu tuliotumia ulikuwa ni kwenye Kata, lakini nataka niseme *impact* ya mbolea ile ilikuwa ni kubwa sana, wananchi walifarijika mno. Lakini tatizo linakuja mahitaji halisi ya Mkoa wa Mbeya ni tani 70,000, tulichopata ilikuwa ni tani 18,000, kwa hiyo, pengo lilikuwa dogo. Lakini pamoja na pengo hilo, dhamira na nia ya Chama cha Mapinduzi ilionekana dhahiri.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, mimi nataka niseme tujitahidi sana kuimarisha kilimo, tumetenga fedha kwenye kilimo kama kipaumbele, tunataka tuone programu ambazo baada ya miaka mitatu zitaleta matokeo. Isifike mahali miaka 10 inapita hatujaona hizo fedha zimefanya kazi gani katika kuongeza uzalishaji wa mazao ya biashara na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, nitatoa mfano wa Chuo cha Kilimo cha Uyole na Chuo cha Utafiti. Kabla halijafika pale Shirika la Kilimo Uyole, maisha ya wananchi wanaozunguka bonde la Uyole yalikuwa ya chini sana. Viazi mviringo walikuwa wanapata gunia tatu, lakini baada ya miaka mitatu ya utafiti na kufanya kazi na programu nzuri ekari moja sasa inampatia mkulima wa Mbeya gunia 70 mpaka 80 za viazi mviringo. Maisha yamebadilika, tunataka programu za namna hiyo.

Mheshimiwa Spika, ninamwomba sana Mheshimiwa Stephen Wasira wanapofanya utafiti, vilevile waangalie kwenye vijiji vyetu ni miradi ipi inaweza kusaidia. Lakini la umuhimu ambalo wenzangu wamelizungumzia katika nchi hii miaka ya 1977 na 78 tulikuwa na vijiji karibu 8,000 na tulikuwa na maafisa ugani 6,000 ule utaratibu umekwenda wapi sasa? Tumepeleke maafisa ugani katika kila kijiji wafanye kazi ya kuhamasisha kilimo ambacho kitatusaidia katika kukuza pato la taifa, lakini mwisho itatusaidia katika kuhakikisha kwamba kile tulichokipata kinakwenda chini kwa watu wetu ambao tuliwaomba kura na wametupa dhamana ya kusimama ndani ya jengo hili.

Mheshimiwa Spika, Mbeya tumedhamiria kuanzisha cha kiwanda cha mbolea na Mheshimiwa Rais Jakaya Mrisho Kikwete aliahidi kwamba atafufua viwanda Mbeya. Kwa ujasiri mkubwa sana mwenzangu Richard Nyaulawa naomba nimpongeze sana katika hili, tunashirikiana naye vizuri sana, lakini yeye yuko mstari mbele katika kuanzisha kiwanda hicho. Tumeona itakuwa ni usaliti tukisema Mheshimiwa Rais aliahidi kufufua viwanda. Halafu sisi Waheshimiwa Wabunge ambao ndiyo watendaji kazi wake tumekaa tu tumenyamaza, tunasema tunangojea ahadi ya Mheshimiwa Rais, haiwezekani! Tumeamua kuanzisha kiwanda cha mbolea Mbeya kama sehemu ya utekelezaji wa ahadi ya Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Spika, sisi tayari tumekwishakusanya karibu shilingi milioni 38 kwa watu maskini, si kitu kidogo hicho. Mtaji wa awali unaweza ukafika kama shilingi bilioni 6, tunatimiza ahadi ya Chama cha Mapinduzi na tunatimizi ahadi ya Mheshimiwa Rais wetu aliyetupatia heshima hii.

Nilikuwa naiomba Serikali iingilie kati juu ya kiwanda cha mbolea cha Mbeya kutusaidia sisi, kwa kufanya hivyo watakuwa wameisaidia Rukwa, Iringa na Ruvuma. *(Makofi)*

Mwisho, Mheshimiwa Spika, naomba niseme sitaki kengele inigongee kwa sababu sisi tuna maadili si vizuri tukakiuka. Ninaomba niwatakie kila kheri na mema nyote Mawaziri wote wawili kwa bajeti hii ambayo imewachukua miezi sita.

Mheshimiwa Spika, ninaunga mkono hoja hii kwa sababu ni bajeti nzuri. *(Makofi)*

**MHE. RICHARD S. NYAULAWA:** Mheshimiwa Spika, ahsante na mimi kunipa nafasi hii niweze kuchangia katika hoja hizi mbili ambazo zipo mbele yetu.

Mheshimiwa Spika, la kwanza ningependa kuwapongeza Mawaziri wote wawili kwa kazi ambayo wameweza kuifanya ya kutayarisha bajeti, lakini vilevile kuiwasilisha vizuri bajeti pamoja na mpango wa mwaka 2007/2008.

Mheshimiwa Spika, kabla sijaanza kuchangia kuhusu bajeti hii ningependa kwa niaba ya wananchi wa Mbeya Vijijini nitoe pongezi zangu kubwa sana kwa timu ya Taifa kwa ushindi mkubwa sana walioweza kuupata. Wananchi wote wa Mbeya wamefarijika na wengi waliweza kunitumia ujumbe wa maandishi kwenye simu kwa kazi nzuri ambayo ilikuwa imefanyika hapa Bungeni katika kuipongeza Taifa *Stars*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini vilevile ningependa kutambua mchango mkubwa wa Waheshimiwa Wabunge wenzangu ambao wamechangia hoja hizi. Mimi natumaini ni mtu kama wa 73 katika kuchangia. Kwa maana hiyo ni kwamba mengi yanaweza kuwa yamezungumzwa, lakini hata hivyo na mimi nitajaribu kuongezea pale ambapo panastahili.

Mheshimiwa Spika, marehemu Baba wa Taifa mwaka 1965 alisema: "Maendeleo ya Tanzania yataletwa na Watanzania wenyewe kwa kujitegemea na alisema hatuwezi kuendelea kwa kutegemea misaada kutoka nchi za nje." Sasa ni miaka 42 toka usemi huo wa Marehemu Baba wa Taifa, lakini bado inaelekea kuna watu wanakuwa na kigugumizi katika dhana ya kujitegemea. Dhana ya kujitegemea maana yake ni lazima tuwe na uwezo wa kukusanya mapato ya kutosha ndani ya nchi ili tuweze kupata maendeleo ya kutosha.

Mheshimiwa Spika, bajeti ya safari hii imelenga katika kutimiza hoja hiyo kwa maana ya kwamba makusanyo yataweza kuongezeka kwa asilimia 23. Kwa maana hiyo,

ina maana kwamba sasa tumeanza mchakato wa kujenga misingi ya kuweza kujitegemea. Hilo ni la msingi sana kama tunataka kujitawala na kujiendeleza sisi wenyewe ni lazima tuweke misingi iliyokuwa sahihi. Mimi ningependa sana kuwapongeza sana Waheshimiwa Mawaziri kwa kazi hiyo ambayo wameweza kuifanyia vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, bajeti hii ni nzuri na mimi ninaiunga mkono kwa asilimia mia moja. Naiunga mkono bajeti hii kwa sababu tano zifuatazo. Moja, inatoa kipaumbele katika sekta ambazo zinajenga misingi ya maendeleo. Katika utafiti uliofanywa na katika uzoefu ulioonekana duniani kote nchi zote za Korea na za Asia zimepiga hatua kubwa katika maendeleo kwa sababu zilikuwa zimeweka misingi mizuri katika elimu, ziliweka misingi mizuri katika miundombinu, ziliweka misingi mizuri katika kilimo, katika afya pamoja na mambo ya umeme.

Mheshimiwa Spika, na mimi nafikiri kwamba hiki kipaumbele kinatuwekea misingi mizuri ya kuwa na maendeleo siyo leo tu, lakini hata kwa siku zijazo. Katika hilo naunga mkono bajeti hii. Lakini pili, bajeti hii imezingatia uwezo wetu, natumaini wenzangu wameishaeleza kwamba kulikuwa na mahitaji ya shilingi trilioni 12, lakini fedha tulizokuwa nazo ni trilioni 6, imezingatia kile ambacho tunacho. La tatu, inatekeleza Ilani ya Chama cha Mapinduzi.

Mheshimiwa Spika, katika Ilani ya Chama cha Mapinduzi kulikuwa na kero za kila aina na bajeti hii inajaribu kupunguza kero za wananchi na inagusa wananchi wengi na inalenga katika kuboresha maisha ya mtanzania; na inawezakana yasionekane leo, lakini kwa sababu tunaweka misingi mizuri mwaka kesho na mwaka kesho kutwa na katika miaka ijayo, hayo maisha bora kwa kila mtanzania yataonekana. Lakini ni lazima tuwe na mahali pa kuanzia. Kwa misingi hiyo naunga mkono bajeti hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nne, naunga mkono bajeti hii kwa sababu inajenga misingi ya kujitegemea na mwisho kabisa ni kwa sababu sisi Wabunge tulikuwa tumeshirikishwa katika kueleza ni kitu gani kipewe kipaumbele ili tuweze kuwa na bajeti ambayo itakuwa inafanya kazi vizuri. Katika misingi hiyo mitano naunga mkono bajeti hii kwa asilimia mia moja. Kila mmoja wetu anataka maendeleo katika maeneo ya elimu na kazi kubwa imefanyika katika maeneo hayo na kazi iliyopo ni kuboresha mazingira mazuri, kujenga maabara, kuwa na mkataba na kujenga nyumba za walimu katika shule zetu za Sekondari. Hiyo inahitaji fedha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kila mtu anahitaji miundombinu ili tuweze kuwasiliana na tuweze kusafirisha mazao yetu. Katika misingi hiyo na mimi ningetaka kukumbusha kwamba barabara zetu za Wilaya ya Mbeya Vijijini ya Isonje hadi Makete, Mbalizi kwenda Ileje, Mbalizi kwenda Mkwajuni ambazo ni ahadi tuliyopewa, natumaini zinaweza kutengenezwa kwa sababu msingi mkubwa wa kutafuta fedha ili kuweza kutekeleza hayo ndiyo hayo ambayo yapo katika bajeti hii.

Mheshimiwa Spika, kiwanja cha ndege cha Songwe vilevile kiko katika bajeti hii, tunahitaji kuwa na fedha ili tuweze kuwa na miundombinu ya kuweza kusafirisha mazao yetu. Bajeti hii inazungumzia kuhusu suala la afya na fedha nyingi zimetengwa katika

eneo hilo. Vituo vya Afya vitajengwa, lakini kazi kubwa itakuwa ni kuhakikisha kwamba tunakuwa na wauguzi wa kutosha kwa sababu hilo ni tatizo kubwa kabisa. Katika maeneo yangu Mbeya Vijijini kuna zahanati zaidi ya 11 ambazo zimejengwa na zimekamilika na zina nyumba za wauguzi, lakini kwa bahati mbaya hazina wauguzi, tunahitaji kutoa kipaumbele katika bajeti ya afya ili tuweze kuwa na wauguzi wa kutosha. Kkatika suala la kilimo natumaini tunasema kilimo ndiyo uti wa mgongo wa maendeleo ya Tanzania, lakini kwa bahati mbaya hatuweka nguvu ya kutosha katika misingi ya kuhakikisha kwamba kilimo chetu kinaendelea sawa sawa. Pamoja na kutambua hayo Tanzania hatuna viwanda vya mbolea, Tanzania hatuna viwanda vya zana za kilimo, Tanzania hatuna viwanda kwa ajili ya kutengeneza madawa ya kilimo. Sasa hata kama tukisema kwamba kilimo ndiyo msingi wa maendeleo tusipokuwa na nyenzo hizo msingi huo uko wapi?

Mheshimiwa Spika, bajeti ya asilimia 6.2 kwenye kilimo ni nzuri, lakini ingeweza ikaongezeka ikafika asilimia 10 kama ambavyo tulikuwa tumeahidi kwa wenzetu katika nchi za *SADC*. Nina imani kuwa tukiweza kufanya hivyo na kutoa kipaumbele katika maeneo hayo, Kilimo kitaongezeka kwa kiasi kikubwa na mchango wa kilimo katika bajeti zetu utakuwa ni mkubwa na mchango wa kilimo katika pato la Taifa utakuwa ni mkubwa sana zaidi ya asilimia 60; na vilevile fedha ambazo zinaweza kupatikana za kigeni kwa kuuza mazao mbalimbali ya kilimo utakuwa ni mkubwa zaidi kuliko hiyo asilimia 45 ambayo inapatikana kwa hivi sasa.

Mheshimiwa Spika, suala la umeme ni zito na mimi nataka kuhakikisha kwamba bajeti hii kwa utaratibu ambao umewekwa inaweza kujenga misingi ya kuhakikisha kwamba hata zile ahadi ambazo tulikuwa tumeziweka huko nyuma zinaweza kutekelezwa.

Mheshimiwa Spika, bajeti hii vilevile inajaribu kusaidia wafanyakazi waweze kupata mishahara mizuri. Maendeleo yoyote yanahitaji fedha. Hayo maeneo ambayo nimeyasema ni ya msingi yanahitaji fedha, hakuna maendeleo yanayoweza kupatikana bila kuwa na uchungu wa aina moja au nyingine, mimi sijawahi kupata maendeleo ya namna hiyo. Kwa hiyo, ni lazima tujifunge mikanda. Hatuwezi kutegemea kupata maendeleo kutoka watu wengine.

Kwa maana hiyo ni kwamba maendeleo kama tunayahitaji ni lazima tujenge misingi imara sisi wenyewe. Pamoja na michango mizuri ambayo imetoka kwa Waheshimiwa Wabunge wenzangu, lakini nilikuwa nafikiria kwamba ili tuweze kupata fedha za kutosha kwa ajili ya maendeleo kunahitajika mambo sita. Jambo la kwanza, ni kukusanya fedha kwa ufanisi kutoka katika maeneo ambayo yameainishwa na Mawaziri wote wawili. Katika hilo, natumaini ningeweza kusema tu hili suala la mafuta ya taa lingeweza kuangaliwa vizuri.

Jambo la pili, ni kupanua wigo wa kukusanya zaidi. Natumaini tunaweza kupanua wigo kwenye eneo la madini, kwani tuna dhahabu nyingi ya kutosha, basi hata bajeti yetu inuke nuke dhahabu kidogo. Tungeweza kukusanya kodi kwenye bidhaa

mbalimbali za misitu, bidhaa za samaki. Lakini vilevile tungeweza kuongeza ushuru kwenye mambo ya forodha. Kwenye maziwa ya kunywa, tunanunua maziwa mengi kutoka nchi za nje na sisi kama Tanzania tuna ng'ombe zaidi ya milioni 17, tunazalisha maziwa ya kutosha. Tungeweza kufanya kazi kubwa ya kuhakikisha kwamba ushuru mzuri unapatikana kwa kuweza kutoza kiwango kikubwa cha ushuru huo ili angalau maziwa ya Tanzania yaweze kutumika vizuri zaidi kuliko ambavyo inafanyika hivi sasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, matunda mengi yanayotumika nchini hapa hasa sehemu za mijini yanatoka Afrika Kusini na tuna uwezo wa kuweza kuzalisha matunda yetu sisi wenyewe. Nina imani kama tukiweza kuongeza kodi ili tuweze kupunguza kiwango cha matunda hayo kutoka Afrika Kusini basi bila shaka matunda ya nchi yetu yanaweza kutumika vizuri zaidi. Tunahitaji kuongeza ufanisi katika ukusanyaji wa kodi, *fast track* siyo suala geni katika dunia. *Fast tracking* katika mambo ya ndani ni kitu cha kawaida limefanyika kwa muda mrefu. Mimi ningependa kutoa pongezi kwa watu wa *TRA* kwa kazi nzuri ambayo wameifanya katika miaka mitano iliyopita kwa kuweza kuwatambua walipa kodi wakubwa 80 katika nchi hii. Wamewafanyia mafunzo kwa miaka yote hiyo na wamewafuatilia kwa kiwango kikubwa sana. Sasa hivi wamefikia mahali ambapo asilimia 60 ya pato ambalo tunalizungumzia linatoka kwa hao watu 80.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, wanachostahili kupata ni kuhakikisha kwamba wanawapa uwezo wa kutoa mizigo yao bandarini kwa ufanisi mkubwa zaidi ili angalau biashara zao za kuzalisha bidhaa zisiweze kukwama kwa urahisi. Kwa kufanya namna hiyo tutakuwa tunawawezesha zaidi katika kuchangia pato letu la Taifa. Kinachohitajika hapa ni kuweka rekodi vizuri, kuwafuatilia vizuri na kufanya kazi hiyo kwa ufanisi mzuri zaidi. Hii kazi siyo mpya, imekuwa ikitendeka sehemu yoyote duniani. Sisi tumechelewa, kwa kweli tunachohitaji hapa ni kuwaruhusu wenzetu ili waweze kufanya kazi hiyo kwa ufanisi mzuri zaidi.

Mheshimiwa Spika, kukopa ni suala la kawaida kama tunataka maendeleo, tunahitaji kukopa, familia inahitaji kukopa kama inataka kujenga nyumba ya bati, kampuni inahitaji kukopa, nchi inahitaji kukopa, hata nchi za wenzetu zinakopa. Tusiogope kukopa kama tunataka maendeleo ni lazima tukope. Fedha tunazozikopa ziende katika mambo ya maendeleo, tuziwekeze kwenye maendeleo. Tusiogope kukopa hata siku moja. Hakuna hata mtu mmoja au hata nchi moja ambayo imeendelea bila kukopa. Kwa hiyo, hilo ni eneo ambalo tunastahili kulifanyia kazi vizuri. Lakini vilevile tuhakikishe kwamba wenzetu sekta binafsi wanapewa nafasi nzuri kufuatana na mchango wa *PPP*. Tumekuwa tukizungumza kwa muda mrefu, lakini hatujawatumia vizuri zaidi. Sekta binafsi inaweza kuwekeza vizuri zaidi katika mambo ya barabara, katika mambo ya viwanja vya ndege, katika bandari na katika mambo mbalimbali, tuwatumie vizuri ili waweze kutoa mchango mzuri katika suala zima la maendeleo.

Mheshimiwa Spika, lingine ambalo nataka kulichangia katika hilo pamoja na kwamba tunazungumzia kuhusu vyanzo vya fedha, lakini tunahitaji kuwa na matumizi mazuri ya fedha tunazokusanya. Matumizi yetu si mazuri sana katika sehemu mbalimbali kutokana na taarifa ambazo tumeweza kuzikusanya. Nguzo nzuri kabisa ya

kuweza kuhakikisha kwamba tunaweza kuwa na mafanikio ni pale ambapo fedha zetu tunazozikusanya zinatumika vizuri. Kwa hiyo, tunahitaji kuwa na utaratibu mzuri wa kusimamia vema fedha zinazokusanywa. Lakini vilevile tuwe na uangalizi wa kutosha; na wale wachache ambao wanaichafua Serikali kwa kuwa na matumizi mabaya wachukuliwe hatua kali, tusiwaone huruma. Hao ndio maadui wakubwa wa Taifa letu. Sisi tunapozungumzia kuhusu kufunga mikanda wao ndio wanafungua mikanda, itakuwa haiwezekani. Kwa hiyo, hao ningeomba wachukuliwe hatua kali kabisa ya kutosha. Vilevile ninataka niwatetee madiwani wenzangu, wanafanya kazi nzuri sana huko pamoja na watendaji wa kata. Nilikuwa nafikiria kwamba wanahitaji kupewa nafasi ya kuwa na mishahara mizuri. *(Makofi)*

Mwisho, Mheshimiwa Spika, tumeweza kujenga Vyuo Vikuu vingi sana, lakini sina uhakika kama tuna walimu wa kutosha. Tunaweza kuwa na Vyuo Vikuu ambavyo havina walimu, inawezekana kwamba ubora wa elimu na wanafunzi wanaohitimu katika Vyuo hivyo wasiwe wazuri sana. Nilikuwa natoa rai kama ikiwezekana Vyuo Vikuu vipewe kipaumbele. Tulikuwa na Vyuo Vikuu viwili miaka 15 iliyopita, lakini leo hii katika nchi yetu tunavyo zaidi ya 30. Serikali imefanya kazi kubwa sana kuweza kuleta mabadiliko hapa nchini. Serikali inahitaji pongezi.

Mheshimiwa Spika, mimi naunga mkono hoja hii iliyopo mbele yetu kwa asilimia mia moja. Ahsante, nashukuru sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ni zamu sasa ya Mheshimiwa Wilson Masilingi atafuatiwa kama nilivyosema na Mheshimiwa Profesa Idris Mtulia na baada ya hapo ajiandae Mheshimiwa Lucas Selelii. Wanaofuata wengine wote siwaoni ndani ya ukumbi nao ni Mheshimiwa Lucy Mayenga, Mheshimiwa Dr. Lucy Nkya, Mheshimiwa Paul Kimiti, kama wapo katika maeneo ya Bunge basi zamu zao zinakaribia.

**MHE. WILSON M. MASILINGI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipatia nafasi hii na mimi nishiriki katika mjadala wa mapendekezo ya bajeti ya Bunge hili ili tuweze kuidhinisha na hatimaye kuanza mwaka mpya wa fedha wa utekelezaji wa Mipango wa Maendeleo.

Kabla sijaendelea napenda niungane na wachangiaji wenzangu katika kutoa salamu za rambirambi kwa ndugu za marehemu wote waliopata misiba kutokana na ajali za barabarani na majini kwa kipindi kilichopita tukiwakumbuka waliokufa katika barabara ya Singida na Ziwa Victoria.

Baada ya pole hizo napenda nimpongeze Mheshimiwa Waziri wa Mipango, Uchumi na Uwezeshaji na Waziri wa Fedha na Serikali nzima kwa kazi nzuri wanayoifanya na waliyoifanya katika kipindi cha mwaka wa fedha kilichopita katika kutekeleza maazimio tuliyoyapitisha hapa yaliyopangwa na kutekeleza miradi ya maendeleo ya sekta zinazowahusu wananchi wetu. Katika mchango wangu nakusudia kuzungumzia mambo yafuatayo. Kwanza, hali ya maisha ya wananchi wa vijijini na mijini na uhusiano wake na mapendekezo ya bajeti. Pili, hoja ya kupeleka madaraka kwa

wananchi kwa utaratibu uliopendekezwa na Mheshimiwa Waziri wa Fedha wa kupeleka shilingi bilioni 286 kwenye Halmashauri zetu.

Mheshimiwa Spika, nitazungumzia mifugo nikikazia kilimo na uvuvi wa samaki, jinsi ambavyo vinaweza vikachangia kuboresha mapato yetu haraka sana katika kipindi hiki kigumu. Tatu, nitazungumzia mikopo ya vijana wetu ambao wako masomoni, kwenye elimu ya juu nikisisitiza umuhimu wa kuwapendelea Madaktari na Wauguzi kwa pamoja bila ya kuwatenganisha maana yake uzoefu tulionao upendeleo ulikuwa kwa Madaktari tukawasahau Wauguzi.

Nne, nitaongelea jinsi bajeti yetu inavyozungumzia walemavu, sisemi kwamba ilipaswa kutajwa humu na mimi nitafuatilia hotuba zote za Waheshimiwa Mawaziri watakaofuatia, ni kwa jinsi gani wanatafsiri bajeti hii katika mikakati yao katika sekta. Naahidi kuchangia kila Wizara ama kwa kuzungumza au kwa kuandika nikitafuta walemavu wameandaliwaje na wazee. Tano, nitaangalia miradi ambayo inaendelea, kuisisitizia Serikali sio iangalie kukamilisha barabara kuu za lami na nyingine za vijijini bali na miradi mizito na mizuri inayonivutia, na nitatolea mfano wa jengo la Uwanja wa Michezo *(National Stadium*) na jengo la Wizara ya Mambo ya Ndani linalojengwa karibu na *Movenpick,* baada ya hapo nitakuwa nimemaliza, sasa nikigongewa kengele hayo yamesikika.

Mheshimiwa Spika, nikianza baada ya shukrani kwa Serikali nimevutiwa sana na uamuzi wa Serikali wa makusudi wa kuamua kusukuma wananchi kujenga Shule za Msingi na Sekondari kila Kata, zahanati kila kijiji, kituo cha afya kila Kata. Watu wengine wanajiuliza hivi Mheshimiwa Rais atatoa wapi fedha au Serikali itatoa wapi fedha, haya ni mambo muhimu sana? Mtoto akiugua ukasema twende hospitali, hawezi kukuuliza baba una hela, atavaa, mnakimbia hospitali, huna hela, una hela huduma ya afya anataka. Sasa na Rais wa nchi hii vilevile ni kama baba. Watanzania wanataka elimu, madawa, sasa tuhangaike jamii nzima na wanaotutakia amani Mataifa ya nje wanaojiita marafiki zetu waje watuone tulie nao. Baada ya hapo naanza na hali ya wananchi.

Mimi ninaongoza ujumbe wa Muleba Kusini ndani ya ukumbi huu, mimi ndio msemaji. Wamenituma nisema haya yafuatayo kuhusu hali ya wananchi kwenye jimbo la Muleba Kusini, ni mbaya kimapato. Huo ndio ukweli. Hali ni ngumu. Sasa hawailaumu Serikali, ndiyo imesababisha hali kuwa ngumu, wanaitazama Serikali tufanye nini? Hata mijini hali ni mbaya kwa sababu mjini mimi naishi, hali ya kipato cha wananchi ni mbaya na waliposikia hotuba ya Mipango na Bajeti, maskini sasa mawazo yao yote yakahamia kwenye bajeti wakasema sasa inatumaliza. Kumbe maskini bajeti inakusudia kuwasaidia. Maana yake mapendekezo ya bajeti hayalengi kuwamaliza wanyonge hao ni kuwaondolea umaskini wa kipato ndio MKUKUTA. Sasa mnafanya nini? Mimi nataka kuipa moyo Serikali kwamba kutawala nchi sio mchezo na ukishapewa lazima utawale, mambo yawe magumu unasonga mbele baada ya miaka 5 unatoa maelezo. Sasa hivi kama Wabunge wa Chama cha Mapinduzi tunashirikiana katika kutoa ushauri kwa wale mlio mstari wa mbele na sisi tulio mstari wa nyuma, hatuko nje ya uwanja, sisi hatutazami. Unapiga kule, kama hamuingizi magoli sisi

tunazuia *full time* huku jasho litatutoka. Maana yake sisi huku kazi yetu ni kuzuia magoli yasiingie lakini na nyinyi mfunge ndiyo maana tutaweza kuendelea mpaka Ghana ya maendeleo hiyo.

Wananchi wanajiuliza wanasema hivi, "hivi kuna kila sababu za msingi hapo mje mnisaidie kwa sababu wanaponiuliza najaribu kwa kadri ya uwezo wangu kutetea sera hizi nzuri". Kwa mfano, jinsi tunavyoendesha mambo yetu kwa kusimamia utekelezaji wa bajeti hasa tukitambua kwamba tumeamua kuwa na sera nzuri ya soko huru, hivi tunalisimamia kwa mujibu wa taratibu na viwango vya Kimataifa? Mbona soko huru limewasaidia wenzetu sisi huku linataka kuleta kasheshe ya kukataliwa, mimi najua upungufu upo kwenye usimamizi (*Regulatory Mechanism*). Tumejenga vyombo vingi vya udhibiti, hawadhibiti, hiyo nitakuja kuwapa mfano, je, Serikali yetu kujitoa kwenye biashara kabisa kabisa ni uamuzi wa kuendeleza au tufanye tathmini tujitazame ni maeneo gani Serikali tuingilie kati kuokoa maskini? Hiyo ni kutathmini, mimi siilaumu Serikali ni yetu, wote, maana yake nyinyi mmepokea mnaendeleza tusaidiane, wataalamu wananiangalia kwenye kioo mtazame hivi tuendelee hivi hivi? Tuseme ni soko huru kila kitu kitajiweka sawa halafu wananchi waendelee kulia na sisi tunawawakilisha. Mimi naamini kuna kila sababu ya kuiangalia upya na nitawapa mfano wa Muleba.

Mheshimiwa Spika, bei ya sukari Muleba ni shilingi 1,200 kwa kilo. Kiwanda cha sukari kiko Kagera hatuna nafuu yoyote ya kuwa na Kiwanda Kagera kwa bei ya sukari, yanahitajika maelezo sijui ya kisera, sijui ya *regulation*, sijui nini tutafakari. Bei ya dizeli kwa sasa kwa bei ya jana shilingi 1,570 kwa lita. Sisi huku tunazungumzia kuongeza shilingi 100 tu ziwe shilingi 200 jambo ambalo naliunga mkono. Utapataje fedha za kutengenezea barabara bila kutafuta fedha za barabara? Lakini hivi kweli ngoja niwaambie petroli lita moja shilingi 1,600, nazungumzia bei ya shamba jimboni Muleba Kusini. Mafuta ya taa shilingi 1,200, saruji mfuko mmoja shilingi 18,500. Saruji kutoka Uganda shilingi 17,800, sabuni mche mmoja shilingi 700/-, sasa Muleba Kusini ni sehemu ya Tanzania na wanajua bei za Dar es Salaam na wanajua bei za Muleba na mikoa mingine ya pembezoni. Tuseme ndivyo mambo yanavyokwenda baada ya bajeti hii ya Julai twende shilingi 2,000 lita moja ya mafuta tunasema tunajenga barabara ambayo naipenda sana kwa sababu Serikali imetoa mchango mkubwa wa kutuunganisha sisi na Dar es Salaam na Uganda. Heko Serikali nawapongeza sana na makandarasi wako wanachemka jimboni. (*Makofi)*

Mimi naishauri Serikali isimamie biashara ya mafuta. Hatuwezi kuacha hawa wafanyabiashara wa mafuta wanafanya kiholela. Serikali muingilie kati, hii ndiyo vita, ndiyo itatunusuru kujibu hoja za wananchi kwamba kupanda kwa mafuta ya taa, dizeli na petroli kutaathiri uchumi, hii ni kweli. Lazima tukubali uchumi utaathirika sana kwa sababu wafanyabiashara watapandisha kila kitu. Mfanyabiashara wa nyanya atapandisha atasema petroli, kila mtu petroli, petroli, tunahujumu! Wapi maskini, tuwasimamie? Tunajua tuna wasomi hapa na mimi mkikosa fursa mnaweza ukanituma sio niwe Waziri hapana, nifuatane na hawa wanaokwenda kununua mafuta, hivi bei ya dunia ya mafuta tunaijua? Sisi tunaunganishwa Dar es Salaam na mafuta yanakotoka kwa meli, tujue mafuta hayo shilingi ngapi au dola ngapi za Marekani.

*Transport cost* na *insurance* kiasi gani mpaka Kurasini pale halafu tujue faida wanayotengeneza wamepata kiasi gani na ushuru wetu tumekusanya kiasi gani tuwabakizie kidogo na tuchukue kidogo. Hii bei ya mafuta inaweza ikashuka sana mimi nina uhakika. Wanapanga bei ya mafuta ya juu sana tena inaweza ikashuka ukakuta sisi tunachangamka mpaka wananchi wanatushangaa mbona bei ya mafuta imeteremka.

Mheshimiwa Spika, sasa niongelee kuhusu kupeleka madaraka kwa wananchi. Wananchi vijijini Katiba inasema tupeleke madaraka kwa wananchi sio kwenye Watendaji wa Halmashauri na hili lisiposimamiwa vizuri chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu nilitaka kuchangia katika Ofisi ya Waziri Mkuu lakini nikasema tuwahi muda upo nitaliendeleza hili. Kuna wapotoshaji hawafuati Katiba na Sheria, wanachukua visingizio vya kuchangia maendeleo wanachangisha watu, funga kamba, piga fimbo kwa kisingizio cha msako wa michango. Hii haikubaliki na ni kinyume cha Katiba na Sheria. Kamati ya Maendeleo ya Kata haina uwezo wa kupanga kiwango cha michango. Wananchi katika mikutano yao mikuu ya kijiji ndiyo wenye uwezo wa kisheria wa kuchagua ni michango gani wachange. Kamati ya Maendeleo ni kutoa mapendekezo kwenye Halmashauri ya Wilaya au Serikali za Vijiji, mikutano mikuu na Muleba nimekuta Mtendaji wa Kijiji anaongoza kikao badala ya Diwani kutokuwepo anaweka shilingi 10,000 kwa kila kichwa. Nikamwambia hiyo ni batili kwanza.

Mheshimiwa Spika, sheria inasema Diwani asipokuwepo Mwenyekiti wa Kijiji aliopo pale ndiye anaongoza Kamati ya Maendeleo ya Kata, tufuate sheria! Mheshimiwa Rais wakati anazindua Bunge letu anasema "Nitaongoza nchi kwa kufuata utawala bora, kuzingatia sheria na kuheshimu umma" na watendaji wasio wabunifu wanaojali maguvu kinyume cha Katiba hawana nafasi. Katiba inasema kuendesha kidemokrasia, kuhamasisha maendeleo si mitulinga, wasipotoshe sera nzuri ya Rais ya kuchangia maendeleo wakaanza kufunga watu kamba, mimi sitakubali nitapambana nao. Wengine wanaweza kusema napinga michango, mimi sipingi michango, nitakabiliana nao na Mheshimiwa Waziri Mkuu utanisaidia najua hupendi haya mambo machafu.

Mheshimiwa Spika, nimalizie na jengo la Wizara ya Mambo ya Ndani na Uwanja wa Taifa. Jamani tafuteni fedha awamu ya pili ya Uwanja wa Taifa imalizike. Wametueleza tulipotembelea uwanja kwamba isipoisha michezo mingine haitafanyika na manufaa ya Uwanja wa Taifa fedha hazitakuwepo. Jengo la Mambo ya Ndani toeni fedha tena ghorofa sio ziwe 8 ghorofa 16. Eneo hilo lote linahitaji wapangaji, mimi natafuta chumba cha Ofisi, Mafuta *House* nimekosa imeshajaa, *PPF, IPS* imejaa, eneo lote limejaa. Jengo, Serikali inajenga inakwenda linasuasua fedha imetusubiri pale. Sasa malizeni miradi ya barabara, mashule, majengo kama ya Mambo ya Ndani yaishe haraka haraka, pangisheni wafanyabiashara, Waziri wa Mambo ya Ndani anakaa chini huko. Uwanja wa Taifa ongezeni mabilioni mtazalisha mabilioni kila mechi ni miradi ya kuleta fedha.

Mheshimiwa Spika, nimalizie na mifugo. Lazima mifugo tuipe uzito sio wa kawaida na samaki kwa sababu ukianza kuuza kesho ndio unapata fedha. Kulima nawaambia mnatuambia tuchangamke kilimo, nani atalima jimboni kwangu, hawana uwezo wa kulima kwa jembe. Tutawadanganya tunakwenda kulima, mwaka jana,

mwaka juzi tulishindwa kwa sababu gani, hatujawezeshwa. Sisi tunahitaji kilimo cha umwagiliaji, mashamba yetu madogo, migomba, tuwe na mabomba ya umwagiliaji tuwaletee maboga, karanga tunaweza kulima mara tatu kwa mwaka, maharage hivyo hivyo. Tusaidieni Muleba Kusini hapo ndiyo utachangisha watu na utakuta wenyewe wanajitolea kuchanga. Kwa sababu mpaka sasa hivi wanachanga, lakini wakishindwa kuchanga msiseme wamekataa maendeleo, hawana fedha, hali mbaya ya uchumi.

Walemavu lazima tuwaangalie sekta zote kwa sababu mlemavu mmoja alipangiwa mtihani, amelemaa mikono muda ule ule wa kufanya mtihani na watu wenye mikono safi kama yangu, Baraza la Mitihani muwaelekeze hawa watu hii haihitaji sheria ya Bunge. Mtu hana mikono hafanyi mtihani wa Kidato cha Nne sawa sawa na mwenye mikono si unamwongezea saa mbili, tatu. Huo ndio upungufu unaojitokeza katika kuangalia sekta hizi, sasa sijui nimemaliza lakini nadhani mmenipata.

Mheshimiwa Spika, napenda kumalizia kwa kusema hotuba ya Rais ya kuzindua Bunge, tarehe 30 Desemba, 2005 zitolewe nakala zingine zaidi kila kijiji kipate na Katiba ya Nchi wapate na Sheria ya Halmashauri ya mwaka 1982, tuendeshe nchi kwa Utawala Bora kwa kuzingatia sheria. Ahsante Mheshimiwa Spika.

**MHE. PROF. IDRIS A. MTULIA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi na mimi nichangie hotuba hizi mbili. Awali ya yote naomba kuwapongeza Mawaziri wa Fedha na Mawaziri wa Mipango kwa hotuba zao nzuri. Kwa kweli inalenga kujitegemea na utawala ni kujitegemea na yeyote anayekataa hili nadhani itabidi arudi tena ajue nini maana ya kujitawala.

Mheshimiwa Spika, kazi iliyofanywa ni kubwa. Nilitaka niseme kwanza niunge mkono asilimia mia moja labda nitasahau huko mbele. Ukichukua mwendo na utekelezaji wa shughuli za Serikali, chukua mwaka mmoja tu, katika elimu. Tumepata *enrolment* ya vijana wa *Primary School* imepanda mpaka kufikia asilimia 96.4. Ukienda Sekondari mwaka mmoja tu tumejenga Sekondari 1,084 haya ni mapinduzi tuyapigie makofi. (*Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ulisema asubuhi hapa wanawake wanaweza. Hii ni alama kweli kweli Waziri wetu wa Elimu ameweza. Makofi mengine yamwendee binafsi Waziri wetu Mkuu na Mawaziri wote na Naibu Mawaziri waliotembelea kila sehemu ya nchi hii kutazama maendeleo ya ujenzi wa Shule za Sekondari. Bado walimu wetu hawana nyumba, bado mabweni yanahitaji kujengwa, bado maabara zinatakiwa na maktaba, hizi zinahitaji fedha. Inakuwaje watu wanaweza kuipinga bajeti hii inayoeleza kwamba mambo haya ndiyo yatamfikia kila Mtanzania popote alipo. Mimi sioni haki hapa mtu kusimama anapinga bajeti hii, jamani angalieni uungwana. Mabweni haya watalala watoto wa *CUF*, CCM, CHADEMA,*TLP* bila ya kubagua. Tukubaliane kimsingi tunajenga nchi hii na kujenga nchi maana yake ni kujifunga mikanda, kwa hiyo, tujifunge mkanda tuweze kujenga nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, bajeti inauma ndiyo, lakini nani anayeumwa *Pneumonia* akakataa sindano impe uhai. Ukiumwa *pneumonia* utapigwa sindano, *X-pen* moja, katika

sindano inayouma sana lakini baada ya sindano 4 unapumua vizuri, unaendelea na kazi zako na maendeleo ya matibabu. Nadhani Serikali yetu tuipongeze katika hili kwa sababu tutahitaji fedha na fedha inatoka katika kodi lazima tuiunge mkono Serikali katika kudai kodi zake. Naenda sasa katika afya, huko tena ndio huachi maana yake kila kijiji kinatakiwa kiwe na *dispensary* na kila Kata iwe na *Health Centre,* hii sehemu moja katika Mapinduzi makubwa katika afya yanayoongozwa na Serikali yetu tuyaunge mkono. Maji mahitaji makubwa kabisa, sasa utaona kwamba bajeti inaendana na kutimiza ahadi zilizowekwa katika Ilani ya Chama cha Mapinduzi.

Mheshimiwa Spika, tumeelezwa kazi yetu kuboresha hotuba hizi, kuiboresha hii bajeti wala sio kuipinga. Sasa nilikuwa nadhani bado niko kwa upande wa wenzangu tuiboreshe tusiipinge. Kwa hiyo, mwisho wa siku tukipiga kura tunataka wenzetu wote tuipigie kura ya ndiyo bajeti hii. Sasa naomba nitoe mawazo kidogo juu ya kilimo. Kilimo kimeshazungumzwa hasa sisi kule Rufiji hatuna viwanda ni kilimo tu na ardhi yetu ina rutuba na maji ni mengi lakini bado ninaomba Mheshimiwa Waziri wa Mipango atazame tena kwa sababu nchi hii yenye hekta 44,000,000 inayolimwa sasa ni asilimia 23. Nchi hii inaweza kutoa pato la Taifa kwa kuchangia asilimia 44.7 lakini wakulima wake asilimia 70 wanatumia jembe la mkono na asilimia 20 ndio wale Wasukuma wanaotumia plau ya ng’ombe, asilimia 10 tu ndio wanatumia matrekta.

Mheshimiwa Spika, nadhani tukiweza kunyanyua matumizi ya trekta angalau yafike asilimia 50, pato la Taifa litanyanyuka mara moja na mara moja maana yake nini? Pale Rufiji unalohitaji ni kupanda pamba, huna haja ya mbolea, basi miezi sita unavuna. Tupeni matrekta pale kama 50 hivi kwa kujaribia tu mimi nitayasimamia tutazalisha mara nyingi sana kila aina ya chakula kutoka katika bonde lile. Kwa hiyo, nilikuwa nadhani kwa kuboresha bajeti hii kilimo kifikiriwe sana na kitatoa ziada kubwa yaani mchango mkubwa kuliko hii asilimia 44.

Mheshimiwa Spika, kuna suala lingine nalo ni la barabara. Barabara zetu hasa kuna moja inaitwa Ndundu/Somanga, hapa nimeiandikia, hili ni donda ndugu la Wizara ya Miundombinu. Haipo, barabara hii ni sehemu ya Kibiti/Lindi na ujenzi wake ulianza 1995 mpaka leo Ndundu/Somanga ni matatizo. Mwaka jana barabara hii ilipangiwa kilomita 60 shilingi bilioni 7.6, senti moja haikutumika sijui fedha hizi tutapata safari hii sijui, maana yake zabuni zinasomwa sasa. Mwaka huu tumepangiwa shilingi bilioni 2, sasa kama shilingi bilioni 7 hatukutumia hata senti moja hizi bilioni 2 tutatumia kweli? Kwa hiyo, tunaomba katika kuboresha bajeti barabara ya Ndundu/Somanga sasa ni donda ndugu tunaomba tulitafutie mruturutu ipone au twende kwa Ma-*surgeon* tufanye *amputation.*

Mheshimiwa Spika, kuna barabara inayokwenda *Selous* nayo ni Ikwiriri/ Mkongo/Mloka/Vikumburu. Pale Mloka ni katikati ya utalii wa kule Rufiji, Mheshimiwa Waziri wa Maliasili atakubali kwamba barabara ya kwenda kule ni mbaya sana. Sisi tulidhani kwa kuwa inavuka zaidi ya kilomita 100, sasa ichukuliwe na mkoa kwa sababu ikiwa na changarawe watalii watakwenda kwa wingi. Kwa bahati mbaya sina hakika kama Mheshimiwa Spika umefika kule *Selous* lakini nakuhakikishia tembo wa kule ni wakubwa zaidi, simba wa *Selous* sio kama vile visimba vinapanda miti kule Manyara,

hapana, hawa ni simba wa *Selous.* Kwa hiyo, naomba barabara hiyo itengenezwe. Kuna ahadi ya Rais ya barabara ya Kibiti/Mkongo/Utete na kivuko chake tumeshaahidiwa katika Bunge hili naomba itimizwe. Mwisho barabara inayounga Utete na Nyamwage ambayo ndiyo *life line* inapitika kwa taabu sana tunaomba iimarishwe.

Mheshimiwa Spika, sasa suala la *SACCOS* na uwezeshaji bado tuna tatizo kubwa sana. Maendeleo yaliyotangazwa hapa ukienda kwa wananchi kule chini utakuta uwezo umekuwa mdogo. Kama nilivyosema umaskini bado upo lakini bajeti hii imeamua kwamba tutokane katika tegemezi twende katika kujitegemea na hivyo hivyo ndiyo umaskini utaondoka, lakini kama tukiimarisha kilimo vijijini angalau kila Mtanzania atapata chakula chake na hiyo ndiyo ataona kweli na kubwa kuliko yote *index* ya kupandisha mfumko ni chakula na chakula kikiwepo basi unakuta mfumko unashuka taratibu. Nilikuwa naomba sana kwamba tutazame hii tabia mbaya iliyozuka ya mapesa mengi yanatolewa kutengeneza miundombinu lakini watengenezaji wa miundombinu hiyo hawafikishi viwango vinavyotakiwa. *We are not getting the value for money,* hela nyingi zinakwenda lakini viwango vya utengenezaji ni hafifu. Tunaomba s Serikali ijaribu sana kuhakikisha kuwa wakitoa fedha na sisi tuwemo na tusaidia kuangalia kama hizo fedha kweli zinaleta tija tulizokubaliana.

Mheshimiwa Spika, mwisho nilitaka niwasifu kipekee *TRA*, *TRA* ahsante sana, mnakusanya. Vilevile niwasifu Benki Kuu, ahsante sana mmetuwekea akiba mpaka leo tunaona fahari. Lakini kuna jambo moja nilitaka Watanzania kupitia Bunge hili niliseme linatia aibu sana, nalo ni kwamba watu waliopewa madaraka wakifanya jambo hatujui namna ya kuwasifia, kila siku lawama tu. Nilikuwa nadhani tujirudi tuweze kusifu kwa dhati kwamba kazi nzuri imefanyika. Utaona kabisa hawa watu wa *TRA* wanatuambia unaweza kupitisha mizigo *fast track* na tukafanya ukaguzi . Huyu huyu bwana tulio mwamini kutoza kule ndiye atakwenda kutoza ile *fast track* kule kwenye *destination,* kwa nini hatumruhusu afanye hivyo na tunakazana kama watapitisha mabomu, watapitisha hivi, mabomu yanapitishwa kila siku, maunga yanapitishwa kila siku lakini nia ya wafanyabiashara ni kunyanyua pato lao na vile vile pato la pale wanapofanyia kazi. Sisi tumetembelea Kiwanda cha Sigara, utaona wazi wazi kwamba hawa watu wana nia kabisa ya kunyanyua pato la nchi hii, kwa hiyo nilikwa nadhani tuiunge mkono Serikali ifanye hata kwa majaribio tuwape hata miezi sita wapitishe *fast track* baada ya pale watupe ripoti hapa kama kweli *fast track* inaleta mazao mazuri, matokeo mazuri au hapana?

Mheshimiwa Spika, lingine ni suala lililojitokeza. Mimi mtanisamehe nitataja majina kidogo. Wakati marehemu Mwaikambo alipojenga Kitega Uchumi, alipata msukosuko, mara kahamishwa *NIC* akapelekwa sijui wapi, mpaka Mwenyezi Mungu kamwita. Haya ndugu yangu Mataka, *PPF Tower* kujenga, matatizo yaani sijui sisi hatutaki kujenga vitu vya maana na sijui nia yetu ni ipi? Mimi nadhani tukubali sasa *PPF Tower* ni fahari. Kama umo katika ndege unafika Dar es Salaam unaona kitu kinasimama hivi unasema ndiyo ile ndiyo nchi. Ukienda Benki Kuu, utakuta ziko *towers* yaani kwa kweli zinapendeza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba kuunga hoja mkono mia kwa mia. Ahsante. *(Makofi)*

**MHE. LUCAS L. SELELII:** Mheshimiwa Spika, kwanza naanza kutoa salaam za pole kwa ajali iliyotokea pale Singida, Mwenyezi Mungu azilaze roho za marehemu mahali pema peponi. *Amin.*

La pili mimi ni msemaji wa 79, sitaki kutofautiana mengi ya mazuri ambayo wengi wetu hapa wameyazungumza na kuyasema na hasa katika kushauri na kuboresha Bajeti yetu hii ya mwaka huu. Kwa hiyo nawaunga mkono waliyosema wapande zote mbili kwa kweli wamesema mambo mazuri ya maana na naamini Serikali itayafanyia kazi na hasa marekebisho ya ushuru kwenye mafuta hasa mafuta ya taa. *(Makofi)*

La tatu, mimi nimesali sana leo na hapa bado nimefunga, natafuta lugha gani nzuri naomba Mungu anisaidie tu nitoe mchango mzuri kwenye Bajeti hii. Ila inauma na msema kweli ni mpenzi wa Mungu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nikiwa kama mwana CCM ninasema nitasema kweli daima, fitina kwangu mwiko. Kwa hiyo, kwa uchungu huo nimerekebisha na kwa sababu ya matakwa na masharti ya Katiba nimerekebisha uchungu wangu niupeleke kwa Waziri wa Miundombinu, Waziri wa Madini  na Waziri Mkuu kuwaondolea shilingi kwenye Wizara zao. *(Makofi)*

Waziri wa Madini kwa sababu mbili, ya kwanza mwaka jana alituahidi kwamba sasa hivi jamani huko vijijini tunaleta umeme huko kaeni mkao wa kula. Tumerudi wanaume tunaenda kuwatangazia wananchi kwamba umeme unakuja, mpaka leo wanakwambia msubiri msubiri. Hawa waliopo mstari wa mbele ni wajanja kweli wao wanajitengenezea kule kwao mazuri mazuri ikifika wakati wa uchaguzi wanakupigia simu tu. Eeh vipi huko Bwana nasikia *CUF* wamekukaba sana, wamenikaba sana kwa sababu hamjatekeleza Ilani ya Uchaguzi. Inauma sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, la pili, juzi wamewakamata vijana wanaowaibia wazungu madini ya Tanzania. Hajasema wale wazungu wanaoiba madini ya Tanzania amewafanya nini na siku zote tunalalamika hapa kwamba mchanga huu wa dhahabu unaibiwa una madini ya dhahabu. Serikali inakataa hakuna, hakuna ushahidi. Sasa mbona mnawakamata hawa Watanzania? Wamesema wameiba bilioni 1.7, mmejuaje hiyo thamani ya madini? Na hamjatuambia ule mchanga unasafirishwa kule nje unaleta shilingi ngapi? Inauma sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Miundombinu, mwaka jana hapa tumezungumza hapa hapa katika Bunge hili hili tena na Waziri Mkuu namkaba kwa sababu gani aliwatetea. Mimi aniambie hawatetei nitamrudishia shilingi yake lakini akiwatetea na yeye shilingi yake naitoa. Waziri wa Miundombinu akaahidi barabara ya kutoka Manyoni – Itigi - Tabora hadi Kigoma, akaahidi barabara kutoka Nzega -  Tabora  - Sikonge hadi Mbeya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wewe hata ukipata habari sasa hivi unatakiwa Urambo leo huendi. Utabidi uondoke hapa uende Dar es Salaam, upande ndege uende mpaka Kigoma urudi mpaka Tabora ndiyo uende Urambo. Wenzio wakitakiwa kwenda Arusha sasa hivi

wanakwenda, wakitakiwa kwenda Mbeya wanakwenda sasa hivi. Kosa tu sisi kule Magharibi mpaka lini? Miaka 45 subira kila siku subira, subira hii mpaka lini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, inauma na inaumiza. Itafika wakati wa uchaguzi, uchaguzi tumetekeleza Ilani, barabara ya Segera, sijui barabara ya Arusha, sijui barabara ya Mbeya, ya Tabora je? Kutoka Dodoma kwenda Urambo Tabora, ni sawa sawa kutoka Dodoma kwenda Dar es Salaam lakini nikatalie na niko tayari kukaa kama wewe ukisema uende Urambo sasa hivi, hufiki Urambo, haki ya Mungu hufiki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Waziri Mkuu akasimama akawatetea, akatoa ushawishi kwamba Serikali imesikia, Serikali itafanya kila kitu. Wamewekeana wao kwa wao tu. Naomba wakati wa barabara na wakati wa madini naomba nitoe shilingi na nitatoa kabisa wajue natoa shilingi ya Waziri kabla ya wakati. Hizo mbili siziungi mkono. *(Makofi)*

Lakini kwa matakwa ya Sheria na Katiba Ibara ya 90 nimeisoma sana nawajibika niunge mkono kwa hoja hii ya Bajeti, ninawajibika. Kwa shingo upande ninaunga mkono hoja hii. Lakini ingekuwa kuna kipengele cha kuunga mkono huku hawa unawanyima mshahara hapa hapa ningeanzia kuwakata mishahara yao, Waziri wa Nishati na Madini, Waziri wa Miundombinu na Waziri Mkuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa nataka kushauri na naomba Mwenyezi Mungu nishauri vizuri hasira imeisha. Naomba kushauri la kwanza, Wizara ya Mipango, Uchumi na Uwezeshaji inayoongozwa na Waziri wa Mipango na wataalam kiwe ni kiungo kama injini ya gari katika kupanga na kuweka *scenario* ya mipango mbalimbali; na ingefaa Waziri wa Mipango, Uchumi na Uwezeshaji awe *Ex-Official* kama alivyo Mwanasheria Mkuu wa Serikali, asiwe mwanasiasa.

Mheshimiwa Spika, juzi katika majibu ya Waziri wa Mipango, Uchumi na Uwezeshaji kwenye magazeti fulani akajibu kwamba, " na Wabunge nao walitaka." Mimi nadhani mipango ilikuwa imeelekeza kwamba Serikali imejipanga kufanya hivi na hivi na hivi katika *scenario* ambayo wataalamu wetu wanatuwekea. Kwa hiyo, hili la kwanza lingerekebishwa ili Waziri wa mipango pengine anasumbuliwa na wanasiasa na Jimbo atafute *Ex-Official* yeyote ambaye ni mchumi aweze kuwa miongoni mwa Mawaziri ambao ataongoza Kitengo hiki cha Mipango. Hilo la kwanza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, la pili wengi wamesema ukuaji utalii, kwamba tunajitaji utalii tuukuze nchi yetu iweze kuwa na watalii wengi. Lakini ukisoma hotuba ya Mipango, ukisoma kitabu cha Waziri wa Fedha, soma vile vitabu vya Bajeti, soma kitabu cha maendeleo, soma vitabu vyote vya mwaka huu, hatujasema kama tunawekeza fedha zozote kwenye kuwa na Shirika la Ndege la Taifa, hakuna. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, utawaletaje watalii kutoka huko wanakotoka bila kuwa na *National carrier.* Tunalalamika kila siku hapa *Kenya Airways, South African Airways*. Wao ndiyo wamewaleta, sasa unataka uvune usichopanda? Hakuna pesa yoyote ambayo imetengwa kwa ajili ya kuimarisha Shirika la Ndege na haiwezekani ukaimarisha utalii kama huna Shirika la Ndege, haiwezekani na tulisema hapa hapa. Unajua wenzetu wa

mstari wa mbele huwa wanatuona sisi wa mstari wa nyuma huku kama vile hatunazo. Tuliwaambia hapa hapa kwamba jamani hii ndoa ya kuungana na *South Africa Airways* haifai, hapa hapa tumesema sana hapa. *(Makofi)*

Lakini wenzetu kwa sababu wamekaa mstari wa mbele wana nini, wanatuona tena sisi basi. Kama ungekuwa na akili na wewe si ungeenda mbele. Mtatuelewa vibaya ndugu zetu. Wote tupo kwenye uwanja mmoja lazima tuwe na makusudi mazima ya kuanzisha Shirika la Ndege la Tanzania. Wenzetu *Kenya Airways* wajanja sana na wataendelea kutuibia hivi hivi, wamejiunga na *Precision,* wamejiunga na *KLM*. Kwa hiyo, wanafika kule ambako watalii wanatoka na lazima washuke Nairobi. Wakishuka Nairobi watakuja Tanzania kama wanakuja chumba cha pili cha Kenya. *South Africa* vile vile, kwa hiyo, sisi kama hatujazingatia kuimarisha Shirika la Ndege kufuata watalii kule wanakotoka hatutakuwa na utalii wa kutosha.

Kwa hiyo, mimi napenda hili katika mipango ya Waziri wa Fedha au wa Mipango lisisitizwe ili tuwe na *National carrier* kama huyo mtalaka *South Africa Airways* bado anakitu anatudai tumlipe ili tuachane naye. Huwezi ukawa na mtu ambaye ana nguvu za kiuchumi ukashindana naye huwezi, tutafute watu wenye mapenzi bora si Shirika la Ndege la *South Africa. (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, la tatu ni sekta ya mifugo. Kusema kweli sekta ya mifugo si kwamba imesahauliwa, inadharauliwa. Narudia sijakosea, si kwamba imesahauliwa, bali inadharauliwa mpaka Waziri wa Mipango, Uchumi na Uwezeshaji anaiita sekta ndogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, inakuaje sekta ndogo ya mifugo? Rais mwenyewe ameunda Wizara kwa ajili ya Mifugo, Waziri wa Mipango anasema ni sekta ndogo. Lakini kwa sababu Tanzania tunapenda kudharau mambo ningependa hapa kwa kweli kama tunataka kuongeza mapato kwenye pesa zetu za ndani na za nje ni kwenye mifugo. Ni kwa rahisi sana kwa kuvuna kuliko hata kulima. Kwenye mifugo ni rahisi sana kuvuna, sasa hivi makampuni mengi na mashirika mengi yanaagiza kuku na yanaagiza kwa dola kutoka nje.

Mheshimiwa Spika, sasa hivi ndugu zetu wengi ambao ni wakulima na ambao ni wafanyabishara wanafuga. Tanzania ni ya tatu kwa mifugo Afrika, ukiondoa Ethiopia ambao wana vita na Sudan ambako kuna vita. *(Makofi)*

Lakini bado hatuja-*take advantage* ya kuwa wa tatu kwenye mifugo kama Botswana walivyofanya. Botswana wana mifugo milioni tatu lakini ni wa kwanza kusafirisha nyama kuliko Tanzania ambao ina mifugo, ng'ombe tu milioni 19, mbuzi tuna milioni 15, kondoo milioni 3, lakini tuna viwanda vitatu kingine cha Dodoma kipo hapa nyuma ya Bunge lako utasema nayo ni machinjio kweli haya. Hakuna hata ng'ombe mmoja anayekwenda kuchinjwa pale. Ng'ombe wetu hawa wengi wanauzwa kwenye mnada, kule kwetu Nzega, Shinyanga. Shinyanga wana ng'ombe wengi kweli wana ng'ombe milioni tano peke yake lakini hakuna hata machinjio, hakuna hata kiwanda kimoja cha mifugo. Wanauzwa ng'ombe kwa kuangaliwa sura, hamsini, sitini, sitini *over,* ng'ombe amekwenda. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, hiyo dharau itakuwepo mpaka lini? Lazima tuchangamkie kwa sababu mifugo ni dhahabu ambayo iko juu, hauhitaji wawekezaji kutoka nje, hauhitaji muda mrefu kutoka nje na haihitaji fedha nyingi kama vitu vingine, ni maamuzi tu. Lakini tumedharau kitu cha muhimu sana na cha msingi mifugo. Mifugo ina mazao manne ya haraka haraka, utakula nyama, utaweka ngozi, utaweka mbolea, utaweka maziwa na samli utapata. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, basi tu inanibidi niunge mkono lakini inauma sana. Mifigo wanadharauliwa. Nimalizie kwa haraka haraka. Mikoa ya wafugaji ningependekeza, kila Mkoa wa wafugaji anzia Shinyanga uende Mwanza na Mara, Singida, Tabora na Arusha yawekwe machinjio na soko la uhakika ili mifugo wauzwe kwa bei nzuri bila kumpunja mfugaji; na huo ndiyo MKUKUTA. Kwa sababu mfugaji atapata pesa na wewe utapata fedha za nje, naomba Serikali ipige marufuku kuagiza nyama nje. Kuku wa nini wa Brazil? Kuna kuku wengi sana Shinyanga, Tabora na kuna kuku wengi sana Singida. Unaagiza wale kuku wa nje wanaougua ndiyo maana mnaleta magonjwa ya ajabu ajabu kwa kutumia nyama ambayo wala haifanani na mazingira yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, la mwisho naomba Waziri akubali, Dar es Salaam iwe *free port*. Lakini ikiwa *free port* aimarishe Bandari zifuatazo, Bandari ya Mtwara, Dar es Salaana na Bandari ya Kigoma. Ikiwa Dar es Salaam ni *free port* aimarishe barabara ya kutoka Dar es Salaam kwa uhakika mpaka Kigoma na Reli kutoka Dar es Salaam mpaka Kigoma. Kuna soko la kutosha kubwa kabisa pale *DRC Congo,* Burundi na kuna soko la kutosha pale Rwanda hata Uganda. Lakini sasa hivi kwa sababu Dar es Salaam na ukiritimba wao badala ya kupitishia Dar es Salaam wanapitishia Mombasa na kwa sababu hatuna miundombinu badala ya kupitishia Dar es Salaam kwa Kigoma kwa kupata soko lile la Mashariki ya Kongo wanapitishia Uganda na Mombasa. Juzi *TRC* hii *TRC* ya sasa ambayo tunaibinafsisha na katika hili ubinafsishaji kwa kweli nilikuwa naomba hii mikataba tuingalie. Ukiumwa na nyoka hata ukiona unyasi tu unashtuka na hapa tunashtuka. Ubinafsishaji gani kila mara subirini kidogo, mara mwezi wa kumi mara lini na hata hivi tuna wasiwasi kwamba hivi hawa watu wanatutakia nini na hasa Mikoa ya Magharibi na Ziwa, tuna nini kule au ndiyo Tanzania B? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, bado ningehitaji hata ile *Dry Port* ya Isaka na yenyewe iimarishwe. Kama huna fedha Waziri Fedha angalau jenga hata kwa *BOT* watalipa. Mfano wa Ghana, inalipa ile reli na bandari kavu ile na kama huna fedha wale watu wa Kongo, Burundi, Rwanda wanahitaji sana hizi barabara na hii reli. Tunaweza kushirikiana nao, tukakubaliana nao tukawapa *concession* miaka kumi au ishirini tukawa na barabara ya kutosha na reli ya uhakika tukapitisha mazao na bado tukafaidika na miundombinu ambayo iko katika maeneo hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sitaki kengele inililie kwa sababu nilisema naunga mkono kwa kufanyeje, basi nikubali yaishe. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. LUCY T. MAYENGA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii ili walau na mimi niweze kutoa mchango wangu katika Bajeti hii. Kwanza

kabisa napenda niungane na Wabunge wenzangu kutoa pole kwa wafiwa wote waliopata matatizo kutokana na ajali iliyotokea Mkoani Singida ikihusisha basi la *Mohamed Trans*.

Mheshimiwa Spika, vile vile nikiwa kama Mbunge wa vijana napenda pia kutumia fursa hii kuipongeza timu ya *Taifa Stars.* Ni vijana wenzangu ambao na wenyewe kwa fani yao wameweza kuonyesha uzalendo na kwa kuweza kwa kweli kuendelea kuhamasisha vijana maana sasa hivi mpira unachukuliwa kama ajira. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi mchango wangu katika Bajeti hii nisingependa sana kurudia kuhusu yale ambayo yamezungumzwa na wenzangu. Kwanza kabisa nitoe pongezi za dhati kabisa kwa Wizara hizi mbili ambazo kwa kweli zimeweza kwanza kutupa sisi Waheshimwa Wabunge kwa kuvipa vipaumbele yale mapendekezo ambayo Wabunge wenyewe waliyapendekeza. Itakuwa si jambo la busara ikiwa kama sisi Wabunge wenyewe ndiyo tulikaa tukakubaliana kwamba jamani vipaumbele viwe moja, mbili, tatu, halafu sasa hivi tunageukana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kupanga ni kuchagua, lakini katika hili Serikali imeweza kukaa na kuangalia kwamba ili nchi yetu iweze kuendelea katika nia ya kuamua kuweka Taifa letu kuwa nchi ya kuweza kujitegemea yenyewe na kwa ujumla tumeona kwamba suala la elimu ni suala ambalo tunaona linaweza likatukomboa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naunga mkono kabisa vipaumbele hivi kwa sababu hata hizi nchi ambazo zimeendelea kwa kiwango kikubwa nchi ambazo zimeendelea kwa kiwango hawana maliasili hawa, hawana milima hawa, hawana madini hawa lakini elimu peke yake ndiyo kwa kweli kwa kiwango kimeweza kuwainua na kiasi ambacho hivi sasa wameweza kufika mbali.

Mheshimiwa Spika, naomba kwamba Serikali kwa kutenga kiwango cha asilimia 18 katika hii Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi kwa kweli ni jambo ambalo halina budi kusifiwa. Kwa kweli imeweza kuonyesha kujali kwake licha ya kwamba Serikali hata hivyo haiwezi kwa kweli kwa siku moja au kwa mwaka mmoja kuweza kumaliza matatizo yote. Yapo matatizo mengine ambayo itabidi kushughulikiwa kama matatizo ya ujenzi wa mabweni, lakini vile vile ujenzi wa maabara. Vile vile napenda kwa niaba ya vijana wenzangu hasa vijana wa Jumuiya ya Vijana wa Chama cha Mapinduzi, kwa kweli hatuna budi kumpongeza Waziri wa Fedha. Waziri mwanamke, Waziri ambaye ameonyesha uzalendo, Waziri ambaye ameonyesha uwezo wake wa kuchapa kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwaka jana nchi yetu ilikabiliwa na matatizo mbalimbali, kuna suala la ukame, kuna suala la umeme na mafuta bei ilikuwa juu. Kuhusu kiwango cha akiba kwa ajili ya *import* nchi iliweza kuwa na uwezo wa kuweza kufikiwa na kiwango cha asilimia 6.6 ingawa kawaida huwa inakuwa ni asilimia nane. Lakini licha ya haya matatizo yote kwa kweli nchi yetu haikuweza kuyumba. Kwa hiyo, sina budi kutoa shukrani zangu za dhati na kwa niaba ya vijana wenzangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ongezeko la Bajeti ni shilingi trilioni 1.2. Sina tatizo sana na matumizi katika Serikali. Tatizo langu ni jinsi matumizi haya yanavyopelekwa katika sehemu mbalimbali. Wasiwasi uliopo sasa hivi kwa wananchi wengi ni kwamba ni jinsi gani Serikali itaweza kusimamia matumizi haya na ongezeko hili la pesa ambazo zimeweza kuongezwa. Wananchi wanaweza wakakubali kufunga mikanda, lakini je, haya matumizi na hizi pesa zinazoongezwa kwa sababu kuongeza Bajeti ina maana kwamba umeweza kujitathmini kuhusu matumizi uliyafanya hapo awali.

Naiomba Serikali iweze kuangalia katika baadhi ya matatizo ambayo yameelezewa katika taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali kuhusu upotevu wa mamilioni ya fedha katika sekta ya manunuzi, *almost* asilimia 20 ya pesa zimepotea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi nadhani, Rais wetu pamoja na Waziri Mkuu, tunajua kwamba ni wakali sana na kwa kweli katika hili inabidi waongeze zaidi. Wananchi watapata uhakika na wananchi wataiamini Serikali yao na watakuwa tayari kufunga mikanda ikiwa kama baadhi ya watu watawajibishwa. Katika baadhi ya maeneo kumekuwepo na uthibitisho, pengine unaweza ukawa ni uthibitisho wa maneno au wa kuona lakini kuna baadhi ya maeneo unaona kabisa kwamba watu *weather* ni wakuu wa vitengo, *weather* ni wakurugenzi au ni watu fulani wakubwa ambao wanakula. Sasa itakuwa sikuwatendea haki wananchi ikiwa kama huku tunawaambia wafunge mikanda na wanakubali wafunge mikanda na kwa sababu hawana jinsi hapa tukishakaa, tukishajadili mambo yatapita. Watafunga mikanda, lakini mimi nadhani Serikali haina budi kwamba hawa watu ambao wanatumia vibaya mapato ya Serikali waweze kuwajibishwa ili uwe mfano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuna vijana wengi ambao wamekwenda shule, kuna vijana wengi ambao wana uwezo ambao wanaweza kuifikisha nchi yetu kule tunapotaka ikiwa kama hawa watu wengine ambao wameendelea kukaa humu ndani ambao wameonekana kuleta matatizo naomba wakae pembeni ili sisi vijana tuendelee na mambo mengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, suala lingine ambalo nataka kuzungumzia ni suala la *fast track*. Kwa maoni yangu ninaunga mkono kabisa kuhusu uamuzi huu wa *fast track*. Mfumo huu unatumika Durban, mfumo huu unatumika Mombasa, mfumo huu unatumika Dubai hadi Singapore. Karibu Bandari hizi kubwa zote ambazo hapa tumekuwa tukikaa tunazungumzia kwamba tunataka Tanzania iwe *free port* kama Dubai na sehemu nyingine wamekuwa wakitumia huu mfumo. Mimi sikubaliani na wenzangu ambao wanasema mfumo huu unaweza ukapitisha silaha. Utaratibu huu ni sawa sawa na utaratibu wa kuwepo *VIP* katika *Airports* na utaratibu wa watu wengine kupita katika njia za kawaida. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuna baadhi ya vitu ambavyo watu wengine hata sisi Wabunge tunapita *VIP,* huwezi kupita na silaha kwa sababu unalinda heshima yako. Kwa hiyo, kuna baadhi ya masuala ni masuala tu ya kuaminiana na kwa kweli ni kulindiana

heshima. Makampuni haya ambayo yanapitisha hizi bidhaa huku *fast track* ni makampuni 80 ambayo yanachangia asilimia 60 ya Bajeti.

Sasa huwezi kusema kwamba hawa watu watapitisha sijui na silaha, watapitisha sijui na dawa za kulevya. Pia tujue kwamba hii ni nchi ambayo haiwezi kukaa inaangalia tu haya mambo eti na dawa za kulevya zinapitishwa na sisi tumekaa tunaangalia haiwezekani. Kutakuwa na mipango ya kuweza kudhibiti haya mambo, kutakuwa na mashine za kufanya *screening* lakini vile vile Serikali ina vyanzo vingi na ina vyombo vingi vya kuweza kuhakikisha kwamba haya mambo mabaya hayatokei katika nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, suala lingine ambalo nataka kulizungumzia ni suala la *Treasury Bills*. Serikali imesema kwamba sasa hivi haitaki kukopa kwa maana ya kununua *Treasury Bills* najua kwamba haiwezi kufanya namna hiyo lakini najua kwamba kwa *money policy* ya kuweza ku-*control money circulation treasury bills* zitakuwepo. Mabenki yote Tanzania yalikuwa yanatumia kununua hati fungani pamoja na *bonds*. Lakini vile vile makosa ambayo yalikuwa yanafanyika Serikali ilikuwa ina-*offer interest* kubwa kiasi kwamba Benki anasema kwamba hivi mimi nikiamua kununua *treasury bills* kwa Serikali nitapata *interest* ya *weather* ni asilimia 17 au 18.

Sasa iweje tena mimi nikubali kumkopesha mwananchi wa kawaida ambaye yeye anataka apate asilimia 10 au 11. Naunga mkono Serikali kwa uamuzi wake wa kufuta hizi *treasury bills*. Lakini vile vile *treasury bills* kwa maana ya kukopa Serikali imefuta, naomba sasa hivi nchi yetu *GDP* ni *12 billion USD. Inflation* iko *around 7 percent, interest rates* iko kwenye *10 to 12 percent*. Naomba kwenye Mabenki kuna mfumo, ninaomba Serikali iweze kuangalia njia yoyote ya kuweza kuongea na haya mabenki ili yaweze kuwakopesha wananchi wetu katika riba ndogo.

Mheshimiwa Spika, hivi sasa wamekuwa wakihamasika na uundwaji wa *SACCOS,* lakini kuna mifumo mbalimbali ya kuweza kuhakikisha kwamba hawa wananchi wanapata mikopo tukianzia na mfumo huu wa hizi bilioni moja ambazo zimetolewa. Lakini naona pia haya Mabenki yanaweza pia yakatumiwa endepo kama yakiomba kwa sababu huwezi kumlazimisha mtu kulingana na *policy* nzima ya Benki katika masuala ya kukopeshana. Waweze kuangalia mfumo mzuri ambao unaweza ukasaidia katika masuala ya kukopa. Lakini vile vile suala lingine *index* ya *inflation* ni chakula. Katika uzito wake asilimia 55 ya mfuko huu yaani *basket of good*s iko katika chakula, *power* na maji ni asilimia 8, usafiri ni asilimia 9, kulingana na hotuba ya Waziri wa Fedha ameelezea kwamba *inflation* itashuka. Hili litafanikiwa ikiwa barabara zetu vijijini zitajengwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Serikali imepanga matumizi na kuweza kuweka makadirio yake lakini ukiangalia hasa unaona kwamba mapato na matumizi yako pale pale hakuna akiba. Kwa hiyo, *inflation* itaweza kufanikiwa kuendelea kushuka chini au kubaki ilipo ikiwa kama Mungu akitujalia tukipata mvua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, suala lingine ambalo napenda kuzungumzia naomba Mheshimiwa Waziri wa Fedha aweze kutuainishia kwamba Serikali itapunguza matumizi

yake katika maeneo gani ikiwa makisio yaliyowekwa hayatatimia. Serikali imepanga kwamba tunatarajia kupata kiwango hiki na tunatarajia kutumia kiwango hiki. Lakini tumekuwa tukiona kwa mfano katika Bajeti ya mwaka jana shilingi bilioni 191 ambazo zilikuwa ni za mradi wa umeme vijijini zilienda katika matumizi mengine na miradi 46 ya umeme ilisimamishwa. Sasa na wananchi huko vijijini wanahitaji umeme. Katika baadhi ya vitu ambavyo wananchi wamekuwa wakivipigia kelele ni masuala ya umeme, barabara na vitu vingine. Sasa mimi nadhani kwamba Serikali iweze kufanya mpango wa kuweza kuainisha maeneo ambayo unaweza kusema kwamba endapo matarajio yetu na mipango yetu isipotimia katika 1, 2, 3 tutafanya 1,2,3 lakini bila kuathiri wananchi hasa walioko huko vijijini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwisho ni kuhusu ushauri wangu, naomba huu mpango wa MKURABITA uweze kufanywa haraka kwa sababu huu ndio mpango pekee unaweza ukamuinua mwananchi kutoka katika hali ya chini. Lakini vile vile suala la *raw materials* za hapa nchini. Hivi kwa nini kila mtu akisimama anasema kuna *gypsum* huku na huko? Waziri wa Nishati na Madini leo asubuhi nimemsikia akisema kuna *gypsum* Kilwa lakini tatizo ni barabara. Sasa basi Serikali iweze kuangalia kama haya matatizo ni barabara au vitu vingine waweze kuhakikisha kwamba hivi vitu vinaweza kushughulikiwa. Kwa sababu tuangalie pia hivi kwa ujenzi huu wa barabara Serikali kama ikiamua ikitoa pesa zake kwenye ujenzi wa barabara pale Kilwa itapata *income* ya kiasi gani kwa kuuza hizo *gypsum*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, la mwisho ni kuhusu mifumo ya kodi katika *East Africa*. Nchi yetu itakuwa kama ni kijiji kimoja kati ya Tanzania, Kenya na Uganda. Lakini tuangalie tunahamasisha kiasi gani kuhusu mifumo ya kodi katika nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, Uganda sasa hivi katika Bajeti yao hii ya mwaka huu wao wametoa kodi zote kwa viwanda ambavyo vinazalisha bidhaa zinazouzwa nje. Sasa Kenya na wenyewe wanajaribu kujiboresha kwa namna moja au nyingine katika masuala ya kodi, Uganda ndio kama hivyo wanaamua kufuta, Tanzania tutasema kwamba sisi tunataka jamani nyie wawekezaji mje, hebu tujiangalie kwamba sisi tutasimia katika kitu gani? Kwamba hivi tunapunguza umeme ili hawa wawekezaji waweze kuja?

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja asilimia mia moja! *(Makofi)*

**MHE. PAUL P. KIMITI:** Mheshimiwa Spika, na mimi niungane na wenzangu kuwapa pole wenzetu wote waliopata mkasa na kuwapongeza vijana wetu wa Taifa Stars kwa kazi nzuri waliyofanya kujenga heshima ya nchi yetu. Lakini, pia nitumie nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Fedha pamoja na Waziri wa Mipango, Uchumi na Uwezeshaji kwa maandalizi mazuri ya Bajeti. Mimi nataka kusema wazi kabisa kwamba naunga mkono hoja hii na nina sababu zangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa wana Rukwa wangependa kutumia nafasi hii kupitia kwangu na kwa Wabunge wenzangu, kumshukuru Rais, Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, kwa heshima aliyotupatia kwa kitu ambacho kilikuwa hakijatokea katika Mkoa wetu, kwa kuwaalika wawekezaji mbalimbali kutoka ndani na nje ya nchi kuja kuona

Rukwa kuna nini na kwa mara yao ya kwanza wameshangaa kuona rasilimali zilizomo katika Mkoa wa Rukwa ni nyingi kuliko Mikoa mingi sana katika nchi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa mara yake ya kwanza, Ndugu yetu Reginald Mengi ambaye tangu kuzaliwa alikuwa hajafika Sumbawanga, alishangaa kuona uwezo mdogo wa wachimbaji wadogo wadogo wa madini mbalimbali yapatayo 32 na akaahidi kuwasaidia kuwatafutia angalau wawekezaji wakawasaidie ili waweze kufufua hali yenyewe waliyokuwa nayo. Tunamshukuru kwa hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa Wabunge wenzangu wamezungumza mengi. Mimi nataka kuanza kwa kusema hivi, wawekezaji mahali popote wanachoangalia ni miundombinu. Kwa Mkoa wa Rukwa watanishangaa watu wa Rukwa pamoja na Sumbawanga kama sitazungumzia suala zima la matatizo ya barabara. Nalisema hilo kwa sababu si kwa Sumbawanga tu. Ajenda ya sasa ya kila mahali ni barabara na vivuko. Leo asubuhi tumeona wananchi wanavyolalamika pale Dar es Salaam, Kivuko cha Kigamboni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ajenda yetu ya kwanza, nataka nimwombe Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Waziri wa Mipango, Uchumi na Uwezeshaji katika nchi hii waangalie suala zima la miundombinu. Mimi nataka nimshukuru Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa dhati, kwa sababu sisi katika Kamati yetu ya Miundombinu baada ya kutambua Bajeti iliyokuwa imetengwa kwa ajili ya miundombinu ilikuwa ni kidogo na isingeweza kukidhi mahitaji, tukaomba tuonane naye kupitia kwa Waziri wa Fedha na Waziri wa Mipango, Uchumi na Uwezeshaji, wakaandaa kikao tukakutana naye na kwa mara yetu ya kwanza tulimshukuru kwa sababu alikubali kwa kushirikiana na Rais kuongeza viwango, hivyo mlivyoviona vimeongezwa kwenye hotuba ya Waziri wa Fedha ni viwango tulivyokuwa tumeomba ya kwamba ni vizuri tukaongeza fedha kwa ajili ya miundombinu ama sivyo, Bunge halitapitisha Bajeti hii. *(Makofi)*

Sasa mimi napenda kumshukuru kwa sababu si kawaida Bajeti ikishaandaliwa wakaja kuifumua, si kawaida, ni mara chache inatokea. Lakini, huu ni mwanzo wa kuonyesha kumbe Wabunge mkitoa maelezo na yakieleweka mapema, Rais huwa anasikiliza na kwa kutumia Baraza lake la Mawaziri hukubali kufanya marekebisho. Mimi nataka kuipongeza Serikali ya Awamu hii ya Nne walivyojitahidi kufanya hivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lingine ni kuwa Rais alipokuwa anaunda Baraza la Mawaziri alikuwa na imani nalo na mpaka sasa ana imani nalo na sisi tunawaamini Mawaziri na ninyi lazima mtuamini. Tunayosema ni kutaka kuboresha utendaji wetu wa Serikali. Kazi yenu na sisi ni moja. Nalisema hilo kwa sababu maneno mengi yamezungumzwa hapa ni maneno ya kuimarisha, ni maneno ya kusaidiana, ni maneno ambayo tunataka tujenge sasa umoja ili yale ambayo mnaona kwa kweli yanaweza kuwa na athari katika uchumi wetu, basi myachukulie *seriously*. *(Makofi)*

Mimi nataka niwaombeni Waheshimiwa Mawaziri kupitia Waziri wa Fedha na Waziri wa Mipango, Uchumi na Uwezeshaji ya kwamba kilio cha Wabunge kuhusiana na ongezeko la kodi ya mafuta mliangalie kwa makini sana na hasa mafuta ya taa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa mafuta ya petroli na dizeli, mimi naunga mkono. Naunga mkono kwa sababu kwa miaka mingi, sisi ambao tumekaa ndani ya Serikali, kumekuwa na tatizo kubwa sana kutegemea wafadhili ndio waje watujengee barabara zetu. Tabia hii tukiendelea nayo, hatutajenga barabara nchi hii. Nalisema hilo kwa miaka yote barabara zote hizi zimekuwa zikichelewa na ahadi za Mawaziri wakati mwingine wamekuwa wakizitoa wakitegemea wafadhili watatupatia fedha. Kama hawakuleta fedha, hutafanya lolote, huna lolote la kufanya. Lazima tuwe na mfuko wenyewe, tukubali kujikamua wenyewe tujenge barabara zetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi nashauri ya kwamba sasa tumeanza vizuri. Hii shilingi 100/= iliyoongezeka kwa lita ya petroli kwa *inflation*, mimi nimefanya hesabu, ooh itaongeza *inflation"*! *Inflation* kama itaongezeka ni *0.4 per cent*, ni *0.4* ndio *inflation* itaongezeka kiasi hicho. Kwa msingi huo, laizma tuone, tukianza kuogopa kwa ajili ya ushauri ambao wanatuletea wataalamu kutoka nje, tutakwama kutengeneza barabara zetu. Siasa na Ilani yetu ya Uchaguzi, tutake tusitake, tutashindwa kuitekeleza na tutakuja tusemwe hapa hapa ya kwamba mliahidi kutengeneza barabara zifuatazo…; Mheshimiwa Aggrey Mwanri alipokuwa anazungumzia, alisema Ilani imeanza kutekelezwa na sisi tulipokwenda kumuomba Waziri Mkuu aongeze fedha ni kuhakikisha ajenda ya Watanzania ya kwanza ni barabara. Jaribuni tu, tengeneza barabara tu, acha hata mengine, mtashangaa kura mtakavyopata, kwa sababu ndio kichocheo cha uchumi katika nchi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi natoa mfano, nikitoka Tunduma wakati wa masika, kufika Sumbawanga ni kilomita 230, natumia karibu saa 7. Lakini barabara ikitengenezwa kidogo, natumia saa 2.30. Nikipata ya lami, nitatumia saa 2. Mafuta nitakayotumia ni kidogo, muda nitakaotumia ni kidogo, wasafirishaji gharama zao zitapungua. Watu hawaelewi! Mimi nasema kuna uzuri wake. Tutasikia machungu sasa, lakini baadae kuna faida yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pembejeo ambazo zinatoka Dar es Salaam kufika mpaka Sumbawanga zinakuwa ni gharama kubwa wanapofikiria barabara yenyewe. Lakini kama unaweza kwenda siku moja unaingia Sumbawanga, gharama yake itapungua. Mkulima atakuwa na hali nzuri, atauza mazao yake, yatasafirishwa mpaka Dar es Salaam, na yeye angalau hata hali yake ya maisha itakuwa nzuri, kwa barabara tu, ndio maana nikasema ajenda yetu *number one* kwa kweli iwe ni barabara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, la pili, utakumbuka na wewe mara baada ya vita kuu yetu ambayo tulipambana na Idd Amin, mimi naita vita kuu, kweli tulipambana. Serikali baada ya kuona kuna matatizo ya kiuchumi, ikaanzisha mpango ulioitwa KAMKUKI, kirefu chake ilikuwa ni Kamati Maalumu ya Kusukuma Uchumi Kivita, chini ya usimamizi wa Mheshimiwa Marehemu Edward Moringe Sokoine, ndiye aliye-*speed* ile ambayo ilikuwa inatakiwa kusukuma mambo kivita. Mpango ule kabla haujakwisha

tukapewa ushauri na wataalamu kwamba, hapana, anzisheni *Structural Adjustment Programme (SAP). SAP* kabla haijakwisha, wataalamu wakatufundisha wakasema hapana, anzisheni *National Economic Survival Programme (NESP)* na kabla haijakwisha, tukanzisha *Rolling Plan and Forward Budgeting*, haijakwisha, wakasema hapana, anzisheni kitu kinaitwa *PESA*. *PESA* ni *Personal Economic Survival Activities. (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, yote hiyo ilikuwa ni mizuri, lakini mipango yote hiyo mingine ilikuwa si yetu, ilikuwa ni mipango inatoka nje. Katika utaratibu ambao tumeanza kujenga kufuatana na Ilani yetu ya Uchaguzi, mpango ambao unaweza kusema ni wetu sasa, ni MKUKUTA. MKUKUTA ni mpango wetu ambao umeanza kwa vigezo na maelekezo ya Ilani yetu ya Uchaguzi ya CCM. Lakini, MKUKUTA wenyewe hauwezi kufanikiwa bila kufanikisha, kama Mheshimiwa Mbunge mmoja alivyosema, bila kufanikisha kwanza MKURABITA. MKURABITA unatakiwa kweli upewe kipaumbele. Usipoupa MKURABITA ambao ni Mpango wa Kurasimisha Rasilimali za Wakulima na wafanyakazi wadogo wadogo kama nyumba zao, viwanja vyao na mashamba yao. Usipoweza kuwapa uwezo wa kurasimisha mali zao wakaweza kukopa, bado umaskini utabaki pale pale. Katika kasi hii, uchumi tuseme unaongezeka wakati idadi ya watu inaongezeka kwa kasi, tutaendelea kuwa maskini. Lazima hivi viende sambamba. Ndio maana nasema namuomba Mheshimiwa Waziri aone namna ya kuweza kurekebisha hali hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, juzi tumepata nakala ya sera ya watu. Sera ya watu sasa ndio imetoka rasmi na tunataka hii sera mama, sasa ianze kujibu matarajio ya wananchi. Hivi idadi ya watu ina uhusiano gani na kukua kwa uchumi! Kipi kinaanza, ni uchumi au ni watu? Hiyo ni kazi mojawapo ambayo lazima tufanye, na mimi nitamwomba Mheshimiwa Waziri akipata nafasi tuje tulizungumze ndani ya Bunge hili kama semina, ili wananchi waelewe shabaha na madhumuni ya sera ya watu na wajue majukumu yaliyopo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, suala la elimu. Elimu ya kujitegemea ilipoletwa na Baba wa Taifa Marehemu Mwalimu Julius Nyerere miaka karibu 30 au 40 iliyopita, haikuwa na maana kwamba iwe ni elimu ya watoto wa shule peke yao kuanza kulima mashamba, ilikuwa ni elimu ya kukuza fikra miongoni mwetu ili tuwe na fikra za kujitegemea wenyewe. Tunaposoma, tusome ili tuweze kujitegemea. Tusitegemee watu wengine kutupangia mipango yetu. Mwalimu alikuwa na maana yake hiyo. Lakini, tukakimbilia kwenye elimu ya kujitegemea ni watoto kulima mashamba, tukadhani ndio mwisho. Sasa katika hali hiyo, sisi tungeshauri MKUKUTA ambao umeanza kwa nguvu zote, tusaidiane na twende kwa kasi kubwa kuliko kasi iliyopo. Nasema kasi yetu ni kubwa, lakini sijaridhika nayo kwa sababu mbili.

Mheshimiwa Spika, kwanza mwaka 2002, kwa taarifa yako, kulikuwa na mpango wa *NEPAD*, mpango huo ulikuwa ni mpango ulioidhinishwa na Umoja wa Mataifa tarehe 2 Desemba, 2002. Mpango huo ulikuwa umetoa kibali ya kwamba sasa miji 10 ya Tanzania kupitia *UN-HABITAT,* ipewe maji. Miji yenyewe wakaanza na Musoma, wakaingia Tarime, Nansio, Bunda, Mwanza, Sengerema, Geita, Biharamulo, Muleba na hatimaye wakaingia Bukoba ili kusudi miji hii ipate maji, tangu mwaka 2002 mpaka sasa.

Mheshimiwa Spika, juzi Mheshimiwa Wilson Masilingi amezungumza ya kwamba mbona mradi haujaanza! Inaonekana hiyo *speed* bado, na kweli sasa ni miaka karibu minne. Tunadhani ni vizuri tukaliangalia. Wakati mmoja niliwahi kumuuliza Mheshimiwa Waziri wakati yupo Mheshimiwa Stephen Wasira, tukazungumza naye, lakini *problem* ikawa baada ya kuzungumza, haikuchukua muda akawa amehamishwa tena, ndio tunaanza upya. *Speed* ya kuhamisha Mawaziri nayo imekuwa ni kubwa, kunakuwa hakuna *continuity*. Lakini, hiyo ni kazi ya Rais mwenyewe. Lakini, tungeomba kweli liangaliwe kwa sababu ni suala ambalo litatusaidia ili yale ambayo tunaamua au ambayo Kimataifa tunayapata, yaweze kutekelezwa haraka iwezekanavyo.

Mheshimiwa Spika, mwisho, naomba Mheshimiwa Waziri wa Fedha atusaidie sana kutoa elimu ya kutosha kwa Madiwani wetu kuhusiana na suala la fedha. Matumizi ya fedha yanayofanywa na wataalamu wetu, Madiwani wetu na viwango vya elimu walivyonavyo, kuna njama zinafanyika ambazo hawawezi kuzijua. Wakati mwingine tunawaadhibu Madiwani, tunaadhibu Halmashauri nyingine kwa kuwanyima fedha za ruzuku za maendeleo eti kwa sababu hesabu zao ni chafu. Zinaweza kuwa ni chafu siyo matatizo ya wananchi, ni watendaji ndio wanatumia fedha vibaya, kama ni adhabu basi wapewe wao, kama ni kushitakiwa washitakiwe wao, lakini wananchi wapewe haki ya kupata fedha za maendeleo. Uingereza najua wanafanya utaratibu huo! *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ahsante na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. RIZIKI S. LULIDA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipatia nafasi hii na kuwa mtu wa mwisho kwa kuchangia mchana huu. Awali ya yote, napenda kuunga mkono hoja asilimia mia kwa misingi ifuatayo:-

Kwanza, nimpongeze Waziri wa Fedha, Mheshimiwa Mama Zakia Meghji kwa juhudi anazozifanya kutaka kuleta mafanikio mazuri katika maisha ya Watanzania. Bila kumsahau Waziri wa Mipango, Uchumi na Uwezeshaji, Mheshimiwa Dr. Juma Ngasongwa kwa jitihada zake anazozifanya sasa hivi kuhakikisha wananchi wa Mikoa sita ambayo iko nyuma, wanapata barabara. Kwa kweli, hili mimi kama mzaliwa wa Mkoa wa Lindi na mwakilishi wa watu wa Lindi, lazima nitoe shukrani kwa hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda kutoa rambirambi kwa wananchi wa Lindi kwa msiba uliotokea wa Katibu wa CCM Wilaya ya Kilwa, Ndugu Mwaya. Mwenyezi Mungu ailaze mahali pema peponi roho ya marehemu. Bila kusahau wananchi wa Lindi wanapenda kutoa rambirambi kwa wananchi wa Singida kwa maafa yalitotokea na msiba uliotokana na wa ajali iliyotokea Singida. Hiyo nayo vile vile napenda kutoa rambirambi zangu.

Mheshimiwa Spika, barabara ya kutoka Kibiti – Lindi ni muhimu. Tumekaa kwa muda wa miaka yote tukiwa katika mazingira magumu. Lakini Serikali imeamua sasa hivi kupeleka macho Kusini ili tupate barabara. Pongezi za dhati kwa Mheshimiwa Rais kwa kuonyesha msukumo kuhakikisha mikoa sita ambayo iko nyuma inapewa

kipaumbele, lazima tutoe shukrani za dhati. Waziri Mkuu bila kumsahau, ni mmojawapo ametoa harakati, alikwenda mpaka Lindi kuhakikisha barabara ya Lindi inajengwa na kuwaita Wakandarasi wote wawili wa *KARAFI* na *SIKO* kuhakikisha barabara ya Lindi inapitika mapema iwezekanavyo. Kwa hili, inaonekana yeye anaonyesha uchungu zaidi kuhakikisha ile barabara inapitika. Kwa hiyo, wananchi wa Lindi tunatoa pongezi kwa hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika kuchelewa kwetu Mikoa ya Lindi na Mtwara kutokupata barabara, lakini sasa hivi ni wakati wetu muafaka. Tumepata Daraja la Benjamin Mkapa ambalo sasa hivi limetoa mawasiliano ya Mikoa ya Kaskazini na Mikoa ya Lindi na Mtwara. Kwa kweli hii ni chachu ya aina yake. Lindi mpaka sasa hivi tuna vitu vingi ambavyo vilikuwa havijatumika kwa wakati huo, lakini sasa hivi vitaonyesha mazingira mazuri. Tunaambiwa leo kwamba Lindi kuna dhahabu, Lindi kuna madini mbalimbali, basi naona maendeleo ya barabara yatatupa mafanikio makubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, si hilo tu, tuna bandari nzuri sana ya Mkoa wa Mtwara. Ile Bandari italeta chachu kubwa ya kuondoa msongamano na mrundikano wa mizigo katika Bandari ya Dar es Salaam kama litatumika ipasavyo. Hivyo, barabara ya Lindi mpaka Mtambaaswala, italeta uunganishi kati ya Msumbiji na Tanzania na tutafanya biashara kubwa na Bandari ile italeta u-*busy* wa aina yake na kutoa ajira kwa wananchi wa Kusini ambao kwa muda mrefu tulionekana kidogo maskini, lakini si maskini, tuna rasilimali za kutosha za kutuonyesha sisi kuwa si maskini, sisi matajiri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa nini nazungumzia hilo suala la Bandari, tuna Gesi ya *Mnazi Bay,* katika ufanisi wa Gesi ya *Mnazi Bay* itatuwezesha kuendeleza miradi endelevu ya mbolea, vyuma chakavu, saruji na bado tunayo *gypsum* ya kutosha kuendeleza viwanda katika Mikoa hiyo na kutoa ajira. Kwa nini tusiifurahie hii hotuba? Kwa kweli ni hotuba ambayo inatoa ishara ya kuondoa umaskini katika Mkoa wa Lindi na Mtwara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, upande wa pili ambao napenda utiliwe mkazo ni Wizara ya Maliasili na Utalii. Mkoa wa Lindi tuna vivutio vyote vya maliasili ambavyo havijatumika. Ningeshauri watendaji wa Wizara ya Maliasili na Utalii warudi Kusini wakaitangaze Kusini katika suala la utalii na suala la miradi mingine ya uvuvi. Tunao wavuvi, lakini wavuvi ni maskini wanahitaji kuendelezwa ili na wao waondokane na umaskini.

Mheshimiwa Spika, leo hii Kilwa ina urithi wa dunia ikiwa namba 41. Lakini ule urithi unapotea sasa hivi kwa vile haujatangazwa. Katika *World Heritage*, Kilwa ni namba 41. Ni muda muafaka sasa hivi kuhakikisha Wizara ya Maliasili na Utalii inatumia nafasi hii kuitangaza Kilwa, Liwale, *Selous* ambayo ina asilimia 2 kwa 3. Lakini kutokana na mazingira ya miundombinu, uwekezaji ulikuwa ni mgumu sana. Sasa hivi ni kipindi muafaka cha Serikali kuangalia Kusini na sisi tufurahie matunda ya Tanzania kwa wananchi wa Kusini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sijaachia hapo, ninaingia katika suala la Elimu. Kwa kweli limeniletea mvuto mkubwa na litawakomboa maskini ambao walikuwa muda mrefu wanahangaika na elimu. Lakini zaidi nimefurahishwa na elimu ya msingi, nimefurahishwa na elimu ya sekondari. Lakini, tutie msisitizo katika elimu ya juu. Tunaingia katika Shirikisho la Afrika Mashariki, hatutakuwa na upinzani katika elimu ya sekondari, inabidi elimu ya juu ipewe msaada na miradi mbalimbali Wizara ya Fedha ielekeze Wizara ya Elimu ya Juu, Sayansi na Tekinolojia ili tupate watalaamu wa kutosha, tupate *engineers* wa kutosha na tupate watafiti wa kutosha ili waweze kutuletea taaluma mbalimbali katika nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sina mengi ya kuzungumza, ila sasa hivi nataka kuzungumzia suala la kilimo. Korosho ni zao namba moja katika Mkoa wa Lindi, lakini si korosho peke yake, tuna zao la ufuta. Katika kitabu hiki, zao la ufuta halikutajwa, zimetajwa mbegu za pamba na alizeti. Ni masikitiko yangu makubwa kuona Tanzania tuna alizeti, ufuta, karanga, lakini tunatumia mafuta mabovu kutoka nje na tunapoteza rasilimali kubwa na pesa nyingi kuagiza mafuta nje wakati ufuta wetu tunaupeleka nje kwa kutumia watu wa nje, maana yake ni nini? Je, sisi Watanzania ni walaji wa vyakula vibovu? Hatuwezi kutumia ufuta wetu tukatengeneza mafuta? Ni wakati muafaka sasa hivi, umeme tunao Kusini, pelekeni viwanda Kusini, ninyi Wabunge mnao uwezo wa kutafuta watu wa kujenga viwanda Kusini ili kuwe na viwanda vya kutengeneza mafuta, tuachane na kula mafuta mabovu ambayo yanaweza kuleta matatizo kwa afya zetu.

Mheshimiwa Spika, tuifufue Ilulu, Nachingwea. Ahsante sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nasema tena kuwa Lindi tuna vivutio vizuri na utajiri mkubwa tukiachilia mbali suala la mafuta, vyakula, lakini bado tuna ardhi kubwa ambayo ingeweza kutumika katika kilimo. Tuweke mazingira mazuri na tupeleke matrekta Lindi na tuwekeze katika suala la kilimo. Bado tuna ardhi yenye ekari milioni moja haijatumika. Nafikiri tukitumia kwa ukamilifu, inawezekana, hakuna kisichowezekana.

Mheshimiwa Spika, kwa kweli sina mengi ya kuongea, namalizia hapa na nasema ahsante sana! Naunga mkono hoja asilimia mia moja! *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana! Waheshimiwa Wabunge, muda uliosalia hautoshi tena kumwita yeyote kuchangia. Wakati wa jioni kuanzia saa 11.00 wapo wachangiaji 11. Kwa hiyo, itatosha tu kufikia muda wa kawaida na baadae nitawataja.

Naomba nikumbushe tu, kesho asubuhi, Waheshimiwa Mawaziri watajibu hoja na baada ya hapo, tutapiga kura kupitisha Bajeti ya nchi.

Kwa mujibu wa Kanuni ya 79(1), kura hizi ni za jina kwa jina *(Roll Call Vote)*. Kwa hiyo, nawasihi Waheshimiwa Wabunge mliopo na wale ambao wananisikia popote walipo kwamba kesho ni muhimu sana kwa sababu tutaitwa jina kwa jina, ila Spika tu, kwa sababu yeye atasubiri kama kura zitafungana, basi yeye ana kura ya turufu. Wengine wote wataitwa kwa jina hadi mwisho. *(Makofi)*

Leo jioni, tutaanza na Mheshimiwa Bernadeta Mushashu, atafuatiwa na Mheshimiwa Bujiku Sakila, atafuata pia Mheshimiwa Khadija Ally Al-Qassmy, Mheshimiwa Ruth Msafiri, Mheshimiwa Mwanne Mchemba, Mheshimiwa John P. Lwanji, Mheshimiwa Mwadini Abbas Jecha, Mheshimiwa Mwanawetu Said Zarafi na tutahitimisha na Mheshimiwa Profesa Jumanne Maghembe. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, inawezekana nisiwepo tena mezani jioni. Hii ni kwa sababu ofisini kwangu kumekuwa na msiba. Msadizi wangu wa karibu Bwana Christopher Ndallu amefiwa na binti yake wa umri wa miaka 22. Alasiri nitakwenda Dodoma Vijijini kwa mazishi. Kwa hiyo, msiponiona siyo kwamba tena nawaachia achia tu wanawake, lakini ni kwamba imebidi niondoke kwa shughuli hiyo ya kusikitisha.

Baada ya matangazo hayo nasitisha shughuli za Bunge hadi hapo saaa 11.00 jioni.

*(Saa 7.00 mchana Bunge lilisitishwa hadi saa 11.00 jioni)*

*(Saa 11.00 jioni Bunge lilirudia)*

*Hapa Naibu Spika (Mhe. Anne S. Makinda) Alikalia Kiti*

**NAIBU SPIKA:** Tuendelee Katibu.

## HOJA ZA SERIKALI

### Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2007/2008 na Hali ya Uchumi wa Taifa kwa Mwaka 2006 na Mwelekeo wa Mpango wa Maendeleo kwa mwaka 2007/2008

*(Majadiliano Yanaendelea)*

**MHE. BERNADETA K. MUSHASHU:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili na mimi niweze kuchangia kwenye hoja ya hotuba mbili zilizo mbele yetu. Nianze kwa kuwashukuru watoa hotuba mbili zilizo mbele yetu. Nianze kwa kuwashukuru Waheshimiwa Mawaziri wawili wa Wizara zote mbili, Manaibu Waziri, Makatibu Wakuu wa Wizara zote mbili, Wakurugenzi na Watendaji kwa kuandaa hotuba ambazo zimeandaliwa kitaalamu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiangalia malengo na Bajeti yenyewe vyote vinazingatia malengo ya milenia, malengo ya MKUKUTA na vile vile hizi hotuba zote mbili zimezingatia maeneo mbalimbali yaliyoainishwa kwenye Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2005. Hivyo itoshe kwamba mimi kusema kwamba Bajeti zenyewe ni nzuri. Tunachofanya hapa ni kujaribu kuchangia kwenye maeneo mbalimbali kusudi tuweze kuboresha na hizi Bajeti ili iweze kuwanufaisha watu wengi na *may be* hata kuweka mikakati mizuri kwa ajili ya Bajeti ijayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kuyasema hayo, tunaelewa wote kwamba zaidi ya asilimia 80 ya wakazi wa vijijini ni wakulima na wengi wa hao wakulima ni maskini. Kwa sababu wanaendelea kulima kwa kutumia jembe la mkono na kwa kutumia zana zilizo duni. Tanzania haiwezi kuendelea kama tutawaacha nyuma hao. Mimi napenda nipongeze Serikali kwa kutambua kwamba kilimo ni kipaumbele na kueleza hivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini ukiangalia Bajeti iliyopangwa kwa upande wa kilimo ambayo ni shilingi bilioni 379.5 sawa sawa na asilimia 6.2 ya Bajeti haitoshi kuweza kuleta mapinduzi ndani ya kilimo na kutofanya hivyo hicho kilimo hakiwezi kutusaidia wala hakiwezi kuendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilichokuwa napendekeza kwa Serikali ni kwamba sasa wakati umefika Serikali ingetafuta fedha nyingi kama tulivyofanya kwenye elimu, kuwe na mikakati kabambe ya kuweza kuleta mapinduzi kwenye kilimo, watu walime kwa kutumia matrekta, walime kwa kutumia majembe ya mikono kusudi waache kuwa na heka kamoja, mtu aweze kulima mpaka *ten, twenty hectors of land,* hapo kweli tutaweza kubadilisha hali ya maisha ya watu wengi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa nafikiria kwamba sasa wakati umefika kwamba labda Serikali ifikirie kuainisha maeneo na labda yaitwe *special agricultural zones* wa-*invest* na watu mbalimbali waweze ku-*invest,* kuwekwe na miundombinu mbalimbali, waweke mashine kubwa kubwa, kusudi tuweze kulima *at a large scale.* Nina uhakika tukifanya hivyo tunaweza tukapata chakula cha kutosha, tunaweza tukapata mazao mengi ya *export* wetu utakuwa na tutakuwa tumeboresha maisha ya Watanzania walio wengi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, najua na vile vile naipongeza Serikali kwa vile vile kuainisha miundombinu kama kipaumbele kwa kuipatia asilimia 12.8 ya Bajeti na wote tunakubaliana hivyo kwamba kama miundombinu itaboreshwa basi biashara na zenyewe zitakuwa, kilimo kitakuwa kimeboreshwa na wawekezaji watakuwa *attracted* kuja kufanya kazi Tanzania, kwa hiyo uchumi wetu utakuwa. *(Makofi)*

Tatizo moja ambalo nimeliona pale, nafikiri wame-*concentrate* sana kwa upande wa barabara, wakasahau miundombinu na mawasiliano ndani ya maji. Lakini wote ni shahidi kila siku ajali mbalimbali zinatokea kwenye maji, mali za watu zinapotea kwenye maji na labda nizungumzie ajali kubwa zilizotokea. Tarehe 22 Aprili, 2006 *MV Nyamageni* ilizama kwenye Ziwa Victoria, wafanyakazi wote 11 wa meli hiyo, pamoja na wafanyabiashara wote waliokuwa wanasindikiza mali zao wakafariki.

Tarehe 21 Mei, 1999 nakumbuka kwamba *MV Bukoba* ilizama watu zaidi ya 1,000 walifariki kwa sababu ile meli ilikuwa ni mbovu na ilikuwa imezeeka, lakini vile vile hata wale waliookoka iliwabidi waelee kwenye maji zaidi ya saa 6 kwa sababu ilikuwa hakuna vifaa vya kuwaokoa. *(Makofi)*

Lakini *as if* hii haitoshi tarehe 11 Mei hadi tarehe 18 mei, 2007 *MV Fundi* ilipotea. Ilipotea kwa sababu kwenye Ziwa hakuna minara yenye taa ya kuongozea meli. *Speed boats* zikaletwa tukafurahi watu tunaokaa kwenye *Lake Zone* lakini kumbe zilikuwa mbovu. Sasa zimekuwa *grounded* kwa ajili ya kubadisha injini. Ipo *MV Serengeti* ambayo *basically* ni meli ya mizigo. *MV Victoria* ambayo inafanya kazi kwa sasa hivi ninawataarifu kwamba na yenyewe imekuwa *grounded* kwa ajili ya matengenezo makubwa. Inayo *capacity* kubwa ya kubeba watu zaidi ya 1,200 lakini ni meli ambayo imeanza kufanya kazi tangu mwaka 1961.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama unasafiri kutoka Bukoba kuja Mwanza unapofika katikati ya Ziwa, unakuta hakuna mawasiliano kabisa, hakuna mtandao wowote unaofanya kazi, hakuna redio, kwa hiyo, kama mkipata matatizo hakuna namna ya kuweza kujiokoa. Nilikuwa napendekeza kwamba basi wakati umefika Serikali ingefikiria kwenye Bajeti hii namna ya kuweka *becons* kwenye Ziwa, namna ya kuweza hiyo minara ya taa kusudi iweze kuongoza meli ziache kupotea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kama kuna uwezekano washawishiwe mawakala na Serikali itoe ruzuku kusudi vyombo vya kuokolea viweze kununuliwa kwa bei nafuu na ikiwezekana hata mtu akaweza kujinunulia *life jacket* basi anaposafiri anakuwa na *life jacket* yake. Katika Ziwa kubwa kama hilo kuna mitumbwi miwili tu ya uokoaji mmoja uko Bukoba na mwingine uko Mwanza. Ndiyo maana juzi juzi ilipozama boti walipokuwa wanasafiria Mheshimiwa Anthony Diallo, Mheshimiwa Maria Hewa, Mheshimiwa Ngeze, Mwenyekiti wa CCM wa Mkoa wa Kagera na wengine iliwabidi waendelee kuelea kwenye maji kwa zaidi ya saa mbili kwa sababu vyombo vya kuokolea havikuwepo, bahati nzuri wakaja kuokolewa na wavuvi ambao walikuwa na shughuli zao. *(Makofi)*

Kwa hiyo, tunachosema ni kwamba wakati umefika sasa hivi Serikali i-*invest* iweze kuweka hivyo vitu *in place* kuweza kuhakikisha kwamba usafiri upo salama ndani ya Ziwa Victoria. Lakini la muhimu ni kwamba nimetumwa na watu ninaowawakilisha wa Mkoa wa Kagera kwamba miaka 46 jamani meli iko majini, meli imechoka, wanaogopa isije ikaleta madhara zaidi, kwa hiyo, naomba kwamba waliangalie hilo na kwa kuboresha usafiri ndani ya meli nina uhakika kwamba Tanzania tutakuwa tumeifungua tuweze kufanya biashara na Uganda, Burundi na Rwanda na kwa kufanya hivyo uchumi wetu utakuwa umekua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nawapongeza Serikali kwa kutumiza ahadi ya Rais. Najua hivi siyo mbali mishahara ya wafanyakazi itapanda na viwango vya kodi kwenye kima cha chini kitakuwa kimepungua, nawapongeza sana. Lakini ninapendekeza kwamba mishahara hiyo ipandishwe kulingana na hali halisi ya maisha na hali halisi ya masoko. Nasema hivyo kwa nini, ukizingatia Mikoa ya pembezoni kama Kagera ni kwamba unakuta bei zipo juu sana na watu wanashindwa hata kumudu maisha yao. *(Makofi)*

Kwa mfano, Mkoa wa Kagera sasa hivi vyakula vyote bei zipo juu, mafuta hayo ndiyo usiseme, *cement* ipo kati ya shilingi17,000 na shilingi 20,000 kwa mfuko mmoja.

Ukiuliza wanasema Mikoa hiyo ipo mbali, sijui mbali na wapi? Hata Kiwanda cha *Kagera Sugar* ambacho kipo Kagera, bei ya sukari ni shilingi 1,200 mpaka shilingi 1,300 kwa mtu wa Dar es Salaam anapokuwa amepata mifuko 10 ya *cement* mtu wa Bukoba anakuwa amepata mifuko mingapi, anakuwa amepata mifuko mitano au sita.

Kwa hiyo, nilichokuwa naomba kwa Serikali ni kwamba sasa hivi waweke mfumo wa kuweza kudhibiti hizo bei kusudi angalau zilingane lingane katika Tanzania nzima, mbona kwa soda inawezekana. Bei ya soda karibu bei ni ile ile kwa Tanzania nzima, bei ya bia karibu ni ile ile kwa Tanzania nzima na bei ya sigara karibu ni ile ile kwa Tanzania nzima, tunashindwa nini kudhibiti na hivi vitu kusudi hata hiyo mikoa inayoitwa ya pembezoni ikaweza kunufaika kwa keki ya kuboresha maisha na kwa maslahi kwa wafanyakazi na kwa kufanya hivyo nina uhakika wale wafanyakazi ambao hawapendi kukaa mkoa wa Kagera labda moja inayowafukuza ni hali ya kwamba maisha yapo juu kwa kufanya hivyo basi watakuwa *attracted* kufanya kazi katika Mkoa wa Kagera. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mfuko wa uwezeshaji. Mfuko huu ulianza mwaka jana, maelfu na maelfu waliomba, wachache walipata mimi nafikiri ilikuwa ni nzuri, mfuko ndiyo ulikuwa unaanza na *the fact* kwamba watu waliomba wengi inaonyesha kwamba tunao Watanzania wengi ambao wana shughuli mbalimbali za kufanya lakini wanachohitaji ni mitaji. Kwa hiyo, ninachopendekeza hapa ni kwamba sasa pamoja na hela hizo kutolewa elimu ya ujasiriamali ilikuwa haijafika. Kwa hiyo, nilikuwa napendekeza kwenye Bajeti hii elimu ya ujasiriamali itolewe kwa kila mtu kusudi hizo hela waweze kuzitumia na kuweza kuzalisha, au kupandisha mitaji yao. Vile vile nilikuwa napendekeza, *SACCOS* tunajua kwamba ni vyama vya ushirika na najua sera ya Tanzania sasa hivi ni kuboresha vyama vya ushirika, ili kusudi kuziboresha basi zile *SACCOS* ambazo zimeshatengemaa wameonyesha historia nzuri ya wanachama wao kujiwekea akiba wao kukopa na kurejesha *on time* zile hela ziende moja kwa moja kwenye *SACCOS* kusudi hata zile asilimia 10 ziweze kubaki ndani ya *SACCOS* na waweze kufaidika wanachama ambao ni wananchi wa kawaida ambao tunawalenga.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa napendekeza kwamba fedha zilizo *CRDB* na *NMB* ziongezwe kusudi watu wengi zaidi waweze kupata. Lakini Serikali iendelee basi kufanya maongezi na hizi benki mbili kusudi waweze kupunguza riba, nafikiri inawezekana kwa sababu *NMB* wao sasa hivi wameshakubali pamoja na kwamba wanakopesha kwenye 10% lakini ni *on reducing balance.* *CRDB* bado, kwa hiyo, mtu wa *NMB at the end of the story* analipa zile hela na asilimia ambayo ni chini kidogo ya 10%.

Kwa hiyo, naomba Serikali basi waendelee kuzungumza na hizi benki kusudi tuweze kupata au kuwasaidia hawa watu wetu. Vile vile nilikuwa napendekeza kwamba sasa wakati umefika, ule mkondo wa pili wa *SCULT* pamoja na benki za wakulima na wenyewe ungepewa hela kusudi na wao wakaanza kufanya kazi. Tukitumia mikondo yote miwili tutaweza kuwafikia Watanzania wengi ambao ndiyo walengwa na kwa kufanya hivyo basi tutakuwa tumeboresha maisha kwa kila Mtanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. BUJIKU P. SAKILA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa kunipatia nafasi hii ili na mimi nichangie katika hotuba hizi muhimu kwa maendeleo ya nchi yetu. *(Makofi)*

Kwanza kabisa napenda nitumie fursa hii kutoa pole kwa wale waliopata maafa mbalimbali, ikiwamo pamoja na hii ajali ya Singida. Naomba roho za marehemu Mwenyezi Mungu aziweke mahali pema Peponi, *Amin.*

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla sijasahau, kwa niaba yangu mimi binafsi na kwa niaba ya wapigakura wa Jimbo la Kwimba naunga mkono hoja hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda nitumie fursa hii, kwanza kuwapa hongera sana Waheshimiwa Mawaziri wote wawili na wenzao walio chini yao katika kuandaa hotuba hizi katika kuandaa Bajeti na mipango hii. Bajeti hii uliotupatia ni misingi muhimu ya maendeleo ya nchi yetu. Inatuelekeza jinsi ya kujitegemea. Nawapa hongera sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuandaa Bajeti siyo kazi ndogo, kwa sababu unazungukwa na mazingira mengi sana, waandaji wa Bajeti hii walikuwa wanaangalia Ilani ya Uchaguzi ya CCM ambacho ni Chama Tawala, MKUKUTA, lakini vile vile walikuwa wanamwangalia Mbunge mmoja mmoja kwenye jimbo lake. Lakini vile vile hata na wenyewe walikuwa wanakuwa na *influence* wao wenyewe, kwa hiyo, siyo kazi ndogo sana. Kwa hiyo, mimi nawapongeza kwa kutuletea hizi hotuba. *(Makofi)*

Napenda nitumie fursa hii kuipongeza Serikali kwa kuweka elimu kuwa ya kwanza katika vipaumbele. Elimu inahitaji msaada mkubwa sana kutoka Serikalini, bila elimu kila mmoja ameshasema hapa, maendeleo yetu au hayatakuwepo kabisa au yataenda pole pole sana. Kwa kupewa kipaumbele elimu kwa imepatiwa shilingi trilioni moja ni jambo jema sana. Kwa mpangalio jinsi walivyoweka mimi nawapongeza sana. Naomba kwa upande wa elimu hata mwakani naomba sana elimu iwe ya kwanza, kwa sababu gani, katika maelekezo ya ujenzi wa shule za sekondari, tulikuwa tunasema kwamba wananchi wajenge madarasa, wananchi watajenga maabara, watajenga nyumba za walimu na watajenga majengo ya utawala.

Mheshimiwa Naibu Spika, siyo kazi ndogo, Serikali kwa upande wake italeta walimu, Serikali kwa upande wake italeta vifaa, hiyo siyo kazi ndogo sana. Mimi naomba tu hii trilioni moja iliyopewa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi kwa safari hii waitumie vizuri na waanze sasa kuangalia jinsi ya kuwasaidia wananchi hasa kwa upande wa ujenzi wa maabara na hosteli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nafahamu ni kazi kubwa sana. Hosteli kama walivyosema Waheshimiwa Wabunge wengi, zinahitajika sana kama watoto wetu, tunapenda wamalize vizuri katika shule zetu na wafike kwenye viwango tunavyovihitaji.

Kwa hiyo, Serikali ingeingilia kati kujaribu kusaidia angalau kidogo katika ujenzi wa hosteli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo lingine ambalo Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi inaweza kuingilia ni ujenzi wa maabara. Ujenzi wa maabara unahitaji gharama kubwa sana. Ni tofauti na ujenzi wa darasa tu, unajenga madarasa matatu, unaweka vifaa, gharama ya ujenzi wa maabara hauwezi kupungua shilingi milioni 80, kwanza siyo jambo dogo sana. Wananchi ukiwategemea watamaliza kazi hiyo peke yao inakuwa siyo rahisi sana. Ombi langu ndiyo maana nasema kwamba naomba sana elimu hata mwaka kesho basi kwa sababu hii hapa imeshapita. Inapopita tunaanza kuandaa Bajeti ya mwaka mwingine, waanze kufikiria tena kuiweka iwe namba moja ili shule zetu zikamilike. *(Makofi)*

*S*asa hivi shilingi trilioni moja inaweza kuonekana ni kubwa sana. Lakini kumbuka kwamba tumeongea juu ya walimu, lazima waajiriwe walimu wa kutosha katika shule hizo na kila shule hawapungui walimu 24, kama idadi inatakiwa kukamilika, kwa kujitosheleza kwa walimu na vifaa. Kwa hiyo, hata wakisimamia vizuri shilingi trilioni moja itatusaidia tu kutusogeza, haitatupeleka mbali sana. Kwa hiyo, mwakani tena wakiongezea itakuwa vizuri zaidi ili kuwapatia unafuu wenzetu wanaoandaa vijana wetu vizuri kwa ajili ya kutumikia Taifa hili. Napenda vile vile kwamba ni ombi, sekta au Wizara ya Miundombinu iendelee kuangaliwa. Tulipokuwa tunachangia uboreshaji wa Bajeti mwezi wa nne, kila mmoja aliyesimama alikuwa anaongea juu ya kuongezewa fedha Wizara ya Miundombinu. Naomba sana Wizara hii iweze kuendelea kupewa kipaumbele. Mimi ninavyofahamu kama tukifungua njia wananchi wetu watakuwa wamepungukiwa mambo mengi ya kulalamika. Wanahitaji kusafiri na wanahitaji kusafirisha mazao. Kwa hiyo, ndiyo maana hii Bajeti naiunga mkono kwa sababu wananchi wa Jimbo la Kwimba watanishangaa nikikataa wakati nahitaji barabara kutoka Mabukwe kwenda Malampaka hawatanielewa. *(Makofi)*

Nahitaji barabara ya kutoka Jojilo kwenda mpaka Magu. Kwa hiyo, kusema kwamba nitaipinga si vyema, ukweli hawatanielewa, kitu tunachojaribu kufanya hapa, fedha hii ipatikane namna gani. Waheshimiwa wengi wameongelea juu ya mafuta na mimi nakubaliana nao kwa kweli suala hili ni gumu sana. Najaribu kufikiria, watu wa sehemu za Luhala, Pizimba A, Pizimba B wasipoweza kupata mafuta, usiku utakuwa giza, tutarudi huko huko kwenye *black continent* kwa hiyo tunahitaji wawe na uwezo wa kununua mafuta. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nafahamu hawa Waheshimiwa Mawaziri wana nyumba yao, suala la mafuta limewagusa, wana wananchi wao, wanafahamu wengine ambao hawana uwezo, kama wakifiria sana na naamini kwamba wamekwisha pokea maombi ya Waheshimiwa Wabunge wengi, waangalie jinsi ya kurekebisha upande wa mafuta, mimi ninaongelea hasa mafuta ya taa. Kama wakiweza na kwenye dizeli na petroli sawa, ili mradi vile vipaumbele visiathiriwe maana yake tunaona kwamba vile vipaumbele ni muhimu sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho ninalotaka kuliongelea ni suala la Mji wa Mwanza, Mwanza ni Jiji, tangu litangazwe kuwa Jiji, kumekuwa na mabadiliko makubwa sana. Tunahitaji msaada, unahitaji kufunguliwa mapema na ndiyo maana tunasema kwamba barabara kutoka Kisesa kwenda Geita na kuendelea ikamilike mapema. *(Makofi)*

Tunajaribu kuokoa Mji wa Mwanza, samahani tunajaribu kuokoa Jiji la Mwanza ili lisije likabanana sana lifunguliwe mapema kabla mambo hayajawa magumu sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna Mheshimiwa mmoja hapa alitaka kulia hapa, hivi Serikali mnataka watu wangapi walie humu ndani? Mimi sina mpango wa kulia. Naomba kama ahadi ilitolewa kwamba pesa itatolewa basi pesa ile wajaribu kuangalia mahali pa kupatikana fedha hiyo ili ahadi hii ikamilike. Ningeiomba Serikali kila inapopanga vipaumbele vile ilivyopanga kwa Bajeti hii vizuri sana lakini vile vile hata kipaumbele cha ahadi za viongozi basi na yenyewe iwekwe pale, kuwe na ufuatiliaji wa ahadi hizo. Tukiziachia Wizara kukamilisha ahadi hizo wakati mwingine inakuwa ni mzigo mkubwa sana. Ni vizuri kila ahadi za vioingozi zikatengewa Bajeti yake, ili ziweze kukamilishwa ndani ya kipindi cha miaka mitano. Itakuwa si vyema sana hamtamtendea haki Rais, hamtamtendea kiongozi yeyote Serikalini kama itafikia wakati wa kipindi cha miaka mitano ahadi zake hazijakamilika. Ni vizuri ahadi hizo zikakamilishwa mapema. Naomba sana barabara ya kutoka Kisesa – Usagara - Geita na kuendelea likamilishwe mapema. *(Makofi)*

Kama nilivyosema naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. KHADIJA SALUM ALLY AL-QASSMY:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia leo hii nikaweza kusimama katika Bunge hili. *(Makofi)*

Pili napenda kukushukuru wewe kwa kunipa nafasi hii ili niweze kuchangia hoja hizi mbili zilizoko mbele yetu. Vile vile napenda kutoa pongezi zangu za dhati kwa hotuba mbili za Kambi ya Upinzani zilizosomwa na Waheshimiwa Viongozi wetu. Vile vile napenda kuungana na Wabunge wenzangu kwa kutoa rambirambi kwa wale majeruhi pamoja na waliopata msiba katika Mkoa wa Singida nasema wote poleni sana.

Kabla sijaendelea mimi yote ninayozungumza hapa nina maslahi nayo, lakini naweka mbele maslahi ya wananchi. Kwa kweli nitazungumzia suala ambalo limeshazungumzwa sana lakini nahisi lina umuhimu sana kulizungumza kwa sababu wananchi waliokuwa na kipato cha chini pamoja na hata sisi tuliokuwa tuko juu vile vile litatugusa sana nalo ni kuhusu habari ya mafuta. Mimi naomba mafuta yote yaondolewe ushuru kwa sababu yote leo tunahisi kama yamepanda kama Waheshimiwa Wabunge wenzangu walivyosema kwamba ni shilingi 4 au shilingi 20 au shilingi 22. Waheshimiwa hizi zitakuja kutu-*cost* kwa sababu watoto sasa hivi wanakwenda shule na tunawaona katika vyombo vya habari, matangazo kila siku yanatoka jinsi wanavyonyanyasika katika magari ya daladala na bado hatujawapatia usafiri mbadala. Kwa hiyo, mimi naomba hili

litazamwe kwa makini sana ili tuwaangalie wale watoto tuliowawekea 18% waweze kwenda shule bila ya kupata usumbufu wowote njiani. Mimi naomba yale maoni ya Kambi ya Upinzani ya kuangalia vyanzo vya mapato kama kwenye uvuvi na maliasili basi viangaliwe kwa kina zaidi ili suala hili likiondolewa lisiweze likatuyumbisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja ya pili naomba kuchangia katika bandari na *TRA*. Mimi kwa maoni yangu nahisi *TISCAN* haifai kuwepo kwa sababu ni usumbufu sana na wananchi wengi wanasumbuka na kitengo hiki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, *TISCAN* unapotoka na mzigo ukaleta *documents* zako ukazipeleka pale zinaweza zikachukua wiki mbili au tatu. Sasa la kusikitisha hapo ni kwamba, wao wanakuwa siyo waamuzi wa mwisho. Karatasi zile ni lazima uzipeleke tena *TRA* au *Long room* ili ziweze kwenda kutiliwa bei nyingine. Kwa hiyo, kwa maoni yangu sioni sababu ya wale *TISCAN* kubakia pale, kwani *TRA* wanaweza kuifanya kazi hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili ambalo linawasumbua sana wananchi pamoja na wafanyabishara ni kwamba naomba Mheshimiwa Waziri atueleweshe jinsi gani unaponunua gari Japan au ukanunua gari Dubai tuseme mathalani la dola 800 kama balloon, saloon na isiyozidi dola 1200 ukapandishiwa ikaongezwa kiwango na ikafikia 2800. Vilevile ukatiliwa *freight* ambayo ile gari ukaingiza kwenye *container* katika *container* la *20 feet* lina *CBM 28* sasa gari lile linakuwa na *CBM 10.5* mpaka *CBM 10.6* na bei ya *CBM 1 k*wa nchi za wenzetu ni dola 85 mpaka 80. Sasa hii dola 1100 mpaka 1200 inakuwa inapatikana wapi?

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, utaona wafanyabiashara wengi wanakimbilia nchi jirani na mlundikano sana wa mizigo bandarini ni kutokana kwanza na bei kubwa ambazo mtu akiwa mfanyabiashara tayari anajipangia kwamba gari hii nimeinunua dola 800, kwa hiyo ushuru wake utakuwa hivi kwa sababu watu wote siku hizi wanajua nini wanafanya. Lakini hivyo sivyo, wakifika hapa gari hiyo inawekwa dola 2800 na unatiliwa na *freight* kubwa kiasi kwamba bei ile inakuwa kubwa sana. Kwa hiyo, kutokana na hilo, naomba ili kuongeza biashara nafikiri biashara ukiiweka kidogo jinsi na wenzetu wanavyokwenda, basi ndiyo pale utakapopata wateja wengi ikiwa utafanya kitu gharama kubwa, basi uhakikishe kwamba wateja wote unawafukuza. Kwa hiyo, kutokana na hilo namwomba Mheshimiwa Waziri aliangalie sana jambo hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ni kwamba kwa maoni yangu sikubaliani kabisa na mpango wa *fast truck*, *green channel* na *re-channel.* Nina sababu za msingi.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hivi ukienda bandarini una *container* la *gypsum board* ambayo inaingia katika *40 feet* inaingia karibu 20,000 *pieces* na *market* yake Sh. 14,000/= mpaka 13,000/= katika Mitaa. Lakini *container* lile utalikuta linatolewa kwa Sh. 4,500,000/= tu wakati gari la shilingi milioni sita linatolewa kwa bei zinalingana na hizo, maana yake ni Sh. 3,500,000/= au Sh. 3,800,000/=. Sasa hapo, yaani hatujaanza hiyo,

tayari uwiano umeshaanza kuwa tofauti na hiyo pamoja na kwamba wafanyabiashara wa Kichina wanapewa *priority.* Kwa sababu walete, lakini wao ni wawekezaji na mizigo ile wanaileta katika Soko la Kariakoo wanashindana na wananchi katika ushindani wa kibiashara.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa ikiwa wao wanafanyiwa bei ndogo na wananchi wanapata kwa bei kubwa, kwa hiyo uwiano wa kibiashara utakuwa wananchi wa Tanzania wataweza kukandamizwa. Kwa hiyo, mimi ninavyohisi kwa maoni yangu, hiyo itazidi kuwadhalilisha wananchi wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa naingia katika Bandari ya Dar es Salaam na ya Zanzibar. Ni masikitiko makubwa kwamba Zanzibar ni sehemu ya pili ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania lakini kuna usumbufu mkubwa kwa wafanyabiashara na usumbufu wenyewe sisi Bandari ya Zanzibar ni mbovu, haiwezi ikaenda meli kubwa, meli zote kubwa za makontena zinashukia Dar es Salaam na magari mengi karibu asilimia 11.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa kutokana na hilo, pale gari zinakuwa *on transit,* ukitaka kuisafirisha gari inayokwenda upande wa pili wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania unakuta ni lazima uandike barua ya kuomba kibali ambacho kinaweza kikachukua wiki mbili, ikawa kunaandikwa *storage* kubwa kwa sababu watu wanapewa siku saba tu, kwa hiyo, inapoandikwa *storage* ina maana ukilipa pesa zile unamtengenezea *ticks* Mapato wakati hayana sababu na wenzetu wanaopitisha pale *on transit* kwenda Malawi, Burundi na Uganda, wao wanaondosha gari zao pale bila hata barua yoyote ile. Kwa hiyo, hili naomba liangaliwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, *TRA* pamoja na wafanyabiashara wa Zanzibar walikuwa na maazimio katika Hoteli ya Masanzi siku ya tarehe 27Julai, 2006 na maazimio yenyewe niko nayo hapa.

Kwa hiyo, katika hayo ambayo wamekubaliana yamekubalika machache sana na wameahidi mengine watayatazama lakini mpaka leo hii tunaona bado wanasuasua sijui kigugumizi cha nini wakati hii ni nchi moja na sote ni raia wa Tanzania na tunahitaji kupata huduma kwa pamoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama mnavyojua, Zanzibar ni kisiwa kidogo chenye watu milioni moja tu na uchumi wetu unategemea biashara pamoja na utalii na watu wake wengi wanawake pamoja na wanaume, basi wote wanategemea biashara na kama mnavyojua Zanzibar watu wanazaa sana, mtu mmoja familia yake ina watu wasiopungua 10 na wote wanategemea biashara hiyo ili iweze kuwaendesha. Kwa hiyo, ombi langu kwa Serikali ya Jamhuri najua ni sikivu ituonee huruma ili tuwekewe pale *Zanzibar Free Port* ili tuweze kufanya biashara vizuri. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana na wewe kwa kuzungumza. Mheshimiwa Ruth B. Msafiri, atafuatiwa na Mheshimiwa Mwanne Ismaily Mchemba na Mheshimiwa John Paul Lwanji ajiandae.

**MHE. RUTH B. MSAFIRI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia katika hoja hii.

Naomba nianze kwanza kwa kuwapongeza watoa mada wote kwa jinsi walivyowasilisha hoja zao katika Bunge hili Tukufu.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda nitoe salamu za pole kwa ajili ya wenzetu waliopata ajali mbaya ya kuanguka na hata kuungua Mkoani Singida wakiwa katika basi la *Mohamed Trans* kuelekea Mwanza. Napenda nitoe salam rasmi kwa famili ya Mzee Mrisho Kiwanuka ambaye amepoteza mtoto wake katika ajali, naye aliungua mpaka akawa majivu. Mwenyezi Mungu azilaze roho za Marehemu wote mahali pema Peponi, Amen. Wale ambao ni majeruhi wapate nafuu haraka.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba baada ya kusema hayo niwasilishe salamu za wananchi wa Jimbo la Muleba Kaskazini ambao waliposikia hotuba hizi kusomwa, wapo waliokuja na pongezi zao. Naomba nianze na hizo na mimi naungana nao moja kwa moja kwamba Serikali ipokee pongezi kubwa sana kwa uamuzi wa kutenga asilimia 18 kwa ajili ya elimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na sera nzuri za Chama cha Mapinduzi, Jimbo la Muleba Kaskazini mwaka 2000 lilikuwa na shule moja ya Sekondari ya Serikali. Tunavyozungumza leo hii zipo shule 11 za Sekondari za Kata. Kwa hali hiyo, ni kwamba zimejengwa shule 10 katika kipindi hiki cha miaka sita na kwa hiyo, hizi ni shule ambazo zimetokana na Ilani ya Chama cha Mapinduzi na nguvu za wananchi kwa kuitika na kuunga mkono. Kwa hali hiyo, kuongeza bajeti kufikia asilimia 18 itakuwa ni ukombozi mkubwa kwa wananchi wa Jimbo la Muleba Kaskazini kielimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, wananchi wa Muleba Kaskazini wanapongeza sana katika utaratibu huu wa Shule za Sekondari za Kata wameweza kupata ajira katika kujenga madarasa, wamejiongezea kipato cha familia na mtu mmoja mmoja na wamepata mahali pa kwenda kufanyia kazi kwa sababu maeneo mengi yalikuwa yakiendelea na bado yanaendelea na ujenzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ambacho tunaomba kiendelee ni kasi ya ujenzi. Shule zetu zilizoanzishwa zimeanzishwa zikiwa bado zina madarasa machache na kila mwaka madarasa yatakuwa yanaongezeka kwa sababu watoto wanapanda madarasa. Kwa hiyo, katika kipindi cha miaka minne inatakiwa angalau madarasa yasiyopungua nane ukiongezea mwelekeo wetu wa mikondo minne minne yanatakiwa madarasa 16. Kwa hali hiyo, ukiongeza na maabara tatu na nyumba za walimu, maktaba na kadhalika utakuta kwamba kazi hii ya ujenzi ni kazi ambayo itatuchukua muda mrefu na ni kazi endelevu na ya kudumu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hali hiyo, tunachokiomba, mimi na wenzangu wote ni kwamba kazi hiyo ni kazi endelevu na ni kazi ya kudumu. Kwa hali hiyo, tunachokiomba ninaongea na wenzangu wote kwamba pesa hizi zielekezwe kule ambako kumelengwa na wale ambao wanayo makusudi ya kusubiri pesa hizo ili wajiwekee katika mifuko yao na kumalizia miradi yao wajue siyo hizi wasubiri kutumia nguvu zao kupata mahitaji yao, lakini sio katika pesa za bajeti hii. Pesa za bajeti hii zitumike katika kujenga maabara.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi katika Jimbo langu, shule 10 ambazo tumeongeza ni shule moja tu. Namshukuru Rais wa Uganda aliyetujengea Shule ya Muhutwe kwa zawadi, ndio peke yake yenye maabara pamoja na iliyokuwepo mwaka 2000. Lakini shule zile zilizobaki hatuna maabara. Kwa hali hiyo, tunahitaji kuona maabara inakuwepo, nyumba za walimu zinakuwepo ili tuweze kukabili tatizo hili la upungufu wa walimu, lakini na kuhakikisha kwamba kila mtoto aliyefaulu kwenda Sekondari aweze kupata nafasi ya kujiunga na Sekondari.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ambalo linajitokeza ni watoto kuchaguliwa wakashindwa kwenda shule kwa sababu ya kukosa ada, walio wengi ni kutokana na hali mbaya za familia zao, yaani kuwa na uwezo mdogo.

Kwa hali hiyo, ninaomba katika ule mchango, ule mpango wa Serikali kusaidia wanafunzi wasiojiweza usimalizikie tu kwa wale wanaokwenda chaguo la kwanza, hapana. Mpango huu ufahamu kuna wanaokwenda chaguo la kwanza, lakini kuna wale ambao wanasubiri baada ya chaguo la kwanza, wanakwenda chaguo la pili na hata la tatu kwa sababu ya kuona kwamba zile nafasi hazikujazwa. Hawa wanapokuja kuchaguliwa wanakuta tayari ule mpango wa kuwasaidia umekwisha wanapata tatizo la kukosa masomo. Kwa hiyo, kuwe na asilimia fulani ambayo itabaki kusubiri machaguo mengine yanayofuata ili watoto wote wanaochaguliwa waweze kwenda Sekondari.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini lingine ambalo mimi nilikuwa naliwaza ni kwamba, hizi shule za Kata zimejengwa na wananchi kwa nguvu yao. Nilichokuwa nafikiri sana kwamba tuone uwezekano wa kipindi hiki kuwaondolea Sh. 20,000/= ya ada kusudi hawa wazazi badala ya ada ile Sh. 20,000/= ya mwaka wapate kuwapa watoto wao uji shuleni, na mlo wa mchana kwa sababu watoto wanaondoka nyumbani saa 11:00 alfajiri wanarudi nyumbani saa 12:00 jioni hawakupata uji, chakula cha mchana na kwa maana nyingine hata ule uwezo wao wa kuelewa na kufuatilia masomo kwa kweli kwa namna fulani hautaweza ukakaa vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, nafikiria katika bajeti ijayo, Serikali ije na mpango wa kuona kwamba ada hii ya Sh. 20,000/= iondolewe kwa shule za Kata ili wazazi waingize katika gharama za kugharamia watoto wao na kuhakikisha kwamba watoto wote wanapata chakula cha mchana na huduma hizi za uji wanapokuwa shuleni.

Mheshimiwa Naibu Spika, pongezi nyingine zimetolewa na walimu pamoja na wafanyakazi wa Jimbo la Muleba Kaskazini kupungua kwa kodi ya ajira kutoka asilimia 18.5 hadi asilimia 15 kwao ni ukombozi kwa sababu kabla bajeti haijasomwa walishaleta

malalamiko kwamba hili niliwasilishe katika Bunge lako Tukufu ili liweze kujadiliwa. Kwa hiyo, walipopokea taarifa hii walipongeza moja kwa moja na mimi naziwasilisha kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Muleba Kaskazini ambao ni wafanyakazi wakiongozwa na Mwalimu Vedasto Mkimala na Mkuu wa Shule ya Katoke "B" Shule ya Msingi.

Mheshimiwa Naibu Spika, yale ambayo pengine niseme wananchi wamependa Bunge hili liyafikirie, la kwanza kabisa ni lile la tozo ya viwango vipya vya ada za magari kutoka Sh. 20,000/= kwenda katika viwango vya Sh. 80,000/=, Sh. 230,000/= na Sh. 100,000/=. Kwa kweli hivi vimewatisha sana. Mimi naungana na wenzangu kwamba hizi ada zisitozwe kwa kuangalia CC za magari.

Mheshimiwa Naibu Spika, haya magari mpaka yenye CC 2500 ni magari madogo na ni magari ambayo Watanzania sasa hivi ama kapata mkopo tena ni magari *used*, mwananchi alikuwa anafanya kazi akapata hela zake kidogo, wameuza magari ya ofisi aka-*tender* na yeye wakamkubalia akatoa kidogo kidogo. Huyu ni mkulima, ameuza mazao yake kidogo, huyu ni mfugaji wa Tanzania kauza mifugo yake. Sasa ni vizuri kuangalia kwamba haya magari isiwe ni adhabu na sio kipindi cha kuendelea kufikiria kwamba magari ni vyombo vya starehe, hapana. Magari siyo chombo cha starehe, ni chombo ambacho kinaisaidia familia katika shughuli ndogo ndogo za kifamilia, kama zipo zile kubwa za biashara sasa hilo ni suala lingine ambalo naomba Serikali iliangalie.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashauri sana kwamba hiki kiwango cha Sh. 20,000/= mpaka Sh. 230,000/= kingetazamwa pengine kikaweza kuwa kimoja kwa kutazama CC za mwanzo. Halafu kile cha Sh. 230,000/= kitazame upya magari ambayo kweli ni mazito na kwa kweli naweza kusema ni magari ya watu wenye uwezo kwa sababu *VX* na *GX* na kadhalika nafikiri ni magari ambayo yana *status* nyingine tofauti kabisa ambayo isimwingize huyu ambaye ni mkulima na mfanyakazi mwenye kipato chake kidogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ambalo mimi napenda niliseme ni hili la mafuta ya taa ambalo wenzangu wameliunga mkono. Lakini naiomba Serikali iondoe ongezeko kwenye mafuta ya taa na matatizo ya wafanyabiashara yaangaliwe kama ni matatizo ya wafanyabiashara na kudhibiti mwenendo wao katika kuchanganya mafuta kwani yanaharibu hata *engine* za magari. Wanatakiwa washitakiwe. Yule ambaye anaweza akajenga kesi nzuri atasaidia sana kuliko kuwaadhibu wakulima ambao hata magari hawana wanategemea tu wao wapande magari yaliyokwisha nunuliwa na wengine.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi ninachotaka kuomba sana ni kwamba Serikali idhitibiti habari ya ongezeko kidogo iliyoongezeka kwenye petrol na diesel. Hili sio ongezeko kubwa la kutisha lakini tulipofika Dodoma kwenye kituo cha *petrol* mafuta yalikuwa Sh.1,360/= leo hii mafuta ni Sh.1,380/= sasa sijui, mwingine anasema ni Sh.1,390/= lakini mimi nimeona ni Sh.1,380/=, sasa sijui tutakapofikia tarehe 01 Julai itakuwa ni shilingi ngapi! Mimi nashauri sana, hapa ni mahali ambapo Serikali iangalie

sana katika vituo, wauza mafuta wasipandishe holela holela kama wanavyopenda wao. Ongezeko la shilingi mia lisijekuwa sasa ni maradufu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla ya ongezeko hili, Kagera nilipoondoka tulikuwa tunanunua lita moja ya mafuta Bukoba Mjini Sh. 1,600/=, sasa sijui sasa hivi itakuwa ni shilingi ngapi. Katika visiwa napo ilikuwa ni karibu na Sh.1,900/=. Kwa hiyo, ni vizuri kuangalia hili ongezeko lisitishe.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa wafanyabiashara ya usafirishaji na wenyewe nauli ziangaliwe kusudi isije kuwa ni kutoza gharama ambazo zinatisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilipenda nichangie na suala moja linalohusu miundombinu katika Mkoa wa Kagera. Mkoa wa Kagera ni mkoa ambao uko mpakani na ni mkoa ambao kwa yeyote anayependa kwenda Kagera ni lazima aipange safari, sio mahali mtu anaweza akasema anataka kwenda Dodoma, nitapita Morogoro na Pwani kwa sababu ni njiani, ni lazima ahakikishe amepanga safari ya Mkoa wa Kagera.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala zima la usafiri wa meli linatisha. Kwa sasa hivi Serengeti yenye uwezo wa kubeba abiria 400 ndiyo imekuwa badala ya *Victoria* yenye uwezo wa kubeba abiria 1,200 na mizigo ya tani 1,000.

Mheshimiwa Naibu Spika, unaweza kuona ugumu uliopo huu na hivi ndiyo imekuwa kwa kipindi kirefu tangu Mv. Bukoba ilivyozama, ikaja Mv. Mageni iliyokuwa inafanya shughuli zake, *anyway* ilikuwa inapita lakini ilikuwa inabeba abiria, tatizo linapungua kidogo. Sasa hali hii imeendelea kuwa ni tatizo mpaka hivi tunavyozungumza. Hivi tunavyozungumza leo, hakuna usafiri wa meli, kwa hiyo wananchi hawasafiri kwa njia ya meli kuja Mwanza wala kutoka Mwanza kwenda Bukoba na kubeba mizigo yao kwa gharama nafuu kwa sababu usafiri wa meli licha ya kubeba watu wengi kwa wakati mmoja lakini pia gharama za usafiri na usafirishaji ziko nafuu sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba Serikali ifikie mahali hili suala linekane ni la kushughulikiwa kwa umuhimu wa kipekee kwa sababu *population* kubwa iliyopo Kanda ya Ziwa inategemea sana usafiri wa ziwa ndani ya Ziwa Victoria. Zamani meli hizi zilikuwa zinatumika hata kwenda Uganda na hata Kenya lakini kwa sasa hivi usafiri huo una matatizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, njoo katika barabara, mkandarasi aliyepo ambaye anatakiwa atujengee barabara ya lami kutoka Kagoma kwenda Rusahunga mpaka sasa hivi hana hata nusu ya kilomita ambapo ameweza kuweka lami, mimi sijui anaendelea au lah! Anatuambia ataijenga hiyo lami lini?

Mheshimiwa Naibu Spika, njoo katika kiwanja cha ndege cha Bukoba. Tumeomba sana na tukaahidiwa kwamba kiwanja hicho kimetengenezwa, hakikuongezwa hata inchi moja, isipokuwa ambacho sisi tulikuwa tumekiomba, tuliomba kihamishwe, lakini tukaambiwa kwamba hakitahamishwa, badala yake kitapanuliwa.

Siku mimi nasafiri kuja Bungeni hapa, ilibidi nikae pale saa 13 kusubiri usafiri kwa sababu ndege iliharibika mvua zikinyesha hakuna usafiri.

Mheshimiwa Naibu Spika, ikisha kuwa jioni saa 12 hakuna ndege inayotua wala kuruka. Hali hii sisi inatusononesha kwa namna fulani. Tunaomba kwamba Serikali iangalie haya kwa sababu tutaendelea kupata shida hizi mpaka lini? Kila bajeti tulie? Kila bajeti tupige magoti tuombe? Tunaomba katika bajeti inayokuja ije na mpango rasmi wa kuona kwamba tunapata ufumbuzi wa usafiri katika Mkoa wa Kagera.

Mheshimiwa Naibu Spika, kitu kingine ninachoomba ni Kahawa. Kilimo cha buni maana yake siyo Kahawa, ni kilimo cha Buni. Kilimo cha buni kiboreshwe ili tuanze kusafirisha Kahawa badala ya kusafirisha buni. Buni ni mbegu na Kahawa ni zao, tusafirishe zao, tusafirishe *product* ya Kahawa iliyokwishatengenezwa tayari. Kwa hiyo, ninaomba kwamba uwezekano basi wa kupata namna ya kuboresha kiwanda chetu cha *BUKOP* au kutusaidia tuweze kuona kwamba tunaweza kutengeneza Kahawa, tu–*process* Kahawa itoke kwenye buni iwe ni Kahawa ili tuweze kupata pesa za kutosha kwa ajili ya wakulima. Hii inaendelea kushusha bei ya kahawa kwa wakulima wa Mkoa wa Kagera na imeshusha hata uzalishaji wenyewe wa Kahawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho, ninalopenda kulizungumza ni kwamba tumekubaliana kwamba bajeti hii ni ngumu yenye kulenga kuleta maendeleo kwa wananchi, yenye kufundisha kujitegemea kutekeleza kujitegemea. Watenda kazi waliopo ndani ya Serikali wanaopata mafungu wahakikishe kwamba wameyasimamia ipasavyo, *LAAC* na *PAC* kazi yao ni kukagua matumizi ya pesa hizi sasa adhabu zitolewe kwa aliyetumia pesa vibaya siyo kwenye Halmashauri iliyopata hati chafu kwenda kuendelea kuumiza wananchi ambao wanategemea pesa hizi ziwainue kimiradi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama ni kushushwa vyeo na kama ni kuondolewa kazini ifanyike lakini si kwa kuwanyima fedha za maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo napenda niseme naunga mkono hoja hii. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. MWANNE ISMAILY MCHEMBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ili na mimi niweze kuchangia hoja iliyopo mbele yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote naomba ichukue nafasi hii kuwapongeza Mawaziri wote wawili Mheshimiwa Waziri wa Fedha Mama Zakia H. Meghji na Waziri wa Mipango, Uchumi na Uwezeshaji Mheshimiwa Alhaji Dr. Juma Ngasongwa.

Naomba niwapongeza pia Manaibu Waziri wote wa Wizara zore mbili, Makatibu wote wa Wizara na watendaji wote wa Wizara zote mbili kwa hotuba yao nzuri waliyoiwasilisha hapa mbele yetu yenye mwelekeo wa kuleta maendeleo katika nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, niichukue nafasi hii pia kutoa pole kwa ajali iliyotokea hivi karibuni katika Mkoa wa Singida. Wengine wameumia na wengine wamefariki lakini wote niwaombee Mwenyezi Mungu kwa wale waliopoteza maisha awaweke mahali pema peponi na wale ambao bado wanaumwa, basi awape nafuu wapone haraka.

Nichukue nafasi hii kumpa hongera nyingi sana Mheshimiwa Mkuu wa Mkoa wa Singida kwa kazi nzuri aliyoifanya kwa kuwahi kwenye tukio pamoja na Wabunge wa maeneo hayo, nawapongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue nafasi hii pia nisije nikasahau, maana nakwenda kidogo kidogo mwisho nitapanda zaidi niunge mkono hoja iliyo mbele yetu asilimia mia kwa mia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi mwenyewe binafsi nilikuwa nimeamua kuchangia hotuba ya Waziri Mkuu, lakini kwa jinsi ulivyokuwa umetuhamasisha kwamba nafasi ile haitatosha, inawezekana wengine wakakosa, nikafuata ushauri wako, nikaamua leo nichangie mbele yako na mbele ya Waziri ili zile salamu ziweze kumfikia. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Yupo hapa anasikiliza kwa makini!

**MHE. MWANNE ISMAILY MCHEMBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kwa bahati nzuri Waziri Mkuu anaelewa tatizo ambalo linatukera sisi watu wa Tabora. Naomba nichangie moja kwa moja kuhusu miundombinu, hiyo ndiyo kero. Mheshimiwa Waziri Mkuu mwaka jana kwanza nitangulie kuomba radhi nitakutumia sana, lakini naomba radhi imebidi niseme hayo ambayo nataka kusema kutoka kichwani kwangu.

Mheshimiwa Waziri Mkuu wakati wa Bajeti mwaka jana Mheshimiwa Lucas Lumambo Selelii alipokuwa anachangia kwenye Wizara ya Miumbombinu ikaleta utata mkubwa sana, watu wawili walijitokeza. Waziri Mkuu aliomba akasema, bwana naliomba hili suala uliache nimelichukua. Mheshimiwa Spika akasema, mdogo wangu, ndugu yangu, hebu achana nalo hilo tutalifuatilia.

Mheshimiwa Naibu Spika, umeona, watu wawili hao! Kwa mtazamo huo nikajua kwamba Wizara ya Miundombinu, Wizara ya Uwekezaji na Mipango, Wizara ya Fedha pia imelipokea kwa sababu mkubwa akisema bwana ni lazima uogope. Kwa hiyo, nikajua kwamba wataliingiza hili safari hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kupitia vitabu hivi vyote nikianza na upande wa Mipango, Hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Mipango ambaye ndiye anaendesha nchi hii, hakuna alichokielezea, badala yake amezungumzia habari nzito ya kwamba kutakuwa na ukarabati wa barabara za Tabora na baadhi ya Mikoa ya wenzetu.

Lakini kilichotokea ni kwamba anachokarabati ni nini? Mwaka 2006/2007 hakukuwa na fedha za matengenezo ya aina yoyote kwenye bajeti ya vitabu siyo ya kwangu moyoni, hapana. Kwenye bajeti ndivyo ilivyokuwa ikisomeka, hakukuwa na

fedha iliyotengwa kwa ajili ya barabara ya Itigi - Tabora - Kigoma ndiyo iliyoleta utata. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini nilitegemea kwamba humu humu kwenye vitabu vya leo Serikali ingeeleza walichoweza kufanya na walichoshindwa. Mimi ninachofahamu ni kwamba walikuwa na tegemeo kubwa la fedha za nje ambazo nampongeza sana Mheshimiwa Rais, nampongeza Waziri wa Fedha na nampongeza Waziri wa Miundombinu aliyekuwepo. Walifuatilia sana suala hili upande wa *Kuwait Fund*, wakashindwa. Kama walishindwa kupata fedha za wafadhili walishindwa nini kuweka fedha za ndani ili angalau watengeneze barabara iweze kupitika kwa kipindi chote cha masika na kiangazi? Mimi siwalaumu, ndiyo maana natoa angalizo kwa sababu nilikuwa nafuatilia, nilimwuliza Waziri wa Miundombinu, nilimwuliza Waziri wa Mipango, Uchumi na Uwezeshaji, nilimwuliza Waziri wa Fedha, wakasema wanafuatilia, inawezekana mwaka huu wakafanikisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kwa sababu fedha hazikuwa kwao, sio lazima kutoa majibu sahihi, lakini basi hata hili! Mimi naomba nizungumzie sababu za msingi kuhusu hiyo barabara . Barabara ya kutoka Itigi kwenda Tabora mpaka Kigoma itafanya mambo mawili makubwa. Kwanza kabisa itasaidia kufungua masoko au njia kuu za uchumi baina na Tanzania na nchi jirani kupitia Tabora. Lakini pia itasaidia kufungua barabara za Mkoa hadi Mkoa kwa masoko yetu ya ndani, ndiyo sababu zake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kwa sasa hivi hiyo barabara haijatengewa fedha. Waziri wa Miundombinu akienda sasa hivi getini pale ataona magari makubwa yanavyokatisha kwenda njia ile kwenda Tabora. Ni zaidi ya magari 100. Kwa hiyo, wakitengeneza hiyo barabara bado watapata faida kubwa tu. Anaweza kuweka mashine ya mizania pale kwa yale magari, bado inaweza ikagharimia na kujilipa zile fedha zake na gharama za matengenezo ya barabara ile. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini isitoshe kuna barabara ambayo inatoka Tabora - Sikonge - Rungwa. Mheshimiwa Waziri Mkuu na Waziri wa Miundombinu ingewezekana siku moja wakapitia katika hizo barabara, wangejua tunazungumza nini. Tabora - Ipole - Sikonge hadi Rungwa ni sehemu ambayo watu wa Kitunda wako Kisiwani, hakuna barabara inayopitika kule, lakini inaitwa Mkoa wa Tabora.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ndiyo nilikuwa nataka kulizungumzia kwa uchungu kwamba hiyo barabara ya Rungwa ukiangalia kitabu cha maendeleo hakuna fedha za wafadhili, lakini fedha za ndani imetengewa shilingi milioni 300. Hivi milioni 300 unaweza ukatengeneza nini na zitasaidia nini. Sisi tunazungumzia kutengeneza barabara kwa kiwango cha lami. Naomba Serikali ielewe hatuzungumzi barabara ya lami uwezo wetu ni mdogo, lakini kuna barabara ya kutoka Ipole - Konga - Mpanda. Mimi ni Mbunge wa Viti Maalum, ndiyo mjue jinsi gani tunavyoweza kuzunguka kuyapata hayo kama Mbunge wa Viti Maalum Wanawake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunakwenda kuungana na Wabunge wenzetu tunawakuta kule. Hiyo barabara imetengewa milioni 400, lakini kilomita zake ni nyingi.

Sasa sijui itatengenezwa kwa kiwango cha lami au itatengenezwa kwa kiwango cha changarawe haijulikani fedha zake ni ndogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimezungumzia kwa uchungu kuhusu barabara. Lakini pia kuna barabara ya Tabora-Nzega ambayo inaunganisha Mwanza, hakuna fedha yoyote iliyotengwa na hakuna mategemeo.

Mheshimiwa Naibu Spika, niende moja kwa moja kwa sababu kengele ya kwanza imelia, sitaki kengele ya pili inigongee. Mwaka jana kiwanja cha ndege kilikuwa kimetengewa fedha kidogo. Ndege hazikuweza kutua kutokana na mvua za masika za mwaka jana zilivyokuwa kubwa. Naiomba Serikali iangalie jiografia ya Tabora na kiwanja cha ndege na nchi nyingine. Pale pana usalama wa kutosha, pana mali nyingi sana na pana jeshi kubwa sana. Hivi pakitokea vurugumechi sasa hivi tunafanye nini? Kwa kweli ni sehemu ambayo inahitaji kutengenezwa na kuboreshwa hasa sehemu muhimu kama hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nizungumzie suala nzima la afya. Vituo vya Afya vilivyojengwa kwa nguvu za wananchi kupitia *TASAF I* ni vingi sana kwa Mkoa wa Tabora. Lakini havijaanza kufanya kazi sasa hivi, naiomba Serikali iangalie suala zima la Vituo vya Afya vilivyojengwa na nguvu za wananchi ili wanapoingia kwenye awamu hii ya nchi nzima wafuatilie kwanza maeneo hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niende haraka haraka katika suala la mazingira na ufugaji. Tusipoangalia, Serikali ya Tanzania yenye uchungu mkubwa na watu wake tutaleta matabaka baina ya wakulima na wafugaji. Wafugaji wanapokwenda kwenye maeneo ambayo wametengewa wanafukuzwa na wakulima, tutakuwa na kizazi chenye chuki. Wanaosumbuka mle ni wanawake na watoto pamoja na watu wazima, wataona nchi yao inawanyanyasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ombi langu kwa Serikali wanakowapeleka hao wananchi wafugaji waangalie kuwapelekea madawa ya binadamu, kuwapelekea chakula, kwa sababu wanaachwa tu porini. Wanaambiwa nendeni huku na kule kuna mbung'o, njia zetu za ng'ombe hazijatengenezwa, wanapita tu mtu anakwenda anatokea kwenye mji wa watu. Mimi naomba liangaliwe sana hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho tuangalie hasara za hifadhi za mazingira, hao wenye ng'ombe wanaingia kwenye hifadhi jinsi ya kuwatoa ni tatizo, jinsi ya ufuatiliaji ni tatizo kwa sababu hatukujipanga. Tuliamua kuwaondoa kwenye maeneo nyeti, lakini hatukupanga maeneo ya kuwapeleka. Sasa haya ndiyo tuliyokuwanayo. Lakini bajeti ni nzuri, ninaiunga mkono kwa asilimia mia moja. Bajeti ni safi sana, ni bajeti ambayo mimi siwezi kukiuka miiko ya Chama cha Mapinduzi, ninaiunga mkono yote yaliyoandikwa. Upandaji wa bei ya vitu kwa Tanzania siyo kwa ajili ya bajeti hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hivi sukari kilo moja inauzwa Sh. 1,200/=, sasa hivi mfuko wa sementi unauzwa kwa bei mbaya, hivi ndiyo bajeti hii. Mimi naomba bajeti hii ishike uzi, bajeti hii iendane na jinsi matakwa ya Serikali tuliyoyakubali wakati

wa semina yetu hayo mambo yote yatekelezeke. Kitu kikubwa kwa Waheshimiwa Wabunge ni ufuatiliaji. Niwapongeze Mawaziri, kwa kweli wanafanya kazi nzuri sana kwenye Wizara zao na wanafanya kazi nzuri katika Serikali ya Awamu ya Nne kwa Ari Mpya, Nguvu Mpya na kwa Kasi Mpya. Uzi ni ule ule. Mimi siwezi kusema kufunga mkanda kwa sababu siyo sera ya Chama cha Mapinduzi kufunga mkanda. Kwa hiyo, mimi naomba nirekebishe na nizungumze, sisi hatusemi Mtanzania afunge mkanda, hatujazungumza wala hakuna hotuba yoyote iliyozungumzia ni matashi ya watu. Kwa hiyo, naomba lisibebwe kwamba ni kufunga mkanda kwa wananchi, hapana. Ni utekelezaji wa mipango na mambo ya nchi yetu ili yaende vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja. Ahsanteni sana. *(Makofi)*

**MHE. JOHN P. LWANJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia hoja hii. Nadhani pia nimpongeze jirani yangu aliyekaa sasa hivi kwa hotuba nzuri na kwa kweli ni jirani kwa sababu ameyasemea maeneo yangu pia.

Mheshimiwa Naibu Spika, niipongeze Serikali kwa kazi nzuri ambayo imefanywa kwa kipindi kilichopita. Bajeti hii nadhani ina *consolidate* hayo mafanikio. Juzi tumeipongeza Timu ya Taifa *Stars* kwa ushindi iliyoupata. Tuliipongeza siyo kwa sababu imefikia ile *ultimate* goli ya kwenda Ghana, hapana. Lakini kwa hatua iliyofikia tuliipongeza hapa. Ndiyo maana Serikali nayo tunaipongeza kwa hatua iliyofikia.

Mheshimiwa Naibu Spika, utakumbuka wakati Serikali inashika hatamu ilipitia kipindi kigumu cha ukame, hali ilikuwa mbaya sana, nadhani ilikuwa patashika pale kwenye Ukumbi wa Pius Msekwa. Hali ilikuwa mbaya, mifugo ilikuwa inakufa ovyo, chakula kilikuwa hakuna. Sasa nadhani ilibidi ijipange, tusisahau haraka sana. Lakini mafanikio ambayo yamepatikana katika kipindi kilichopita nadhani yanatuonyesha kwamba tunakwenda kwenye njia sahihi. Maana yake tumefanikiwa katika elimu, tumefanikiwa katika kuondoa hilo tatizo la njaa, tumepigana vizuri sana kwa tatizo la umeme na suala la *TRA* kila mmoja anajua mapato yameongezeka. Halafu pia na pato la Taifa pia limeongezeka na kama nilivyosema hapa hata kwenye nyanja zote na michezo nayo tume-*improve* tunakwenda vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, nadhani tusikate tamaa, tusonge mbele tuweze kupigana hii vita ya kumkomboa Mtanzania. Mimi sipendi kuzungumzia sana tatizo la mafuta, lakini wenye umri mkubwa ndiyo wanatambua matatizo ya mafuta na mwenendo mzima. Historia ya kupanda kwa bei ya mafuta inaeleweka. Mwaka 1967 wakati wamepigana vita Wayuhudi pamoja na Waarabu bidhaa ya mafuta ilikuja ikageuzwa ikawa silaha, siyo bidhaa tena. Upande mmoja uliposhindwa lakini ulikuwa na mafuta ukaamua kwamba wawaadhibu wale wote Mataifa ya Magharibi yaliyom-*suppor*t Muisrael, toka wakati ule mpaka leo bei ya mafuta imekuwa ni kitendawili. Sisi hatuna kauli juu ya bei ya soko la mafuta labda tupate kisima hapa nchini. Maana tunazungumza kana kwamba tuna visima vya mafuta, hatugawani vizuri au tunapandisha bei ya mafuta, hapana.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi ningeiomba Serikali ijaribu kuona uwezekano wa ku-*invest* katika *exploration* ya mafuta hapa. Tukiweza kupata mafuta labda tunaweza tukajinusuru kutokana na tatizo la kupanda kwa bei ya mafuta. Lazima tuelewe kwamba dunia iko vitani. Sasa hivi sisi siyo kisiwa, *Middle E*ast wanapigana, *Gulf* kuna vita, sasa bei ya mafuta itashuka namna gani katika Soko la Dunia ni *fluctuations!* Leo bei ya mafuta inashuka na kesho bei ya mafuta inapanda. Kwa hiyo, tusije tukaona kwamba sisi siyo sehemu ya dunia, sisi ni sehemu ya dunia na *as long* kuna vita hivyo, wenye mafuta hayo ndiyo wanaopigana na ndiyo wenye uamuzi juu ya suala hilo siyo sisi hata kidogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata Nigeria nao wamepata mafuta, lakini hawana amani, Angola tumesoma kwenye kitabu cha bajeti hapa wana mafuta, Mji wa Luanda pale wana kisima cha mafuta, lakini pato lao juzi juzi hapa limeanguka. Kwa hiyo, mimi nafikiri tuwe *serious* tuone tutakabiliana namna gani na hali hii tusikwepe matatizo, tuyakabili kama yalivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo langu linakuja, kwenye suala la kugawa kidogo tulichonacho. Hapa mimi ndipo ninapoona tatizo kwa muda mrefu nimekuwa nikiona kwamba kile kidogo tunachokipata katika kukigawa japokuwa hatuwezi kugawana sawa kwa sawa, lakini maeneo mengine naona kama vile yamesahaulika.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mkoa wa Singida ni Mkoa wa Tisa kwa ukubwa, una kilomita za mraba 49,000, *population* yake ni zaidi ya milioni moja na laki mbili au laki tatu. *Population density* ni watu 24 *per kilometre*, lakini tunazidi Mikoa mingi. Lakini sasa tunapokuja kugawana hayo mapato ndiyo tunakuta kuna Mikoa masikini ambayo inasahauliwa na inaendelea kuwa masikini.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa mfumo mzima wa bajeti na mfumo mzima wa kugawana ningeomba tuangalie Mikoa ambayo iko nyuma kimaendeleo ili tuweze kuisaidia ili iweze kuja mbele. Tatizo letu ni hilo.

Mheshimwia Naibu Spika, nasema hivyo kwa sababu tumeathirika. Wenzetu kuanzia mwaka 1970 Wilaya karibu 35 au 40 zimepatikana. Tumesema toka uhuru mpaka miaka ya 1970 mpaka sasa Wilaya mpya 35 zimegawanywa ukiacha Dar es Salaam na Manispaa. Lakini Mkoa wa Singida ni Mkoa pekee ambao Wilaya zake hazikugawanywa labda na Mkoa wa Kigoma. Kuhusu Lindi Wilaya mbili wamepata, Wilaya ya Ruangwa na Liwale na Mchinga iko njiani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini ninachozungumza hapa sasa hivi muda umefika kwa ajili ya Mkoa wa Singida kupata Wilaya mpya. Mimi Wilaya yangu ninayotoka ni *square* kilomita za mraba 28,000 ni mara mbili karibu ya Mkoa wenyewe. Sasa tunaendesha namna gani shughuli zetu? Dhana hiyo ya *D by D* itaendeshwa namna gani? Hiyo lazima itadumaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ningeomba sana kwamba Wilaya ya Manyoni na Wilaya za Mkoa wa Singida ziweze kupewa kipaumbele kama sisi tumeweza kusubiri

kwa miaka yote hiyo, basi wenzetu wasubiri, wenzetu wamefikia hata hatua ya kugawa Mikoa na hata sasa wanajadili kupata Mikoa mingine. Unapokuwa na Wilaya zinakuwa ndiyo *resources* zenyewe zinasogea kwa wananchi, rasilimali watu, rasilimali fedha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naiomba Serikali ije na mkakati wa makusudi kabisa wa kuweza kutusaidia. Nina *figures* zinazoonyesha kabisa kwamba kila Mkoa una Wilaya mpya ilizowahi kuzipata.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama Lindi nilivyosema, Ruangwa na Liwale zimepatikana katika kipindi cha miaka ya 1970 mpaka sasa na katika Mikoa yote mingine Wilaya zimepatikana.

Mheshimiwa Naibu Spika, ningeiomba sana Serikali iweze kuliangalia hilo itusaidie. Juzi Waziri Mkuu alitutembelea pale Itigi watu walimweleza wazi na yeye aliona hali halisi kwamba jamani sasa muda umefika tuweze kupata Wilaya. Kwa hiyo, ningeliomba suala hili liweze kuzingatiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikija tena katika kugawana kile kidogo tulichonacho kwa maana ya bajeti ya mwaka huu, Singida tumepata shilingi bilioni 38, yaani hata Mkoa wa Manyara ambao umeanza juzi unapewa shilingi bilioni 39, umetupita kwa bilioni moja. Sasa hao wanaopanga, wanapanga namna gani? Ndiyo hapo sasa inakuja ile dhana ya *managerial revolution,* watu wanakaa wachache wanapanga na wanafuata *tradition* kama Mkoa ulikuwa hivyo miaka ya nyuma, ndiyo hivyo hivyo, yule anayefika pale anaambiwa bwana ahaa, wewe bajeti yako *ceiling* yako ni hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa naomba hilo suala waliangalie angalau watusaidie ili tuweze kusonga mbele kwa pamoja. Katika Kasma hata ya barabara lile fungu 4200 Singida haikupangiwa, umepangiwa Mkoa wa Lindi, Mtwara, Ruvuma, Kigoma, Rukwa, Tabora. Huyo mtu alivyokuwa na mtazamo ni kwamba hiyo ni Mikoa maskini. Lakini nashindwa kuelewa kwa nini Ruvuma iko hapa badala ya Singida? Kwa sababu tukijilinganisha na Mkoa wa Ruvuma siyo maskini. Lakini sasa utakuta kuna Mkoa wa Ruvuma hapo, Mkoa wa Singida hakuna. Katika programu maalum ya maendeleo na ukarabati wa miundombinu Mikoa sita imetengwa, Lindi, Mtwara, Ruvuma, Kigoma, Rukwa na Tabora tena, Singida hakuna.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa mimi nadhani tungekuwa *fair,* barabara zetu ndiyo hizo, tungeomba sasa kwamba nchi iunganishwe na miundombinu mizuri. Hapa juzi Mheshimiwa Waziri Mkuu alikuja Manyoni na Singida wake wengine wametuweka katika mashaka wanasema labda barabara yetu itakamilika mwaka 2010. Sasa sisi tulitarajia kwamba nchi hii inaunganishwa mapema iwezekanavyo na mvua ndiyo hizo, watu wanavuna sasa, mwezi Septemba na mwezi Oktoba, mvua zinaanza tutakuwa na yale yale ya Kamenyanga na mambo mengine.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi ningeomba sana kwamba tuwe *serious,* tuunganishe nchi hii kwa barabara. Mkoa wa Singida unaonekana kama vile umesuswa,

uko katikati ya nchi, lakini sasa watu wanazungukia Nairobi kwenda katika Mikoa mingine wakati sehemu ya barabara isiyobaki kujengwa ni ndogo tu . Ningeiomba Serikali iweze kuliangalia hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu reli ya kati, sisi tunasubiri sana hatua ya Serikali na katika bajeti hii Serikali imezungumza kwamba imesaini Mkataba na Kampuni ya *RITES* ili iweze kuanza kazi. Ila sisi tunashangaa kwa nini mpaka mwezi Septemba, 2007? Sisi tulifikiri Kampuni hiyo ingeweza kuanza kazi hata mwezi Julai, 2007. Pamoja na kuishukuru Serikali, tungeomba huduma za reli zirejeshwe. Tulikuwa tunasafirisha mifuko kukboresha maisha ya wananchi lakini sasa tunaambiwa kwamba sisi Mkoa wa Singida ni masikini zaidi kuliko Mikoa mingine kwa sababu ya matatizo ambayo yamejitokeza. Tulikuwa tunasafirisha mifugo kila mara kwa reli, lakini huduma za reli sasa hakuna.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ningeomba sambamba na hilo kuna habari zisizothibitishwa kutoka Msumbiji kwamba hiyo Kampuni ya *RITES* haifanyi vizuri kule, inasuasua. Treni inasimama kwa ukosefu wa mafuta pamoja na vipuri. Sasa tunaiomba Serikali iweze kuangalia isije ikawa inachukua Kampuni mbovu. Ningewaomba sana wanaohusika waliangalie hilo tuletewe kitu ambacho kitafanya kazi kweli na hiyo kampuni iweze kutupatia reli ya kudumu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi mbali ya hilo, ningeomba kusisitiza suala la makandarasi. Tumeona bajeti imesema kwamba mwaka juzi makandarasi 2,900 wamepewa mafunzo ya kuwawezesha kutenda kazi zao. Hali halisi ya wakandarasi tulionao hapa nchini wengi ni wababaishaji, ni kweli kabisa.

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara zetu zinashindwa kutengenezwa vizuri kwa sababu makandarasi wengi hawana uwezo, makandarasi wengi hawana vifaa. Sasa pamoja na hili, sielewi wamefunzwa nini. Lakini kuna fedha zimetumika hapa kwa wakandarasi 2,900 imesema hivyo kwamba kuanzia mwaka 2000 mpaka sasa hivi wamefundishwa na wameitwa katika kozi mbalimbali kuweza kupewa mafunzo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ningeomba watumie hizo fedha vizuri. Kama kuna mafunzo mengine, basi liwepo na somo la maadili. Lakini sisemi kwamba siyo waaminifu, lakini liwepo somo la maadili ili waweze kufanya kazi zao vizuri ili kuweza kutukwamua.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaiunga mkono Serikali katika bajeti hii na ninadhani ni bajeti ambayo inaweza ikatukwamua, kinachotakiwa ni kama tulivyokubaliana kwamba malengo yetu haya tuyapanie ili tuweze kuyafikia. Nina uhakika chini ya timu iliyopo nadhani tutafika huko tunakokwenda.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru na ninaunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. MWADINI A. JECHA:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, nakushukuru wewe kwa kunipatia nafasi na mimi niweze kuchangia katika hoja hizi mbili zilizopo mbele yetu. Hoja ya Waziri wa Fedha na hoja ya Waziri wa Mipango, Uchumi na Uwezeshaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini nadhani wanadamu tuna tabia ya kusahau sana. Itakumbukwa Marehemu Baba wa Taifa wakati wa vita vya Kagera aliwaambia Watanzania tufunge mikanda. Wakati Waziri wa Fedha anawasilisha bajeti yake alisema tukanze mikanda. Leo Mheshimiwa Mbunge anakaidi kauli za Serikali, sijui imekuwa namna gani. Lakini tusameheane, ndiyo mambo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla sijachangia, naomba awali ya yote nizungumzie machache kuhusu kauli ambayo alizungumza rafiki yangu Mheshimiwa Adam Kighoma Malima alipokuwa anachangia hoja hizi mbili asubuhi ya leo.

Mheshimiwa Adam Kighoma Malima alikuwa anashangazwa, anasema kwamba badala ya Kambi ya Upinzani kuwasilisha maoni, imesema inawasilisha Bajeti Mbadala na kwamba haoni sababu kwa sababu Kambi ya Upinzani haina Serikali. Lakini nataka Bunge lifahamu kwamba unaposema Serikali ya Kambi ya Upinzani hiyo ndiyo *Shadow Cabinet* na inatambuliwa Kikatiba.

Kwa hiyo, kwa namna yoyote ile inapaswa kuwasilisha Bajeti Mbadala ambayo madhumuni yake makubwa ni kuangalia udhaifu wa bajeti ya Serikali, lakini na kadhalika kutoa maoni na ushauri kwa Serikali hasa kukubali Serikali au kukataa ni wajibu wake mwingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nadhani hili rafiki yangu Adam Kighoma Malima labda alipitiwa, na nadhani sasa ipo haja inaonekana kwamba baadhi yetu hatufahamu wajibu wa Kambi ya Upinzani na inawezekana pia wengi wetu hawatujui maana ya siasa ya vyama vingi. Naomba Bunge lako Tukufu liandae semina tuelimishwe nini siasa ya vyama vingi na nini wajibu wa Kambi ya Upinzani katika Bunge la Vyama vingi. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mbunge, naomba ukae chini. Mpaka sasa Kanuni zetu hazitamki Bajeti Mbadala, zinatamka maoni ya Kambi ya Upinzani. Kwa hiyo, tunapoendelea kutunga Kanuni labda hilo lizungumzwe hivyo. Lakini mpaka sasa hatuna Kanuni inayotamka Bajeti Mbadala ila ni maoni ya Kambi ya Upinzani. Naomba tuelewane hivyo. *(Makofi)*

**MHE. MWADINI A. JECHA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante ingawa ujumbe umeshafika.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani katika hotuba zake mbili imeishauri Serikali kuangalia vyanzo vya mapato vile ambavyo ama Serikali haikuviona au kwa bahati mbaya imeviacha.

Kwa maana hiyo, Serikali ya Kambi ya Upinzani ilikuwa inajaribu kuangalia namna ambavyo inaweza kuleta unafuu kwa wananchi badala ya kuweka kodi katika mafuta iwe mafuta ya taa, petroli au dizeli badala yake iwe inaangalia vyanzo vingine ambavyo kwa sasa havijaangaliwa vizuri na ambavyo vinaweza kuleta mapato katika nchi na kuwasaidia wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la kupandisha kodi ya mafuta ni rai ya Serikali iliyokuja Bungeni kujadiliwa, wala sifahamu kama kuna siku, kwa sababu kuna watu wanaweza kupotosha hapa kwamba Serikali ilikaa na Waheshimiwa Wabunge kupanga kodi za mafuta. Hii sio kweli.

Ninachokumbuka mimi ni kwamba, Serikali ilikaa na Waheshimiwa Wabunge kwenye semina maalum kujaribu kupanga *priorities* za Serikali ili kutekeleza Ilani hiyo ya Uchaguzi ya CCM katika kutekeleza agizo la MKUKUTA. Sasa wanapotosha kwamba Waheshimiwa Wabunge walikaa na Serikali kupanga kodi za mafuta. Naomba wabadilishe usemi wao.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha, ukurasa wa tisa alizungumzia masuala ya *TRA,* akasema kwamba katika kipindi cha Julai, 2006 hadi Machi, 2007 mapato ya ndani yalifikia shilingi trilioni 2.0 sawa na asilimia 81.4 ya bajeti ya Serikali. Lakini kadhalika ni sawa na asilimia 109.7 ya matarajio yaliyowekwa. Hii ni hatua nzuri na kwa kweli ni hatua ya kupongezwa.

Mimi naungana na wenzangu kuipongeza *TRA* kwa kazi kubwa ambayo wanaifanya. Lakini tukubali kwamba popote ambapo pana mafanikio, kadhalika kuna matatizo. Napenda niseme kwa sifa kubwa kwamba wafanyabiashara wanaofanya biashara baina ya Zanzibar na Tanzania Bara wanapata matatizo makubwa ya kupata *double taxation*. Wanatafuta mizigo yao kule Zanzibar na baadaye kuamua kupeleka Tanzania Bara wanatozwa ziada ya kodi ambapo tuliambiwa kwamba viwango vya kodi baina ya Zanzibar na Tanzania Bara vilikuwa tofauti. Tukaambiwa katika Bunge hili watafunga mitambo na kuweka mfumo mpya wa kodi ambao unaitwa *SCUDA++* na mfumo huo wa kodi unatumika Zanzibar, nadhani sio chini ya miezi nane iliyopita, lakini hadi leo wafanyabiashara wanaofanya biashara baina ya Zanzibar na Tanzania Bara wanatozwa ziada ya kodi ya bidhaa zao.

Hili ni tatizo na nadhani ni miongoni mwa kero ambazo zinapashwa kujadiliwa katika kero za Muungano kwa sababu ni bora kufanya biashara baina ya sehemu hizi mbili zenye Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, tuje kwenye magari ambayo Mheshimiwa Khadija amezungumza. Mimi nitazungumza kwa upande wa pili. Ukiteremsha gari yako Zanzibar na ukapenda kutumia gari ile Tanzania Bara nataka niseme kwamba sisi Wabunge wengi wa Zanzibar tumetoa gari zetu Zanzibar pale kuleta Dar es Salaam ili kutumia baina ya Dar es Salaam na Dodoma kurahisisha usafiri. Lakini taabu ambayo tumeipata kwanza ile *double taxation* imetukuta, lakini la pili gari ikishuka na ZNZ haitakiwi kuonekana barabarani inatembea. Mimi huwa najiuliza Zanzibar ni nchi gani?

Yamenikuta na nasema kwa uhakika kabisa kwamba nilishawahi kuleta kama mara tatu gari yangu ZNZ kuja Dar es Salaam nikakamatwa, kwa nini natembea na gari ya ZNZ. Sasa Zanzibar ni nini? Ni nchi, ni hadithi ya nchi au ni nini?

Tunasema Zanzibar ni sehemu ya pili ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mtanzania ana haki ya kuishi mahali popote ili mradi havunji sheria za nchi, lakini inakuwaje leo gari ya Zanzibar ipate kibali cha kununua Dola 25 kwa miezi mitatu nadhani! Alipie Dola 25 kupitia katika barabara za Tanzania Bara, kwa nini? Kuna uhalali gani wa kumnunulisha mtu kibali kutembeza gari ya sehemu ya pili ya Jamhuri ya Muungano kwenda sehemu ya pili ya Jamhuri? Uhalali huo uko wapi?

Mimi nadhani kero ndogo ndogo kama hizi Mheshimiwa Waziri Mkuu mnapokaa na Mheshimiwa Waziri Kiongozi naona mziangalie vizuri. Ni adha, ni usumbufu na uonevu. Hii hadithi ya vibali nadhani vipigwe marufuku kuanzia leo. Itakuwaje wewe mtu ununue kibali uko nchini kwako? Gari ya Burundi ikate kibali, Rwanda, ikija Tanzania itake kibali, Kenya ikienda Tanzania ikate kibali basi na Zanzibar pia!

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye hotuba ya Waziri wa Mipango, Uchumi na Uwezeshaji kwenye ukurasa wa 45. Mheshimiwa Waziri alipokuwa anazungumzia Mpango wa Mwaka 2007/2008 mambo ambayo Serikali inalenga katika Sekta ya Nishati nilikuwa naangalia ule mradi ambao umeanzishwa hivi karibuni wa kupeleka umeme Pemba kupitia Tanga. Nimeutafuta sikuuona. Sasa napata wasi wasi nikijua wazi kwamba Kisiwa cha Pemba ni kisiwa ambacho kina matatizo makubwa ya umeme. Wamekuwa wanatumia *generators* ambazo zilifungwa nadhani wakati wa Rais wa Awamu ya pili ya Zanzibar kama sio ya tatu. Zimechoka *generator* zile, zina-*drain under capacity* na wakati wote ni spana mkononi, matokeo yake ni kwa kila wakati Pemba umeme ni wa mgao.

Mheshimiwa naibu Spika, Serikali kwa makusudi mazima iliamua kutoa umeme Tanzania Bara kuupeleka Pemba kuwaondolea wananchi wa Pemba matatizo ya umeme. Ninavyofahamu, huu mradi umeshaanza, lakini kwa sababu sikuona katika vitabu hivi, napata wasiwasi kwamba labda umeachwa njiani. Mheshimiwa Waziri wakati akifanya majumuisho labda aniambie huu mradi umesita, umeachwa au imekuwaje?

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ibara ya nne, ibara ndogo ya tatu naomba kunukuu. "Kwa ajili ya utekelezaji bora wa shughuli za umma katika Jamhuri ya Muungano na kwa ajili ya mgawanyo wa madaraka juu ya shughuli hizo baina ya vyombo vilivyotajwa katika ibara hii, kutakuwa na mambo ya Muungano kama yalivyoonyeshwa katika nyongeza ya kwanza iliyokuwemo mwishoni mwa Katiba hii na pia kutakuwa na mambo yasiyo ya Muungano pamoja na mambo mengine yote yasiyo mambo ya Muungano." Tukija katika nyongeza ya kwanza kwenye *item* ya 11, utakuta kumeandikwa bandari, mambo yanayohusika na usafiri wa anga, Posta na Simu. Nimejifunza kutoka katika ibara hii na kwa mambo haya ni mambo ya Muungano na kwa vyovyote vile yanahitaji mtazamo katika Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka nikwambie kwamba pamoja na Bunge lako Tukufu, Uwanja wa Ndege wa Zanzibar unahitaji kuboreshwa sana. Uwanja ni mbovu, uwanja una mashimo, *runway* ni fupi lakini kadhalika na majengo ya Kiwanja ni mabovu na hayastahili kupokea hata wageni wa nje ambao tunawaita ni watalii katika nchi yetu. Lakini Uwanja uliopewa jina la Muasisi wa Mapinduzi ya Zanzibar wa Karume uliopo Pemba, uwanja huu umesahauliwa kwa muda mrefu.

Mheshimiwa Naibu Spika, uwanja unahitaji matengenezo makubwa, unahitaji kuongezwa *runway*, majengo yote yamekuwa hayafai, yanavuja. Nadhani Serikali ilione hili kuwasaidia wananchi wa Kisiwa cha Pemba na Kisiwa cha Unguja viwanja hivi viwili vya ndege vipanuliwe, viongezwe vifaa vifikie *standard* ya kwa nini viwanja ambavyo vinapokea ndege kubwa kwa ajili ya kukuza utalii wa Zanzibar na kukuza uchumi wa Zanzibar.

Mheshimiwa Naibu Spika, kadhalika kwenye suala la simu la kiganjani, kuna baadhi ya Mashirika na Makampuni ya Simu yamewekeza huduma zake kule visiwa vya Zanzibar. Tulikuwa na *ZANTEL* ambayo ilikuwa imesajiliwa kule Zanzibar, nadhani imehama sasa na ambayo ilikuwa imejiimarisha vya kutosha katika maeneo mengi ya kule Zanzibar, lakini bado kuna baadhi ya sehemu *ZANTEL* haipatikani.

Lakini kadhalika *VODACOM* wameanza kuingia sasa, lakini wao pia bado hawajatawanyika vya kutosha na hasa ukiangalia kama maeneo ya Mkoa Kaskazini wa Pemba na nadhani Mikoa ya Kusini na Mikoa ya Kati Unguja bado *VODACOM* haipatikani vizuri. *TIGO* nayo haipatikani sawa sawa katika visiwa vyetu viwili vya Unguja na Pemba na kwa maana hiyo, naiomba Serikali basi ishawishi haya Mashirika ya Simu na Makampuni ya Simu kuongeza huduma zao kule Zanzibar ili mawasiliano ya simu za viganjani iwe imeboreka zaidi ili kuboresha mawasiliano.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna bandari. Alivyozungumza Mheshimiwa Khadija, mimi nazungumza bandari kwamba imekufa na haina uwezo wa kuhudumia meli kubwa. Siku hizi inapokea meli moja kubwa ya mizigo zikifika nyingine, inabidi zifunge nje kusubiri meli iliyotangulia kuteremsha mizigo. Imekuwa ni usumbufu kwa mishale ya meli na hata wenye bidhaa za biashara wameamua mizigo yao kuteremsha Mombasa au Dar es Salaam na kwa maana hiyo, bandari ya Zanzibar imeshindwa kuipatia mapato Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kujiendeshea mambo yake.

Nadhani sasa ipo haja Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuisaidia Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kuhakikisha bandari ya Zanzibar inatengenezwa kwa *standard* ya Kimataifa, lakini kadhalika inapanuliwa kuongeza nia yake ya kuongeza ma-*container* ili kukuza biashara baina ya bandari za *East Africa* na bandari za Asia.

Mheshimiwa Naibu Spika, kadhalika bandari ya Mkoani na bandari ya Wete ni matuta ya bandari, yanasaidia lakini yanahitaji kuboreshwa. Bandari ya Wete meli haifungi mpaka maji yajae. Kwa hiyo, ikichelewa kuingia na abiria kama maji yametoka, abiria wanakaa nje ya bahari. Kadhalika kama inapokea kuchelewa kuondoka abiria wanabaki pale bandarini mpaka maji yajae ndiyo yaweze kuondoka. Nadhani kunahitaji

matayarisho madogo tu ni kufukua ile bandari kama nilivyosema maji yanaingia zinakaa meli zinaingia wakati wote na kutoka bila usumbufu kwa abiria.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka nimalizie kwa kibwagizo kimoja kidogo. Jana rafiki yangu mmoja alikuwa anazungumzia goli la *penalt*y, akasema, *penalty* goli lake halikataliwi. Lakini kocha Bendera amenifundisha kwamba ukipiga *penalty* ikigonga mwamba ikarudi uwanjani ukaja kuipiga ukafunga, hilo sio goli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru. *(Makofi)*

**MHE. MWANAWETU S. ZARAFI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi nami kuchangia maoni katika bajeti hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza natoa shukrani kwa Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kufika leo hapa katika Bunge hili. Pili, natoa shukrani kwa wale wote ambao walinisaidia wakati nilipopata ajali mwezi wa pili baada ya kumaliza Bunge hili tarehe 14 na kupotelewa na binti yangu. Nawashukuru sana hasa viongozi wa Mkoa wa Pwani na Ikwiriri, Polisi. Shukrani ziwafikie Katibu wa CCM, Mary Nchimbi ambaye alijitolea kunipeleka hospitali mimi na familia yangu na kuacha shughuli zake. Pia natoa shukrani kwa wale Wabunge ambao walihudhuria kwenye mazishi ya binti yangu ambaye alifariki kwenye hiyo ajali na pia kuja kunifariji katika msiba huo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kitu cha kwanza ninachotaka kuzungumza hapa ni kuwa, naamini kwamba kila mtu ana haki ya kusema kile anachojisikia ili mradi asivunje sheria. Kama anaona vinafurahisha na bila kujali kama vinamuudhi mtu mwingine, lakini asivunje sheria. Hivyo basi, sisi Kambi ya Upinzani tutazungumza, tutakosoa, tutatekeleza yale ambayo tutakosolewa na wenzetu, tuko tayari kukubali kukosolewa kwa yale ambayo tunayaeleza bila utaratibu ili mradi tu tunatekeleza yale matakwa ya wananchi ambao ndio wametuleta hapa.

Mheshimiwa Naibu Spika, sina mengi ya kuzungumza kilio changu, ni kile kile cha watu wa Kilwa. Kilio changu cha kwanza ni kwamba sisi Kilwa sio maskini na Mkoa wetu sio masikini, narudia kwa mara nyingine tena. Mkoa wa Lindi una raslimali za aina zote kuanzia bahari, fukwe, misitu ya hifadhi, madini na hivi sasa wamegundua mafuta, lakini tatizo lililopo naomba kumweleza Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa siku ya leo naomba anisaidie.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri Mkuu, Halmashauri ya Kilwa ilileta *bylaws* ambazo zilipelekwa TAMISEMI na mimi nilijaribu kufuatilia. Zililetwa TAMISEMI kabla sijaacha kazi na kuwa Mbunge nikiwa pale kama mmoja wa Wakuu wa Idara. Lakini hadi leo hii hizo *bylaws* bado hazijaletwa Kilwa. Sasa sisi watu wa Kilwa tutawezaje kupata mapato wakati hatuna hata zile *bylaws* ambazo zitaturuhusu tupate yale mapato madogo madogo?

Mheshimiwa Naibu Spika, ninachoomba leo hapa, sina maelezo zaidi kwa sababu zilikwenda TAMISEMI na kule tukiulizia tunaambiwa ziko Ofisi ya Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Waziri Mkuu nakuamini kwamba wewe unafanya kazi masaa 24 na ninakuamini, siku moja nimepanda ndege tukiwa na wewe tukitokea Mnazibay. Tukiwa wote ulikuwa unaletewa faili ukiwa ndani ya ndege kufanya kazi. Kwa maana hiyo, ninaamini kwamba na *bylaws* zetu pindi nitakapotoka hapa Bungeni aidha nitapewa kwamba zimekubalika au nikifika nitazikuta zimefika katika Halmashauri ili tuweze kuingiza mapato katika Halmashauri yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ambalo ningependa kulizungumzia, ni kama alivyozungumza mwenzangu; binadamu tuna hali ya kusahau. Mheshimiwa Mbunge aliyepita amezungumza kwamba kufunga mkanda sio sera ya CCM, lakini nakumbuka bajeti hii Mheshimiwa Waziri wa Fedha ndiye aliyezungumza ili kuonyesha ugumu wa bajeti uliopo. Kwa misingi hiyo, nasema hivi kinachosemwa na Waziri ni usemi wa Serikali. Kwa hiyo, hakuna haja ya kupotosha usemi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu suala la vibali vya uchimbaji wa madini, kama nilivyosema, Kilwa hatuna matatizo ya raslimali. Kinachotushangaza watu wa Kilwa, vibali vinatolewa vya kuchimba madini vya wachimbaji wadogo wadogo bila ya wananchi kufahamu wanashtukia tu kwamba watu wanachimba madini. *Gypsum* hakuna kinachoingia Halmashauri, Wanakijiji hawana taarifa yoyote jamani ile sheria ya kuwapa madaraka wananchi, imepelekwa wapi au ipo katika Mikoa mingine isipokuwa Kilwa?

Naomba hili liangaliwe, wananchi wa Kilwa pia wanahitaji kupata mafanikio kutokana na raslimali zao. Kwa hiyo, kama kuna chochote na kama wanatoa vibali kwenye Kanda ya Kusini, basi wananchi waelewe kwamba mahali pale panachimbwa kitu gani, panafanyiwa nini ili waweze kupata mapato yao kutokana na raslimali zinazowahusu. Hili suala la kuitwa Wilaya ya Kilwa masikini, limetuchosha kwa sababu sisi sio masikini. Naomba hili liangaliwe ili na sisi pia tuwe na mafanikio kama maeneo mengine ili litutoke hili suala la kuitwa masikini katika Mikoa yetu ya Kusini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kitu kingine ninachotaka kuzungumzia ni kuhusu mwekezaji wa gesi ya Songosongo. Kama alivyotangulia kusema Mheshimiwa Hasnain Dewji, kwamba mwekezaji huyu ana majibu ya kushangaza. Mimi mwenyewe nilikuja na nyaraka ambazo sikuwahi kuzifikisha hapa, zimepotea kwenye ajali.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuja na nyaraka ambazo mwekezaji huyu amepeleka Halmashauri kukataa kwamba yeye amepewa *exemption* kwenye gesi ya Songosongo. Kwa hiyo, hana haki ya kuipa Halmashauri kitu chochote wala senti yoyote kuhusu kodi ya Songosongo kuhusu gesi. Kwa misingi hii, nashindwa kuelewa. Hii barua inaonyesha kwamba ilitolewa kutoka Ofisi ya Wizara ya Fedha akiwepo Mheshimiwa Basil Mramba wakati huo.

Mheshimiwa Waziri naomba hili liangaliwe kwa sababu sisi Halmashauri ya Kilwa tusiwe omba omba. Tukiomba hela ya mchango, tunakwenda tu kuomba, lakini tunajijua kwamba hatuna haki kwa sababu nyaraka zinaonyesha wazi kwamba hatuna chochote cha kumwambia mwekezaji yule. Kwa hiyo, naomba hilo liangaliwe na nafikiri katika mikataba inayotakiwa irekebishwe mmojawapo uwe wa gesi ya Songosongo ili na sisi tuweze kupata mapato ya eneo lile. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nitaongelea kuhusu Madiwani na naliongelea hilo kwa sababu na mimi ni mmoja katika Madiwani katika Halmashauri ya Wilaya ya Kilwa, Madiwani wana kazi kubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi kama Wabunge tunayo kazi, lakini wao wana kazi kubwa kwa sababu wao wanakaa kwenye maeneo yale muda wote wakati sisi tukiwa Bungeni. Kazi nyingi wanazifanya wao na wanazifanya hizi kazi wakitembea kwa miguu kwenye maeneo yao.

Muda mwingine zile posho ndogo wanazopata wanazitumia kwa nauli kwenda kwenye eneo la wananchi ili kuhamasisha maendeleo. Lakini cha kushangaza hatuoni ongezeko lolote la posho ya Madiwani! Posho zao ziko pale pale wakati kazi wanazozifanya ni kubwa na wakati mwingine wanatumia fedha zao za mifukoni ili kuweza kuhamasisha wananchi kwenye kazi za maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa naiomba bajeti hii iwawekee angalau Madiwani posho kila mmoja apate Sh. 100,000/=, sio vile tunawapa Sh. 30,000/= kama vile tunawafikiria. Zaidi ya hapo kwa wale ambao huwa wanakwenda Majimboni maana sio wote tunakwenda Majimboni mara kwa mara wanaweza wakaamini kwa kiasi kikubwa jinsi gani Madiwani hawa wanafanya kazi kwenye maeneo yale.

Mheshimiwa Naibu Spika, tulielekeza kipindi fulani kwamba kila Halmashauri iwaongezee posho Madiwani lakini hali halisi za Halmashauri nyingi hazina uwezo wa kutoa posho kuwaongezea Madiwani. Kwa hiyo, hapa hakuna uwiano Madiwani wa Dar es salaam au sehemu nyingine ambayo inaingiza mapato kwa wingi, wanapata fedha kwa wingi wakati Madiwani ambao wako kwenye maeneo mengine ambayo kipato chao kidogo wanapata fedha kidogo wakati kazi wanazozifanya zinafanana. Kwa hiyo, ombi langu ni hilo, naomba Serikali iwafikirie Madiwani hao.

Mheshimiwa Naibu Spika, kila mtu anafahamu au kwa wale wanaosoma miongozo kwamba katika nchi zote za Jumuiya ya Madola bajeti yao ya Wapinzani kunakuwa na bajeti mbadala, lakini sisi hatujali isiitwe mbadala, na iitwe Maoni ya Kambi ya Upinzani. Kwa hiyo, ninachotaka kuzungumza ni kwamba hili lieleweke na kama watu hawasomi magazeti, sisi hatuko kwa ajili ya kubadilisha bajeti, isipokuwa ni kutoa maoni tu.

Kwa hiyo, kila Mbunge nafikiri pamoja na kwamba *internet* zinaonekana kwamba sio kitu cha maana, lakini wasome *internet* na waelewe katika maeneo mengine ya nchi wananchi au Wabunge wa maeneo hayo huwa wanaishi vipi kwenye Kambi za Upinzani na Chama Tawala? Kwa hiyo, hili lieleweke kwamba sisi tunachofanya hapa sio kosa labda kosa ni hilo la kuitwa Bajeti Mbadala, badala ya kuita Maoni ya Kambi ya Upinzani. Waliangalie hilo wasione kwamba sisi tunaloongea hapa ni kwamba kazi yetu ni kuharibu, hatupo kwa ajili ya kuharibu tunataka kutengeneza.

Mheshimiwa Naibu Spika, demokrasi inasema hivi: “Una haki ya kufuata chama chochote unachokipenda, lakini pamoja na kufuata chama chochote unachokipenda,

maendeleo ya nchi hii ni ya Watanzania wote." Kwa hiyo, sisi hapa tuko kwa ajili ya maendeleo ya wananchi wote wa Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, sina maelezo zaidi, isipokuwa maombi yangu ni hayo. Nasisitiza kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu atusaidie Kilwa ili na sisi pia tutoke kwenye ramani ya Tanzania sio ramani ya umaskini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. *(Makofi)*

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kukushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kushiriki katika mjadala huu wa bajeti ya Serikali. Kwanza napenda niwapongeze sana Waheshimiwa Wabunge ambao wametoa hotuba zao tangu mjadala huu ulipoanza. Wengi wao kwa kweli wametoa hotuba nzuri na wametoa michango ya msingi ambayo ningependa niwapongeze sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wabunge wengi walichangia katika eneo la maliasili na nimeona ni vyema nikatoa maelezo kidogo kama sehemu ya Serikali ya majumuisho ya bajeti hii na ningependa niongelee katika maeneo makuu matatu. La kwanza ni juhudi za Seikali katika kutangaza utalii.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilipokuwa najibu swali Na. 34 la Mheshimiwa Parmukh Singh Hoogan nilieleza kwa kifupi juhudi za Serikali za kutangaza utalii. Juhudi hizi zinahusu kupeleka wataalamu katika masoko ya utalii Duniani na Serikali inachangia pamoja na sekta binafsi kutengeneza mabanda kule katika masoko hayo na watu wa sekta binafsi wakiwemo na wafanyabiashara wa Kitanzania wengi wanaokuja katika mabanda hayo na kutafuta wateja wa utalii katika msimu wa utalii unaofuatwa.

Tangu Januari, 2007 tumehudhuria masoko ya *World Travel Market* huko London na kulikuwa na *exhibitors* wa Tanzania zaidi ya 55. Tulihudhuria maonyesho ya *TIB Milan, Fittur Madrid, ITB Berlin, New York Times,* tulifanya *Road Show* kule Marekani, Mjini *New York* tulifanya *Road Show* D*allas Texas* na *San Diego California*. Mwaka huu mwezi Septemba, tutafanya *Road Show* katika nchi za Ujerumani, *Austria* na *Switzerland*.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika juhudi hizi tumeitangaza Tanzania pia katika magazeti ya kila siku katika nchi za Marekani, tumetangaza kwenye *column* ya usafiri katika gazeti la *New York Times* na Uingereza, tumetangaza katika gazeti la *The Herald* na katika magazeti katika mji wa *Dallas*, *San Diego* na Ujerumani. Pamoja na matangazo hayo katika magazeti ya kila siku tumefanya matangazo katika majarida ya safari.

Hapa nina majarida ya mwezi Juni peke yake ambayo yametoka na yana taarifa za Tanzania. Ningeleta ya Januari, Februari, Machi, Aprili, Mei ingekuwa mzigo mkubwa. Ningependa niseme kwamba juhudi zetu ni kutangaza utalii katika nchi ambapo watalii wanapotoka. Katika jarida hili ambalo ni moja ya majarida yanayosomwa na matajiri

wakubwa duniani na yanayotumiwa katika kuchagua maeneo ya kusafiri, tunalo tangazo hapa la kurasa 21 ambalo thamani yake ni Dola za Marekani milioni 2.5.

Mheshimiwa Naibu Spika, mtakumbuka kwamba bajeti ya *TTB* ni Dola 1.5 milioni. Hivyo tangazo tumelipata kwa kutumia ubunifu, Mashirikiano mazuri na nchi za kigeni na uzoefu wa viongozi mbalimbali Serikalini kuweza kupata watu wa kulipia matangazo hayo. Tangazo hili linazunguka Marekani, Canada, *Western Europe* na maeneo mengi ambapo watalii wanatoka.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninalo tangazo lingine hapa la jarida la mwezi Juni, huko Italia na lenyewe limeitangaza Tanzania, limetangaza Serengeti, *migration* na ndani humu limetangaza Zanzibar *Stone Town*. Hapa ninayo majarida mengi ambayo yametangaza hili na wale ambao wanapenda kuona ni jinsi gani tunaitangaza Tanzania katika majarida mbalimbali tunawakaribisha katika ofisi zetu ili muweze kuja na kukagua.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuanzia mwezi Agosti, 2007 nilieleza Bunge lako Tukufu kwamba tutaanza matangazo katika Televisheni ya *CNN* ambayo tutaweka matangazo katika *CNN America, CNN Headline News*, *CNN Travel* na *CNN Airports*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, itakapofika mwezi Septemba mwaka huu, tumekubaliana na *Africa Channel* ya Marekani ambayo itaanza kutangaza matangazo yake katika Kituo cha Matangazo ya Televisheni cha *Sky News* waweze kuitanga Tanzania kupitia katika matangazo hayo. Pamoja na juhudi hizi viongozi wetu wakuu wamefanya kazi kubwa sana ya kuitangaza Tanzania. Napenda kwa pekee kabisa nimshukuru Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete Rais wetu kwa kuitangaza Tanzania kwa juhudi kubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mwezi Septemba mwaka jana Mheshimiwa Rais alifanya juhudi kubwa sana ya kuitangaza Tanzania Marekani na baadaye alifanya juhudi kubwa ya kuitangaza Tanzania katika *Africa China Summit* ambayo ilifanyika Mjini Beijing. Juhudi hizi zimefanyika Uingereza, Korea, Japan na nchi nyingine. Matokeo yake ni kwamba *African American Institute* ititangaza Tanzania kwa wiki nzima mwezi Septemba mwaka huu na kumtunuku Rais wetu katika kazi hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, Rais atashiriki katika *Wild Talk Africa* itakayofanyika Johannesburg mwezi August mwaka huu ambayo itatangazwa na vituo vikuu vya televisheni vya *CNN, BBC, Sky News, Al-jazeera* na kadhalika. Katika kufanya hivi, watalii wataongezeka na tutaongeza mapato kufikia karibu Dola bilioni 2.0 ifikapo mwaka 2010. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la pili ambalo ninataka nilizungumzie ni suala la magogo. Mwaka 2004 kulikuwa na wimbi kubwa sana la kuvuna magogo katika nchi yetu, uvunaji huo ulikuwa haramu na ulikuwa unafanyika kwa kiasi ambacho kama kingeendekezwa, misitu yetu yote ingepotea. Kwa hivi Serikali kutumia Sheria ya misitu

ya mwaka 2004 ilisimamisha uvunaji huo. Uvunaji na usafirishaji haramu wa mazao ya misitu ulitokea na ni kweli kwamba tangu wakati ule watu wengi wamesafirisha, wamevuna na kusafirisha mazao ya misitu kwa njia haramu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kazi ambayo Serikali imeamua kufanya ni kwamba kuanzia wiki ijayo, *Commissioner General* wa Tanzania wa *TRA*, atakutana na Makamishina *Generals* wa China, Japan, India Thailand na Korea kuhakiki na kukokotoa ni kiasi gani cha mbao kutoka Tanzania kimekwenda huko ili kufuatilia ni akina nani wamepeleka mbao hizo na kuweza kuzifuatilia ili wenyewe waweze kulipa mapato ambayo yaliweza kupotea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali pia imeamua kusimamia kidete utaratibu wa kuvuna misitu, kusafirisha na uuzaji wa bidhaa za misitu. Aidha, Serikali imepiga marufuku kuuza magogo nje ya nchi. Hatua hii inatokana na ukweli kwamba kama tutakuwa tunauza magogo watu katika nchi ambazo hazina misitu hawawezi kuja kuwekeza hapa. Kwa hiyo, magogo hayatauza nje wale wanataka kuyatumia waje nchini wawekeze kuongeza thamani kwa kuyapasua na kuleta ajira hapa nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika usimamizi wa uvunaji wa magogo tumekokotoa kiasi cha magogo ambacho kitavunwa katika mwaka ujao wa fedha katika misitu ya kupanda na katika misitu ya asili. Katika misitu ta kupanda na kwa kubadilisha mrahaba wa mbao na magogo, Serikali imekadiria kupata Shilingi bilioni 34.59 na kutoka katika misitu ya asili Serikali imekadiria kupata shilingi bilioni 10.575, jumla ya shilingi bilioni 45.6.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika suala la uwindaji, hili ni suala ambalo ninataka nilizungumzie. Serikali imeangalia biashara nzima ya uwindaji wa kitalii na nitaeleza kwa kinaganaga zaidi katika Bajeti ya Wizara ya Maliasili na Utalii, lakini ili kuhakikisha kwamba Tanzania inafaidika na uwindaji wa kitalii tuliangalia bei mbalimbali za biashara ya uwindaji wa kitalii kuangalia kazi iliyofanywa na Kamati maalum ambayo iliundwa na Waziri wa Maliasili na Utalii na kubadilisha bei za uwindaji kulingana na bei za nchi majirani na Soko la Dunia. Kutokana na mabadiliko haya, Serikali inategemea kupata shilingi bilioni 33.355. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, najua kwamba muda utakuwa umekwisha, lakini nadhani haya mengine yaliyobaki nitayatoa katika Bajeti ya Waziri wa Maliasili na Utalii.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kama nilivyosema, orodha ya wachangiaji wetu katika Hotuba ya Bajeti na Hotuba ya Uchumi na Mipango imekwisha.

Kwa hiyo, kesho asubuhi kutakuwa na kipindi cha maswali kama kawaida na baada ya kipindi cha maswali Waziri wa Mipango, Uchumi na Uwezeshaji ataanza kujibu

hoja zinazomhusu kwa muda wa saa moja halafu na Waziri wa Fedha atajibu kwa muda wa saa moja na baada ya hapo mtahojiwa lakini tutaingia kwenye kupiga kura.

Kwa hiyo, ni tegemeo langu kwamba kesho kila Mbunge atakuwemo humu ndani kuweza kutimiza wajibu wake wa kikatiba wa kuweza kupitisha Bajeti ya Serikari. Kwa hiyo, muambizane huko na walio mbali nao warudi. Kazi hii ya upigaji kura itafanyika katika kipindi cha asubuhi. Kwa hiyo, nategemea kwamba wote mtakuwepo ndani ya Bunge.

Tangazo la pili, naomba kuwakumbusha Wabunge wa Chama cha Mapinduzi kwamba baada ya kuahirisha kikao hiki, wakutane kwenye Ukumbi wa Msekwa kwa ajili ya kikao chao.

Kwa hiyo, baada ya kusema hivyo Waheshimiwa Wabunge sina matangazo mengine nawashukuru sana kwa kazi iliyofanyika siku ya leo nawatakia jioni njema. Naahirisha kikao mpaka kesho saa tatu asubuhi.

*(Saa. 1:08 usiku Bunge liliahirishwa mpaka Siku ya Ijumaa, Tarehe 22 Juni, 2007 Saa Tatu Asubuhi)*